Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 02 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani juu ya muhtasari wa Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 23

Kero ya Kuwekwa Vizuizi Mlangoni kwa Abiria Wanaofika na kutoka Uwanja wa Ndege wa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejidhatiti kuhakikisha kuwa wananchi wake hawapati usumbufu wanapotaka huduma mbali mbali. Ukweli huo upo kinyume na hali inayoendelea uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Aman Karume Zanzibar, ambapo kwenye mlango wa kutokea nje ya uwanja kwa abiria wanaowasili, kumewekwa mkanda wa kuzuiwa kupitga na badala yake abiria anatakiwa azunguke upande wa kushoto mwa mlango ili atoke nje, hali ambayo inawasumbua abiria waliochoka na safari, nyengine kutoka mbali.

Kwa nini mlango ule umewekewa mkanda wa kuzuia abiria wanaowasili wasipite lakini wafanyakazi wa Uwanja wa Ndege wanapita.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 kama ifuatavyo.
Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kama alivyoeleza Mhe. Mjumbe kwamba kumejitokeza suala la usumbufu katika suala zima la utokaji wa abiria wetu katika uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Aman Karume uliopo Kisauni Zanzibar.

Uwanja ule kwa sehemu kubwa ya mabadiliko yake hasa ya kimaendeleo yanalenga kuimarisha na kuboresha huduma stahiki ikiwa ni pamoja na huduma zenyewe za miundombinu ndani ya eneo husika na nje ya eneo husika. Hivyo baada ya kukamilika ujenzi wa maeneo wa wasindikizaji na kupunguza baadhi ya ofisi katika eneo lililozunguruka jengo la uwanja, tatizo linalozungumziwa hapa limechukuliwa hatua.

Tukumbuke lengo kubwa la *Zanzibar Airport Authority* ni usalama wa abiria na kuwaondoshea usumbufu likiwemo suala sugu la msongamano wa abiria wanaotaka kuingia uwanjani na wale wanaotoka. Kwa kuwa maeneo yale yapo karibu sana ndio maana ikaamuliwa eneo la Kusini watumie wanaowasili nchini na eneo la Kaskazini watumie wanaokusudia kusafiri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa *ICAO* kwa maelekezo yake yaliomo katika nyaraka, yaani *Annex 9* inayohusiana na masuala ya *Facilitation* katika *airport* na *Annex 17* inayohusiana na masuala ya *security* inawataka wasafiri wanaoingia na wanaotoka wasikutane.

Kutokana na maelekezo hayo katika taratibu za kiusalama, nyaraka hizo uongozi wa uwanja unatakiwa kudhibiti mtiririko wa abiria, yaani *passenger flow* wanaoingia na wanaotoka na kuhakikisha kuwa hawakutani.

Aidha, kunakuwa na msongamano mkubwa wa abiria na watu wanaofika uwanjani kwa ajili ya kuwapokea abiria hao nao pia wanatakiwa wawazuiwe.
Mhe. Naibu Spika, kutokana muundo wa jengo letu la abiria pamoja na udogo wake, kuna uwezekano mkubwa wa abiria hao kukutana. Ili kunusuru mkutano huo ndio maana ikafanyika hivyo abiria wote wanaotakiwa kupita kushoto wanapotoka nje. Uamuzi huo umelenga kuimarisha huduma na uboreshaji na taratibu katika wafanyakazi pamoja na wasafiri wetu.

Mhe Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuuliza maswali mawili ya madogo ya nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba kuna pana usumbufu pale *airport*, ninashukuru kweli pana usumbufu kweli ...

Mhe. Naibu Spika: Inamia kipaza sauti ili tusikie.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ulichosema kuwa kuna sehemu ya kuingilia wanaweza kukutana. Ninavyokumbuka mimi Mhe. Naibu Waziri mlango wa kuingilia na kutokea mbali. Lakini pale mimi nilitaka kukwambia Mhe. Naibu Waziri kama haitowezekana basi tufanye ziara mimi na wewe kwa makusudi, kwa kweli wananchi wanateseka na hakuna sababu ya msingi kuweka mkanda ule.

Mimi ninafikiri tufanye siku uende ukaone *physically* wala sitaki kushindana kubishana asubuhi yote hii, lakini kwa kweli wananchi wanateseka na wanasumbuka. Kama hapa hapatoshi Mhe. Naibu Waziri leo miezi sita mtu anachukua zawadi zake kama embe au mabungo anatoka nayo Pemba ameshaya-*pack* kufika pale anafunguliwa upya, hakuna *x-ray* sababu gani. Sijui suala hili kama linavyoeleza hivi kuq ni usumbufu kitengo kile cha uwanja wa ndege kinawatesa wananchi tena kwa makusudi, wallahi ninakaribia kulia mimi.

Leo nimeshamkuta mgonjwa mimi anateremka pale na *x-ray* zake, anashushwa kule juu kuliko ngazi hapana hata *wheel chair*, baada ya maradhi mtu anazidishwa maradhi. Serikali hii haipendi kusumbua wananchi. Hapa pana haja leo miezi sita *x-ray* hamna ya kupimia mizigo, mtu akifika pale achukue maboksi yake afunguliwe.

Mhe. Naibu Spika: Swali.

Mhe. Jaku Hashim: Ni lini usumbufu huu utaondoka Mhe. Naibu Waziri. Mimi nikuombe sana kwa sauti ya chini kabisa Mhe. Naibu Waziri watu wanateseka vibaya kweli.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo.

Jambo la kwanza ningemuomba sana Mhe. Mwakilishi asilie. Uongozi ni changamoto, malengo ya serikali ni kuimarisha huduma anyamaze, maana yeye kama ni kiongozi awepo moyo hawa anaowaongoza kwa kuona kuwa changamoto zao anazichukua anazifikisha serikalini na serikali inachukua hatua katika kuimarisha huduma zake.

a) Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwakilishi amezungumzia suala la mlango wa kuingilia abiria pamoja na mlango wa kutokea. Tumeeleza kwamba maeneo ya mlango wa kuingilia ndege kwa wanaosafiri na mlango ambao anapendekeza Mhe. Mwakilishi kwa ajili wanaotoka nje wanaoingia nchini yapo karibu. Kwa mujibu wa taratibu na maelekezo ya *ICAO* si busara kwa mtu anayeingia nchini na yule anayesafiri kukutana. Kwa kutambua kwamba uwanja wetu ni mdogo ndio maana tukatengeneza upande wa Kusini utumike kwa wale wanaoingia nchini na upande wa Kaskazini utumike kwa wanaosafiri nchini ili kuondosha watu wale wasikutane. Kuna faida zake.

Kunakuwa baadhi ya nyakati watu wanaingia na maradhi ya mripuko, maradhi mengine ambukizi ambayo yote wakati watu wale wakikutana munaweza mukasababisha majanga.

b) Pia ameuliza suala la *x-ray*. Ni kweli kwamba wasafiri wanapata taabu uwanja wetu wa kimataifa *x-ray* zinaharibika. Lakini jitihada za mamlaka tayari wameshaingia mkataba na kampuni husika ya Afrika ya Kusini na makubaliano yetu kwamba kabla ya kutengenezwa kwa *x-ray* zile nne ambazo mbili ni kubwa na mbili ndogo, watatahakikisha kwamba wanatupatia wao *x-ray* za kufanyia kazi.

Kwa hivyo nimuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba si muda mrefu *x-ray* hizi zitafika zitaanza kutumika ili kuondoa usumbufu unaotokea kwa wananchi wetu.

c) Watu kushuka eneo la juu kwamba wanasumbuka na mizigo yao. Ni kweli lakini Mhe. Mwakilishi nikuoneshe kwamba jambo hili wizara, *management* pamoja na *board* tumeshakaa tumezungumza tumekubaliana tuone utaratibu mzuri zaidi wa kuona msafiri anapata nafasi nzuri ya kushuka yeye na mizigo ili kuweza kupata nafasi ya kusafiri vizuri zaidi.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Naibu Spika, pamoja majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri swahiba wangu mpenzi, Mhe. Jaku Hashim Ayoub kalia sijui kafanya nini.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninataka Mhe.Naibu Waziri akiri kwamba uwanja wa ndege bado kuna usumbufu wa kutosha kwa abiria wa wanaoshuka na wanaopanda, na sisi wengine tumeshuhudia usumbufu unakwenda na mgonjwa utaratibu haupo mzuri wa namna za *packing*, magari yanapigwa makufuli, atueleze ni lini usumbufu katika uwanja wa ndege utaondoka kwa abiria.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na usumbufu huo siku za nyuma. Lakini sisi wenyewe kama wizara kwa kushirikiana na *management* ya uwanja wa ndege pamoja na *board*, suala hili tumelizungumza na tunaamini kwamba hatua stahiki zitachukuliwa.

Sasa kama hatua hazijachukuliwa tutasema nini ambacho tutakifanya sisi kama serikali dhidi ya huyu ambaye hakuchukua haya maelekezo ambayo yametoka serikalini pamoja na vikao na taratibu na maelekezo ambayo tumekwishakuyatoa kwa wale wahusika watendaji wetu.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwisho ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na usumbufu wote ambao Waheshimiwa Wajumbe wametangulia kusema. Je, huoni kwamba usumbufu huu unatokana na *by laws* ambazo Baraza linawapa Waziri kutunga *by laws* hizo.

Lakini la pili, kutungwa kwa kanuni ndogo ndogo ambazo zinakuwa hazipo *friendly* na watumiaji wa eneo lile, sio kutumia madaraka vibaya ambayo Baraza linakaimu kwa waziri ili kutunga kanuni hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mjumbe anazungumzia suala la *by laws*, kwa maana ya kwamba zile *regulations*. Ni kweli kwamba kwa mujibu wa sheria yetu ile iliyoanzisha *Zanzibar Airport Authority* tunalazimika kama wizara kukamilisha *regulations* zile ili kupata *management* nzuri na *flow* ya utendaji kazi. Na hatua tuliyofikia sasa hivi ni kwamba tuna hizo baadhi ya *regulations* ambazo zipo katika pipe line kuzikamilisha ili kuweza kuwa na utendaji wetu unakuwa mzuri katika *management* na ku-*rugulate* masuala ya usalama pamoja na utumiaji wa uwanja wa ndege.

Lakini jambo kubwa liliopo ni kwamba wakati tumeanzisha mamlaka, mamlaka ile ni lazima itengeneze utaratibu wa kuweza kujiendesha ikiwa ni pamoja kuona ile mamlaka inadumu na kuona kwamba yale malengo

yaliyoanzishiwa yanafanikiwa. Kwa hivyo sio kweli kwamba ukosefu wa *regulations* unakwaza ama mamlaka yake kufanya majukumu yake kwamba tunawasumbua wananchi. tunatakiwa tutengeneze *regulations* ili tu-*facilitate* mambo yaende kwa haraka zaidi.

Lakini majukumu yanayochukuliwa na *management* ya uwanja wa ndege ndio wajibu wake kuona kwamba mamlaka inaendelea kuwepo na huduma zinaendelea kuimarika.

Nam. 62

Kutotumiwa Vyema Wachezaji wa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza.

Kwa kuwa timu za Tanzania Bara kama vile Simba, Yanga na Azam FC, zimekukwa zikiwatumia wachezaji wetu hapa Zanzibar kwenye michezo ya ndani na nje ya nchi na hatimaye huonesha viwango na kufanya vizuri, na kwa kuwa hata timu ya taifa ya Tanzania huwatumia baadhi ya wachezaji wa Zanzibar katika mechi zake nyingi hatimae wachezaji hao hukonga nyoyo za Watanzania wote.

Je, ni sababu gani za msingi zinazopelekea Zanzibar kutowatumia vyema wachezaji wetu hao ndani ya Timu ya Taifa ya Zanzibar na kwenye timu zetu hata ikapelekea kuondoka nchini.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 kama ifuatavyo.
Mhe.Naibu Spika, ni kweli timu za Tanzania Bara kama vile Simba, Yanga, Azam FC na timu nyengine zinawatumia vijana wetu kutoka Zanzibar na hatimae kuonesha viwango na kufanya vizuri hata katika timu ya taifa ya Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, kuondoka nchini wachezaji wetu kwa kwenda kujiunga na timu za nje kunatokana na hali ilivyo sasa duniani ya kuifanya michezo ni sehemu ya ajira. Mhe. Naibu Spika, mbali na hayo katika mazingira ya sasa tuliyonayo ya utamaduni wa kila mchezaji yupo huru kujiunga na klabu yoyote ndani na nje ya nchi. Hii inatokana na kukua kwa kasi soko la mpira wa miguu nchini na ulimwenguni kwa ujumla.

Lakini pia kuimarika kwa vipaji vya vijana wetu ambao sasa wanatambua kuwa michezo ni ajira kwao. Mhe. Naibu Spika, bado wachezaji wetu hawa wanatumika vyema katika timu yetu ya taifa ya Zanzibar Heroes ila katika mashindano hujitokeza matokeo tofauti, wakati mwengine huwa tunafanya vizuri na wakati mwengine huwa hatufanyi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, tayari tumekiagiza Chama cha Soko cha Zanzibar kuhakikisha kwamba timu imara ya Tanzania itakaweza kudumu kwa muda mrefu na hatimaye tutaweza kuipatia ushindi katika michezo ya ndani na nje ya nchi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.
Kwa kuwa wachezaji wa timu ya taifa wanachaguliwa kupitia kamati ya ufundi. Je, ni lini Zanzibar itakuwa na wawakilishi ndani ya *TFF* baada ya muda mrefu Zanzibar kutokuwa na wawakilishi ndani ya chombo hicho.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru na ninaomba nimjibu Mhe.Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

ZFA na *TFF* ni vyama tofauti katika mpira ingawa vyote vinafanana. *ZFA* inasimamia mpira hapa Zanzibar na *TFF* inasimamia mpira Tanzania Bara.
Mpira sio suala la muungano. Kwa hivyo hatuwezi kusema kwamba *ZFA* iwe ni sehemu ya *TFF*. Jambo la kufanya katika masuala kama haya wataendelea kushauriana kwenye suala hili ili kufanya mambo yao vizuri.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri, ana mpango gani wa kuunda timu ya taifa ya watu wenye ulemavu, kwa sababu watu wenye ulemavu wanashiriki michezo mbali mbali kwa kila mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa kuuliza swali hilo. Nataka nimwambie kwamba walemavu wote Zanzibar wanashiriki kwenye bonanza la kila mwaka la michezo tofauti na wala hatuwabaguwi kwa sababu ni walemavu. Nakuomba sana Mhe. Mwakilishi uwe unawahamasisha kwenye mikoa yako ya Unguja na Pemba, ili waweze kushiriki na walemavu wengine ambao wataweza kushiriki kwenye michezo mbali mbali ya Zanzibar.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika kuunda timu ya taifa iliyo bora kwa ajili ya mashindano yajayo ya kimataifa, *TFF* ilianzisha mashindano ya vijana katika kila mkoa Tanzania Bara. Niwapongeze *ZFA* kwa kurudisha mashindano ya majimbo ambayo yanatarajiwa kuanza mwezi wa Augusti. Mashindano haya yana lengo la kutafuta vipaji kwa kila jimbo, ili kuunda timu imara ya Zanzibar Heroes.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia *ZFA* kutafuta mfadhili wa kuendesha mashindano haya na kuondokana na kutegemea fedha za michango za wawakilishi na wabunge?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwakilishi, wewe katika miaka iliyopita ulikuwa umo kwenye *ZFA*, lakini nataka nikuambie kwamba wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Michezo, wako tayari na wanaendelea sasa hivi kukaa pamoja, ili kujua kwamba vijana wetu wana vipaji na kuunda timu mbali mbali ambazo zitatuletea tija hapa Zanzibar.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, swali langu limesema kwamba *ZFA* wamerudisha mashindano ya majimbo, ili kuendesha mashindano haya kwa kuibua vipaji kutokana na kila jimbo katika Zanzibar. Je, wizara na Baraza la Michezo wana mpango gani wa kuwasaidia *ZFA* ili kupata mfadhili kuweza kuendesha mashindano kwa ubora zaidi, kuliko kutegemea michango ya mwakilishi na mbunge.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Michezo na wizara hazijapata ombi kutoka kwa *ZFA* kwamba inahitaji kusaidiwa katika kutafuta wafadhili. *ZFA* ikihitaji wafadhili kupitia kwa wizara, basi wizara wakati wowote iko tayari kuvisaidia vyama vyake vya michezo vyote namna gani ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuendesha *ZFA*. Kwa hivyo, kama amepata penyenye kwamba kuna tatizo hilo, basi awashauri *ZFA* waje Baraza la Michezo na wizarani, na wizara itakaa na kuangalia namna gani ya kutatua tatizo liliopo.

Nam. 22
Tishio la Homa ya Ini Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Homa ya ini imekuwa tishio duniani ambapo kwa mujibu wa Shirika la Afya la Umoja wa Mataifa (*WHO*), watu wapatao 600,000 hufariki duniani kote kwa mwaka kutokana na ugonjwa huu. Hivi karibuni ugonjwa huu umeanza kujitokeza na kuwa tishio hapa Zanzibar.

(a) Je, Wizara ya Afya imeliona tatizo hilo na inawaambia nini wananchi kuhusu chanzo, kinga na tiba ya maradhi hayo.

(b) Je, wizara imejipanga vipi kukabiliana na maradhi hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 22 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, leo nataka nichukuwe nafasi kidogo, univumilie kwa sababu swali hili ni nyeti na ningependa wananchi wafaidike na taaluma nitakayoitoa.

Mhe. Naibu Spika, ugonjwa wa homa ya ini hapa nchini petu upo na chanzo ambacho ni tishio ni kile cha virusi, ambavyo huambukiza kutoka kwa mtu mmoja kwenda mwengine kwa njia ya kugusa damu yenye maambukizi. Inasemekana virusi vya homa ya ini ni hatari zaidi, kwani vina uwezo wa kuishi nje ya mwili zaidi ya masaa 48 tofauti na virusi vyengine.

Njia za maambukizi zinafanana na ukimwi, nazo ni kujamiiana, maambukizo ya mama kwa mtoto wakati wa kujifungua, ikiwa uchungu ni wa muda mrefu na anae mnyonyesha mtoto kama chuchu zitakuwa na vidonda, kupandikizwa viungo kama ini, figo, moyo baada ya viungo vya muhusika kushindwa kufanya kazi, kusafishwa damu mara kwa mara mafigo yakiacha kufanya kazi na kuongezewa damu isio salama kwa alie pungukiwa nayo.

Mhe. Naibu Spika, njia nyengine ni kuchangia mabomba na kujidunga sindano na haya zaidi ni kwa watu wanaotumia madawa ya kulevya, vyombo vya kutolea huduma hospitalini ambavyo havikusafishwa vizuri na kuchemshwa ipaswavyo, kutumia vyombo vyenye ncha kali kama kuchora tatoo na vya kukata kama vijembe vya kunyolea, vifaa vya kutengenezea kucha za miguu na mikono kwa wanaokwenda ma-*saloon* na misuaki hivyo ni vifaa ambavyo hubaki na chembe chembe za damu zinazoonekana na ndicho chanzo cha maambukizi.

Mhe. Naibu Spika, virusi vya homa ya ini vimegawika aina kubwa tano (virus *HAV, HBV, HCV, HDV* na *HEV*) Kati ya hayo ni aina mbili tu B na C ndio ambazo zipo hapa nchini kwetu. Kwa wale wenye kinga imara mwili hupambana navyo na wenye kinga dhaifu huwa wanabaki na virusi hivyo, (*carries*) na ndio wanaoathirika na maradhi haya ambayo huchukuwa muda mrefu bila ya dalili yoyote kujitokeza na hatimae ini huathirika. Asilimia 15 tu ya wanaougua wanapata dalili za ugonjwa na kati ya hao asilima 10-15 ya wagonjwa dalili huondoka wenyewe na hasa kwa vijana na wanawake.

Mhe. Naibu Spika, dalili za homa ya ini ni kukosa hamu ya kula, uchovu wa mwili, kichefuchefu, maumivu ya misuli na viungo, kupungua uzito, mwili na macho kugeuka rangi ya manjano ghafla. Maradhi huchunguzwa kwa njia ya kupima damu au kukata sehemu ndogo ya ini na kuangalia kwa darubini. Asilimia 80 ya wanao ambukizwa na virusi wao wanauguwa kwa muda mrefu usiopunguwa miezi 6. Wengi wao hupata dalili kidogo za ugonjwa au hapati kabisa na baada ya muda mrefu ini hukakamaa (*Cirrhosis*) na kuugua saratani ya ini.

Mhe. Naibu Spika, tafiti hutumia kina mama waja wazito kama kioo cha kiwango cha maambukizi katika jamii. Utafiti wa mwaka 2010 ulionyesha kwamba asilimia 1.3 walikuwa na maambukizo ya homa ya ini ya aina B, na asili mia 0.3 walikuwa na homa ya ini aina ya aina C. Utafiti wa mwaka 2012 kwa waliotumia dawa za kulevya ulionesha kwamba asili mia 5.9 walikuwa na homa ya ini ya aina B na asilimia 25.4 walikuwa na homa ya ini aina ya C.

Takwimu za benki ya damu zinaonesha kwamba, asilimia 2.5 ya damu wanayoikusanya imeambukizwa virusi vya homa ya ini, yaani HBV. Katika kupamba na hilo wizara inahakikisha damu zote zinazowafikia wagonjwa zimetolewa na kitengo cha damu salama ili iweze kupimwa maradhi tofauti kama HIV na homa ya ini.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba tofauti ya HIV na ugonjwa huu, kinga ambayo hupatikana kwa chanjo. Miongoni watu waliopo kwenye hatari ya kupata maradhi haya pamoja na watu wanaojidunga dawa za kulevya, wagonjwa wanaohitaji kuchangiwa damu mara kwa mara kama vile *Sicklers* na wafanyakazi wa afya.

Kukabiliana na maradhi haya wizara imejipanga kwa kufanya mambo yafuatayo:-

1. Kuhimiza watu kutumia condom kama hawana uhakika wa wanachokifanya
2. Kuwapatia chanjo ya maradhi haya watoto wachanga ili kuweza kuwakinga
3. Kuwachanja wafanyakazi wa afya walio hatarini kuambukizwa maradhi
4. Kuwapa wagonjwa dawa za kumeza badala ya sindano
5. Kupunguza maambukizi kwa jamii kwa kutumia vifaa kama bomba na sindano mara moja bila ya kurudia tena
6. Kupima wote wanaochangia damu, na kuhakiki damu yenye

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri na kutupa darsa humu ndani kwa muda mrefu kidogo, naomba nimuulize maswali mawili madogo tu ya nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa ugonjwa huo unahitaji mwamko wa kutosha kwa wananchi.

(a) Je, ni elimu gani ya afya imetolewa kwa wananchi hadi sasa ili tiba iweze kupatikana kwa muda muafaka?

(b) Kwa kuwa idadi kubwa ya wananchi kipato chao ni kidogo cha dawa za kutibu ugonjwa huo na ni ghali. Je, serikali inazo dawa za kutosha ili kuwaondoa wasi wasi wananchi. Isijekuwa kama wananchi wangu wa Jambiani hivi juzi walikuwa wanahangaika kutafuta dawa, baada ya jitihada za mwakilishi na mbunge ndio wakapata dawa, naomba serikali itowe majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, mwamko kwa wananchi unatolewa, elimu kwa kupitia vyombo vyote vya habari inafanyika na wanaokuja hospitalini wanaelimishwa, wanaokuja kutoa damu wanafahamishwa, wanaojichoma dawa za kulevya wamefundishwa na watakaotokea zaidi wataendelea kufundishwa, kwa sababu inatumika hiyo njia hasa katika *Sober Houses*.

Kwa hivyo, elimu ya kutosha ipo. Lakini sasa binadamu ndio binadamu, ukifundishwa leo kesho unasahau. Tutazidi kuendelea kuwakumbusha kadiri siku zinavyoendelea.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la dawa, ni kweli dawa ni ghali na ili liweze kutumika hilo, panahitaji utafiti wa kutosha na ndio tafiti zimeanza kufanywa kama hivyo nilivyozitaja na hicho ndicho kitakachotupa kiwango cha watu wanaoathirika, ili kuweza kufanya makadirio ya dawa hizo.

Lakini dawa ni ghali mno kiasi ambacho katika taratibu za dawa za kawaida ambazo tunaziagiza kwa utaratibu huu hautowezekana. Kwa hivyo, inatakiwa kama miradi mingine tutengeneze miradi baada ya kupata taarifa za kutosha, ili tuweze kuwaomba wafadhili waweze kutusaidia kwa hili.

Suala la dawa za Jambiani kuchelewa kwake, kwa sababu sio Jambiani tu, ni mfumo mzima wa dawa hizi ulikawia kufika, kwa sababu dawa zinaponunuliwa *MSD* zilikuwa hakuna na hatukuwa na njia nyengine ya kufanya mbadala, kwa sababu pesa zilikuwa zimeshakwenda huko. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nashukuru sana kwa majibu ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Nam. 63

Zanzibar Kuwa na Vyanzo Vyake vya Umeme

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la mabadiliko ya tabia nchi yanaendelea kuathirika nchi yetu katika kila sekta, kwa maana ya mazingira uchumi na ustawi wa jamii, na kwa kuwa matumizi ya nishati ya mafuta na kuni yanazidi kuongeza hewa ukaa sambamba na uharibifu mkubwa wa mazingira yaliyotuzunguka.

Kwa kuwa nishati ya umeme imekuwa ghali katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba, kwani nishati hiyo tumelazimika kuinunua kwa bei mbaya kutoka Tanzania Bara.

Na kwa kuwa Zanzibar ni tajiri wa vyanzo mbali mbali vya nishati ukiwemo upepo, maji, jua na nguvu za Ardhi.

Je, ni lini Serikalii itaanzisha vyanzo vyake vya umeme au kuruhusu wawekezaji kufua umeme katika vyanzo vyetu badala ya kutegemea umeme kutoka Tanzania Bara ambao ni ghali sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 63 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kushirikiana na *EU* inafanya utafiti juu ya uanzishaji uzalishaji wa umeme kwa njia ya upepo ambapo utafiti huo umefunguliwa rasmi tarehe 06/05/2014 hapo katika Hoteli ya *Grand Palace Zanzibar*. Baada ya utafiti huo ndipo serikali itatoa taarifa juu ya lini chanzo hicho kitaanza kutumika kuzalisha umeme hapa Zanzibar.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa vyanzo vya nishati ya umeme katika nchi yetu ni vingi sana na vingi vyao inaonesha ni rahisi mno, na kwa kuwa mambo kama *hydroelectric power* kwa Zanzibar inaonekana ni rahisi zaidi ukilinganisha na hiyo *solar electric power*, hata *Geothermal* inaonekana zaidi ni rahisi kuliko hii ya jua.

Je, ni sababu gani za kimsingi zilizowafanya nyinyi wataalamu wa wizara hii, mkaamua kutumia hii *solar energy* badala ya kutumia *Geothermal* pamoja na *hydroelectric power* ambayo ni *available* zaidi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kupitia wizara yangu imeliangalia suala hili, lakini baada ya kufanya utafiti zaidi tumegundua kwamba kutumia umeme wa upepo Zanzibar, ni chanzo ambacho kitatupa maslahi makubwa na ndicho ambacho kitakachokuwa rahisi zaidi kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa madai haya au mazungumzo haya ya kupata umeme mbadala hapa Zanzibar yameanza muda mrefu, na kwa kuwa ndio kwanza leo unatuambia kuwa ni juzi tu mwezi wa Mei ndio wameanza kufanya mazungumzo ya kufanya utafiti.

a) Je. Mhe. Naibu Waziri haoni kama serikali imechelewa sana kuanzisha suala hili?

b) Je, utafiti huo utachukua muda gani mpaka Wazanzibari kupewa taarifa ya kina ya utafiti huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, serikali inataka kufanya kitu cha uhakika na jambo lolote ili ulifanye vizuri na liwe la kudumu basi lazima unatakiwa uvute subra kwa kufanya utafiti ambao utafaa.

Kwa hivyo, serikali haijachelewa kabisa kufanya utafiti wa kulitafutia ufumbuzi suala hili la kuzalisha chanzo cha umeme Zanzibar. Kwa hivyo, kuchelewa huko sio sababu itakayosababisha pengine kupoteza muelekeo, isipokuwa tulichelewa au tulitumia muda mrefu kwa ajili ya kutaka kufanya jambo hili liwe la uhakika. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kutokupatikana umeme wa gharama nafuu, serikali haioni kuirudisha nyuma sekta ya uwekezaji viwanda kutokana na gharama kubwa za umeme?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kwa sasa serikali inachokifanya ni kutaka kuzalisha umeme Zanzibar. Suala la gharama baada ya kuwepo hicho chanzo cha umeme ambao utazalishwa Zanzibar, hapo ndipo kitakapojulikana kwamba umeme huo utakuwa ni wa gharama ya juu au gharama ndogo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwakilishi tusilijadili suala la gharama, tusubiri kwanza tutapate hicho chanzo cha umeme hapa Zanzibar.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 -
Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitowe taarifa kwamba wachangiaji waliopo huku niliko mimi mpaka sasa hivi kuna majina 40 na wamechangia wajumbe 12. Kwa hivyo, bado wachangiaji 28, ningeshauri kwamba tusirudie, mwenzako akishazungumza wewe sema jipya, sio tena nakazia, naongezea inakuwa tena unarudia mule kwa mula. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nikimwita mjumbe hayupo basi sirejei tena. Ninayemwita anachangia, tunaendelea na kazi. Nikimwita mjumbe yuko nje akirudi simwiti tena. Kwa hivyo, kila anayetaka kuchangia atulie angoje nafasi yake achangie dakika 20. *(Makofi)*

Tunaanza na Mhe. Panya Ali Abdallah

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Kwa mujibu wa taarifa ya juzi mchangiaji wa kwanza asubuhi ilikuwa ni Mhe. Mohammed Mbwana Hamad. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Sawa Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi halafu Mhe. Panya Ali Abdalla nilikuruka samahani na kufuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu pamojana Mhe. Subeit Khamis Faki. Wanne hao, kwanza tuanze na Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi hii ya kuweza na mimi kutoa mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Miko na Idara Maalum za SMZ. Lakini pia nachukua nafasi ya kukushukuru wewe kwa uadilifu wako, kwa sababu baada ya taarifa yangu ya kuchangia leo kwa mujibu wa taarifa ya juzi umeikubali bila ya kikwazo cha aina yoyote hongera sana kwa hilo.*(Makofi)*

Halafu jengine nachukua nafasi ya kumpongeza waziri kwa uwasilishaji wake mzuri uliokuwa na ufasaha wa hali ya juu. Baada ya shukurani hizo nianze mchango na kitabu cha kwanza ukurasa wa 50 Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nataka nizungumzie kuhusiana na Mkoa wa Kusini Pemba. Kifungu cha 119(i) "kuimarisha ulinzi na usalama kwa raia na mali zao". Suala la ulinzi katika mikoa mbali mbali ni suala muhimu na ni suala ambalo kama ulinzi upo unawaweka wananchi katika hali nzuri na amani pamoja na uhakika wa mali zao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tukiangalia hivi sasa matatizo mbali mbali ya ujambazi yanatokea katika mikoa, wilaya na shehia zetu. Kwa kweli kwanza nichukue nafasi ya kuwapa pole watu wangu wa Jimbo la Chambani wale wote ambao walipata kadhia ya kuibiwa katika kipindi kifupi kilichopita na wale ambao walipata kadhia ya kutiliwa moto nyumba zao. Mheshimiwa niiombe Serikali ya Mkoa iwe makini sana katika suala zima la ulinzi katika maeneo mbali mbali ya mikoa yao.

Serikali chini ya Jeshi la polisi imeanzisha dhana ya Polisi Jamii. Hili ni jambo zuri ni jambo ambalo linaweza likapunguza kwa kiasi kikubwa sana ujambazi na wizi katika maeneo husika. Lakini jambo la kusikitisha vituo hivi vya Polisi Jamii sijui serikali inaviangalia vipi. Natoa maelezo haya kwa sababu katika Jimbo langu la Chambani Shehia ya Chambani wameanzisha ujenzi wa Polisi Jamii ni muda mrefu sasa jengo lile halijamalizika, jengo ambalo vijana wake wako makini sana lakini mpaka leo halijamalizika. Namuomba Mhe. Waziri atapokuja hapa anieleze ni utaratibu gani wanautumia kuviimarisha vikundi vya Polisi Jamii, vikundi ambavyo vitaondoa kero kubwa ikiwa vitawekewa mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, jengo hili kwa kweli lipo pahala pazuri lakini hivi sasa Polisi Jamii ya Chambani inashindwa kufanya kazi zake vizuri wanategemea siku ya Jumamosi kufanya mikutano yao na mambo yao katika skuli. Hili ni tatizo kwa sababu skuli ni kituo mbali na kina shughuli mbali mbali wakati wameonesha moyo wa kujenga jengo zuri kubwa naiomba serikali ilisaidie jengo hili ili vijana hawa waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende moja kwa moja katika Soko la Qattar Chake Chake. Soko hili ni soko ambalo vijana wengi wamepata ajira pale kwa ajili ya kuuza bidhaa zao, lakini hali ya soko lile ni mbaya ni soko ambalo kukiwa na mvua tabu, kukiwa na jua tabu. Ni lini serikali chini ya wizara hii italiboresha soko lile ili vijana wetu wakiwepo pale wanaouza na kununua wawe katika hali nzuri inayoendana na wakati wa leo.

Nikiondoka katika Soko la Qattar niende moja kwa moja mpaka Tundauwa. Kuna soko Tundauwa limejengwa kwa msaada wa *TASAF* muda mrefu sana na lile soko limemalizika zaidi ya miaka mitatu iliyopita, lakini soko lile mpaka leo halijafunguliwa. Fedha nyingi za serikali zimetumika, watu walikuwa na matumaini makubwa ya kupata ajira, lakini soko lile mpaka leo limebanwa baa, namuuliza Mhe. Waziri ni lini soko lile litafunguliwa ili mahitaji yapatikane pale? Na kuna tati gani lililosababisha mpaka leo kwamba soko lile halijafunguliwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende katika Stendi ya Chake Chake. Stendi ya Chake Chake ni finyu mno kwa wakati wetu wa leo, watu wanapata usumbufu wanaotembea kwa miguu, wanapata usumbufu wanaotembea kwa vyombo vya maringi mawili kutokana na msongamano mkubwa wa magari yanayoingia pale. Mhe. Waziri ni lini Chake Chake mjini kutawekwa stendi yenye wasaa wa kuingia na kutoka magari?

Wananchi wa Kisiwa cha Pemba Chake Chake takriban ndio *center* ya shugli zao zote, magari wengi, watu ni wengi wanaoingia kila siku, lakini ufinyu wa stendi ni kikwazo. Kwa hivyo, naiomba wizara pamoja na yote lakini suala la stendi iwe ni miongoni mwa vipaumbele ili watu wa kisiwa kile katika mji ule ambao wanaingia na kutoka kwa biashara mbali mbali wawe na uhuru mzuri wa magari yao na wawe na uhuru wa kuingia katika mji ule vizuri bila ya usumbufu wa aina yoyote.

Nikiondoka hapo niende moja kwa moja katika Idara Maalum, nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuzitaja ijapo kimuhutasari Idara Maalum. Lakini kabla ya kuzitaja naomba ninukuu Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Sura ya Kumi Idara Maalum. Mheshimiwa nanukuu kifungu cha 121(1) "Kutakuwa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi yake na shughuli zake zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika sheria zinazohusika".

Mhe. Naibu Spika, zimetajwa Idara Maalum hapa ikiwa ni pamoja na KMKM, JKU, Chuo cha Mafunzo, KVZ na vyenginevyo. Sasa nilitaka niisome hii katiba ili ionekane umuhimu wa kuwepo Idara Maalum Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Idara Maalum ni vikosi vyetu, ni mali yetu ya Zanzibar, tunahitaji kuvilinda, kuvienzi na kuvipa heshima za aina yote. Inasikitisha sana kwamba Idara Maalum kwa kiasi fulani tunaipunguzia hadhi yake. Mimi nakuwa naumia sana kuona kwamba Idara Maalum ni Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya sherehe za Mapinduzi kilamwaka Januari, kwa nini Idara Maalum ya SMZ haziongozi gwaride la Mapinduzi ya Zanzibar? Mimi nakuwa naumwa. Nakuomba Mhe. Waziri ukija hapa utueleze kwa mantiki kwamba kwa nini Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hatujawapa mamlaka ya kuviongoza vikosi vyake katika sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa kweli Idara Maalum ina watu wakakamavu, ina watu wenye uwezo, ina watu ambao wanajiamini kwa nini mpaka leo gwaride la sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar linashikiliwa na JWTZ wakati ambapo sherehe za Muungano pia zinashughulikiwa na JWTZ. Umefika wakati makamanda wetu akina Komodo or Hassan, akina JKU Canal Soud Haji, akina Kamishna Chuo cha Mafunzo Khalid Hassan, Kikosi cha Valantia Luteni Kanali Mohamed Mwinjuma, waonekane na wao wanang'ara wanazisimamisha panga katika Uwanja wa Amani ndani ya sherehe za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini la pili nimuulize Mhe. Waziri kwa nini sherehe za Muungano vikosi vyetu vya SMZ havishiriki?

Mhe. Naibu Spika, niende kikosi kimoja kimoja nianze Kikosi cha Zimamoto. Kikosi cha Zimamoto na Uokozi ni kikosi ambacho kina majukumu makubwa, majukumu mengi kwa ajili ya kuokoa majanga yoyote yanayotokea katika visiwa vyetu. Kikosi hiki kinahitaji kiwezeshwe vile vile, miongoni mwa kuwezeshwa kwao hivi sasa Zanzibar tuna shida ya maji, tuna upungufu wa maji, lakini vikosi hivi inapotokea ajali ya moto inalazimika wapate maji ya kutosha kwa ajili ya kwenda kuzima moto eneo husika. Je, serikali ina mpango gani wa kuanzisha visima maalum vya maji kwa ajili ya kikosi hiki cha Zimamoto kwa ajili ya uokozi wa moto pale unapotokea.

Lakini nikiendelea katika vikosi naomba wanapopata uhamisho watu wa vikosi kutoka Unguja kwenda Pemba, kutoka Pemba kuja Unguja wawezeshwe, unakuwa ni usumbufu mkubwa vikosi vyetu hivi wanahamishwa maafisa au askari wadogo lakini hakuna posho ambalo wanawezeshwa moja kwa moja kwa ajili ya kujikimu, mpaka inakuwa ni kero mtu anapopata uhamisho kwenda Pemba au kutoka Pemba kuja Unguja anaona kwa kweli ameingizwa katika matatizo yaliyo makubwa. Kwa hivyo, naiomba serikali, wizara hii iliangalie vizuri suala zima la kuwaenzi na kuwatunza askari wetu hawa ili na wao wajisikie kwamba wanathaminika na wanathaminiwa katika serikali hii ambayo ipo hapa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende moja kwa moja katika kitabu cha pili kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani. Mhe. Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwanza naipongeza sana kwa ajili ya kuongeza mapato kutoka mapato ya mwaka jana na mapato ambayo wamekusanya kipindi hiki ambacho tunamaliza nacho, lakini pamoja na mapato ambayo yameongezeka ningemuuliza Mhe. Waziri, kwa sababu kuongezeka kwa mapato pia kuongezeke kwa mahitaji ya wananchi katika Halmashauri husika, hapa kuna ukurasa wa 63 kipengele cha 3 hiki kinasema Halmashauri ya Wilaya mwaka 2012/13 imesaidia miradi ya maendeleo iliyoanzishwa na wananchi, hapa anasema shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kusaidia vifaa vya ujenzi kwa wadi tano za Mizingani, Kengeja, Wambaa, Mwambe na Chambani utekelezaji huu umeshatekelezwa na Halmashauri ndio ambayo imefuatilia masuala haya. Suala langu naomba ufafanuzi wa utekelezaji wa wadi ya Mzingani nifafanuliwe ni midari ipi na ipi ya wananchi na wadi ya Chambani, nifafanuliwe ni miradi ipi na ipi ambayo imetekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani katika kipindi hichi kilichopita au hichi ambacho tunacho hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kumalizia mchango wangu katika halimashauri niende kidogo katika Ofisi ya Msajili na kadi za utambulisho, kwa kweli wananchi wetu wanapata tabu sana katika kupata vitambulisho kwa sababu masharti mengine yapo waliyoyakamilisha lakini upatikanaji wake nenda rudi nenda rudi, kuna wengine wanatimiza miaka lakini masharti yaliyomo ni kikwazo kiasi fulani mimi ningeliomba Serikali kwa jumla kama kuna njia ya kubadilisha sheria ibadilishwe sheria, watu badala ya kuwa ulazima au lazima kipatikane cheti cha kuzaliwa lazima hii iondoke nayo iwemo lakini kuwe na vielelezo vyengine, jamani kuna vijana wamemaliza skuli darasa la kumi na mbili, darasa la kumi na nne, Chuo Kikuu, shahada wanazo ivo hivi havijakuwa vitambulisho vya kuonyesha kwamba mtu huyu amekamilisha umri wa miaka 18 suala la kuwabana wananchi wetu kwa vitambulisho kwa ulazima wa cheti cha kuzaliwa kwa kweli hili ni tatizo na hatuwatendei haki watu hawa ambao wanakwenda na kurudi.

Mhe. Naibu Spika, ni hivi karibuni tu kulikuwa na uandikishaji wa vitambulisho vya ataifa hakukuwa na masharti ya namna hii na hata ukiangalia vitambulisho hivi walioandikisha ni wengi zaidi kwa sababu ukienda na leseni, ukenda na cheti cha kuzaliwa, ukenda shahada ya kumalizia skuli unachotakiwa pale ni kuthibitisha umri wako, kwa hivyo leo kuweka vikwazo kwamba lazima mtu akamilishe miaka kumi na nane kwa cheti cha kuzaliwa ni kuwakwamisha watu wetu, ni kuwakwamisha vijana wetu jambo ambalo kitambulisho cha Mzanzibari hivi sasa ni kitu muhimu sana, zamani labda mtu alikuwa akiona kama jambo la kawaida. Lakini kitambulisho cha Uzanzibari dnio roho ya mwanadamu katika safari zake za kwenda na kurudi na ajira na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru umeshaniwashia taa sitosubiri mpaka ukanambia kwamba muda wangu umekwisha, naunga mkono hotuba hii baada ya kupata majibu yangu yakiwemo yale ya vikosi vya SMZ. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia tumekutana hapa asubuhi hii tukiwa salama, lakini pia nichukue fursa hii kukushkuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii nikasema machache.

Mhe.Naibu Spika, mimi mchango wangu utakuwa mdogo sana nadhani wala haya madakika pengine sitoyamaliza, nikasema itakuwa sio busara na mimi ni mdau katika Wizara hii ikawa sikuweza kusema chochote.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu katika Tume ya Utumishi Idara maalum za SMZ, mchango wangu itakuwa ni pale ambapo tunawahamasisha vijana wetu kwenda katika makambi ya JKU ili kujiandaa katika ajira, mimi niombe sana tume hii ijipange vizuri katika kuona uajiri unafanyika katika uhalali ulio mzuri kwa sababu vijana wanakuwa wapo kambini wameshatumikia lakini wakati wa uwajiri wanaajiriwa wale ambao wapo kabisa wala hawajachukua mafunzo yoyote. Tunakuwa hatuwatendei haki vijana wetu na tutakuwa tunawavunja moyo kwamba wao wameshatumikia pale kambini halafu wanakuja kuajiriwa wenzao ambao hawajapita hata katika mafunzo yoyote. Tutawavunja moyo lakini pia wanapoendelea kukaa pale umri pia unazidi na matokeo yake watakuja kukosa ajira kabisa, hilo tulizingatie.

Mheshimiwa nikitoka hapo wenzangu wameeleza na ingawa umetutaka tusirejee lakini Mheshimiwa kwa umuhimu mkubwa kabisa lazima tuyarejee. Mheshimiwa maslahi ya askari wetu lazima tuseme sote kama kweli askari wetu majukumu waliyonayo lakini maslahi ni madogo sana. Lazima hili tuliseme na serikali izingatie kama askari hawa wana majukumu na wananfanya kazi katika mazingira magumu makaazi yao hayaridhishi ni lazima serikali ijitahidi katika kuona wanapatiwa makaazi bora hata zile ofisi zao zina hadhi inayofanana na wao.

Mhe. Naibu Spika, nivipongeze vikosi vyote kwa ujumla wake kwa kazi ambazo wanazifanya. Na pia nichukuwe fursa hii kuwashukuru waheshimiwa wajumbe hasa wale wa upande wa upinzani ambao walikuwa vikosi hivi wakivipiga vita sana wakisema havina kazi lakini leo kila anayesimama hapa mimi nasema kuna mafanikio makubwa. Kila anayesimama anachukua fursa ya kusema anavipongeza vikosi vinafanya kazi mimi ninashukuru kwamba sasa kazi yao imeonekana.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii kukipongeza sana Kikosi cha KMKM hasa pale serikali ilipoona ikawapatia fursa ya kujenga hospitali ambapo inasaidia wananchi wetu kwa juhudi kubwa sana. Ninawapongeza na sifa zao ziko mitaani kwa jinsi wanavyohudumia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, pia nieleze katika kikosi hiki cha KMIKM nimuombe sana Mhe. Waziri kwa sababu yeye mwenyewe ni shahidi kwa sababu Kituo cha Mkokotoni. Kambi ya Mkokotoni Mhe. Naibu Spika, nadhani ndio njia anayopita Mhe. Waziri akienda nyumbani kukagua wazee. Na kile kituo mahala kilipo kiko maeneo ya Ikulu ni sehemu ambayo wanakuja wageni wengi na wanakiona kile kituo pale. Nimuombe Mhe. Waziri kuchukua juhudi za makusudi kukiimarisha kituo kile kikawa katika hadhi ambapo inalingana na lile eneo ilipo.

Mhe. Naibu Spika, na nilisema muda mwingi na ninarudia kusema kwamba jamani kituo cha Kambi ya KMKM kiliopo Mkokotoni ni kituo muhimu sana ni lazima tukiangalie katika kukipatia vifaa ikiwemo boti ya kisasa ambayo pale matukio mengi yanajitokeza, tunaona ajali zinapotokea wao ndio wanakimbilia haraka. Jengine ni ile bandari ambayo ipo hatuwezi kuwa na kikosi pale kikawa hakina zana kwa sababu njia ya kupitia hayo magendo ndio hizo hizo. Mimi kwa macho yangu nimeshuhudia mara nyingi nikiwaona askari wanahangaika kwenda na huku wanaiona boti ile wanacheka nayo lakini wanashindwa. Aidha kama boti ipo hakuna mashine, kama mashine ipo hakuna mafuta. Mhe. Waziri nikuombe sana kituo kile kipewe kipa umbele kwa sababu ya pale mahala kilipo sababu ya bandari lakini na sababu kuwa kipo karibu mkondo wa Nungwi na maafa huwa yanatokea.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu huu niende katika Mikoa. Mhe. nichukue fursa hii kuipongeza Mikoa yote ya Zanzibar, Wakuu wa Mikoa pamoja na Wilaya zake na wenyeviti wa Halmashauri zake kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Lakini nitoe pongezi za dhati sana kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Kaskazini Unguja. Na natoa pongezi hizi lakini pia nitakuwa nina ushauri, ninawashukuru sana kwa kuimarisha ulinzi na usalama kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya lakini ushauri wangu huu Mkoa ninaizungumzia bandari iliyopo. Mkuu wa Mkoa umebahatika kuwa na bandari na bandari hii mimi nimekuwa nikisema inakuwa kwa kasi. Ni lazima pale kuwe na ulinzi wa kutosha. Matatizo mengi yanajitokeza, mabangi yanapitishwa hapo, maunga yanapitishwa hapo nilazima tuwe na uimarishaji mzuri wa kwa sababu pale kuna uingiaji ya wageni mbali mbali kutoka kisiwa chengine.

Kwa hivyo Mheshimiwa nalisema hili na kwa sababu kuna jambo ambalo lilijitokeza ndio maana nakazia kwamba lazima ulinzi uimarike. Kulijitokeza amekamatwa mtu hivi karibuni tena alikuwa ni shekhe anaonekana ana mtasbihi mkubwa kumbe anatudhalilishia dini ya kiislam kwa sababu shekhe mambo yake yote huwa ni mazuri. Lakini yeye alikuwa anapita na tasbihi na subhana zile anazitaja kwa sauti kubwa ili aonekane ni muumini mkubwa. Lakini matokeo yake yeye ndie aliyekamatwa na silaha. Kwa hivyo Mheshimiwa, ni lazima tuwe macho na tuwe imara ili kuhakikisha Mikoa yetu hii inabaki katika usalama.

Mhe. Naibu Spika, pia nilitaka nikusisitize labda uwapatie elimu ya kutosha masheha, kwa sababu masheha wetu inaonekana wageni wanaingia tu katika shehia zao lakini bila ya kuzingatia kama wageni hawa wengine wako katika hali nzuri au ya utulivu. Mheshimiwa masheha wetu mimi nasema badala ya kuwa na daftari lile la wapiga kura lakini wawe na buku la wageni ambao wanaingia na kutoka ili na hii elimu pia tuwape wananchi wetu, tunapofikiwa na wageni jamani ni muhimu kuwajulisha masheha wanaweza wakawa wageni wengine hawako katika hali nzuri ya amani na utulivu. Sasa tutakasema na sisi tutakuwa tumejiweka vizuri, linapotokea lolote kwa hivyo tutaonekana hatukuwaficha wageni hao.

Mhe. Naibu Spika, nieleze madiwani, wenzangu waliwasema sana madiwani na mimi si vibaya kusema madiwani ni waheshimiwa ambao tuichaguliwa sambamba katika mikutano yetu ya uchyanguzi. Ni vizuri na wao wakafikiriwa mishahara, wanafanya kazi kwa bidii kubwa lakini hakuna mshahara isipokuwa wanapata posho dogo tu. Mhe. Naibu Spika, pia kuna Mheshimiwa alisema hapa kuhusu Madiwani wanawake kwamba asilimia na sisi ifikiriwe kuongezwa.

Mhe. Naibu Spika bandari bubu ambazo hizo nazo pia zinajitokeza kwa kasi. Mheshimiwa tukaongeza ulinzi katika kuzidhibiti bandari hizi bubu ambazo zitahararisha usalama wetu, usalama wa afya zetu, kwa sababu inawezekana maradhi kama haya ambayo yanajitokeza ya kuambukiza mgonjwa akaweza kujipenyeza katika boti ile ambayo anajua atakwenda kushuka uchochoroni huko akaja akasababisha madhara makubwa kwa wengine. Lakini halikadhalika mifugo pia. Bandari hizi ambazo hazina uhakika wanaweza wakazitumia katika kushusha abiria au mifugo ambayo haiku salama.

Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameeleza sana kuhusu Baraza la Manispaa, kwa kweli bado hatujajipanga katika usafi wa mji lazima serikali ichukue juhudi za makusudi, pamoja na kwamba juhudi inachukuwa lakini bado ziongezwe za makusudi ili mji wetu uweze kung'ara. Na hili kuna Mheshimiwa alisema hapa Mheshimiwa sheria, kama sheria hatujaitumia bado tutakuwa hatujaweza kujiongoza katika suala zima za manispaa. Mhe. Naibu Spika, wenzetu waliofanikiwa katika miji yao sheria inafanya kazi kisawa sawa ili kila mmoja anachukuliwa hatua pale anapokwenda kinyume na utaratibu uliopangwa.

Mhe. Naibu Spika, bado taka hatujaweza kuzidhibiti, mji wetu bado ni mchafu na ni aibu kwa sababu tunakuwa tuna wageni ambao wanatembelea katika mji wetu. Mji ni usafi pamoja na bustani ambazo zimepangwa vizuri kwa ustadi ndio mji unapendeza. Bado tuna tatizo la bustani, bustani yetu inaonekana hapa ipo, hapa haipo, hapa imezongwa na mwitu. Mhe. Naibu Spika, labda mimi niulize utakapokuja unieleze tatizo ni nini? Tuna uhaba wa wafanyakazi au tuna uhaba labda wa vitendea kazi, labda utakapokuja utueleze kwa sababu mimi nimeona pale Michenzani tulianza kutengeza mahala pakawa panaonesha sura nzuri. Lakini Michenzani hiyo hiyo bado hatujaweza hata kuikamilisha yote ile Michenzani tu tukaweza kuizunguka ikaonekana kwa hapa hatua ya bustani tumeweza kufanikiwa, bado bustani yake iko vipande vipande.

Mheshimiwa mimi naomba hata lile bwawa ambalo tulilijengewa pale ambalo lilikuwa na sura ya kupendekeza lakini bado linaonekana halijaweza kurudi katika haiba ile ya zamani ambayo mwasisi wetu alituachia. Mheshimiwa mimi naomba sana mji wetu uweze kung'ara na kupendeza kuwa kuweza kujengewa bustani na usafi ambao utaridhisha.

Mheshimiwa niseme kuhusu suala la usafi tumeona katika miji ya wenzetu mara nyingi unafanywa usiku ukiamka mji uko safi kabisa, kilichobakia asubuhi watu wakiamka wanafikia kuokota okota zile taka ndogo ndogo lakini yale sasa hivi kwetu bado hatujajipanga usafi unafanyika asubuhi ambapo unawachafua wafanyakazi na suti zao wanapokwenda kazini mwenye fyagio naye anakufyagia. Kwa hivyo mimi naomba sana Mheshimiwa suala la kusafisha makaro utakuta asubuhi watu wanasafisha haipendezi. Wewe unatakiwa kama limetokea suala la karo wafanyakazi waingie usiku baadae asubuhi wakiamka hakijulikali kitu gani kilitokea. Mheshimiwa ninaomba tujipange katika hayo.

Mheshimiwa nilisema mimi nitakuwa sina mengi lakini isingekuwa busara kwa Wizara hii nikawa nisichangie hata kidogo kwa hivyo naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sote tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, pia ninakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii kuchangia hiyo hotuba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Idara Maalum za SMZ.

Kwanza nimpongeze sana sana Mhe. Waziri Mhe. Haji Omar Kheri kwa kazi yake kubwa anayoifanya na ujasiri na uakamavu mkubwa anaouonesha kwa Wizara hii ninampongeza. Pia niwapongeze watendaji wake wote kwa kazi yao pia nzuri hiyo. Na mwisho nimpongeze sana sana Mwenyekiti wa kamati hii Mhe. Ussi Mwakilishi wa Chaani na Wajumbe wake wote kwa kazi yao nzuri waliyoifanya hi kwa ripoti yao ya Kamati waliowasilisha hapa.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi nianzie katika ukurasa wa 3 kifungu namba 7, majukumu waliopewa yanayohusu usimamizi wa Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum SMZ na Idara ya Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua Wizara hii ni muhimu sana katika nchi yetu. Ninasema kama ni roho ya nchi yetu kwa Zanzibar, kudumisha amani, ulinzi na usalama katika Mikoa na Wilaya hadi Shehia, kulinda mali za taifa na za watu binafsi visiibiwe kuzuia uingizwaji wa mageno nje ya nchi pamoja ndugu zetu hawa wa zimamoto. Mhe. Naibu Spika, nimeseme hivi kuwa ninajua Wizara ni muhimu sana na ina mmbo mengi na majukumu makubwa na mazito kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nianzie kwenye ukurasa wa 29 nianze na Mkoa wa Mjini Magharibi hasa suala hilila uhalifu. Lakini kabla sijaanza hapo nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake hii ya bajeti na kuwasiisha ndani yake huu mpango mzima wa CCTV Camera. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua nchi yetu hasa katika Mji Mkongwe nieneo muhimu sana katika Zanzibar na watalii wengi wanakuja kutembelea katika mji huu. Kama tunavyojua una historia nyingi na vivutio vingi vya watalii na pesa nyingi serikali inapata kupitia hawa wageni.

Lakini pia nimpongeze sana ndugu yangu RPC wetu Mkadam wa Mkoa Mjini Magharibi kwa kazi yake nzuri na umahiri wake mkubwa sana anaoufanya na kujitahidi kuweka mjia wetu katika hali ya usalama na kupunguza uhalifu. Lakini mimi Mheshimiwa nije katika hii CCTV Camera, ni jambo jema ni jambo muhimu sana katika nchi yetu likiweza kufanikiwa na kama Mhe. Waziri alivyotwambia katika kitabu chake wapo wawekezaji sasa hivi na wana mazungumzo makubwa.

Lakini mimi nasema Mhe. Waziri hili suala muhimu na lisifanyiwe mchezo na endapo hawa wawekezaji watapata kuweka CCTV Camera nilikuwa nakuomba Mhe. Waziri suala moja muhimu sana tuliuangalie, pia wazalendo wetu wapo hapa wanafunga hizi Camera ni Kampuni ya Electrics hawa jamaa ni wazuri na wataalam wazuri. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri utakapopata wawekezaji hawa watafunga hizi camera basi washirikishwe wazalendo. Kwani zikiharibika hizi camera tusiwe tena kupiga simu nje aje mtaalam hapa, hapa hapa ndugu zetu hawa wafanye kazi hii waweze kutatua matatizo yao katika masuala ambayo yataleta uharibifu. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri wazalendo pia washirikishwe katika kufunga hizi CCTV endapo serikali imeingia mkataba na wawekezaji kutoka nchi nyengine. Kwa nini nikasema hivyo kwa sababu ulinzi ni muhimu, ulinzi ni usalama wa wananchi namali zao.

Mimi nije kwenye suala jengine hapa hapa Mji Mkongwe Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema Mji Mkongwe ni mji muhimu, lakini niseme jambo jengine ambalo hawa wananchi wetu au hawa Polisi Jamii, Polisi Shirikishi kwa kweli wanafanyakazi kubwa na mashirikiano makubwa wanatoa na Polisi wetu hawa. Lakini wao wanakuwepo wanalinda usiku na mchana. Lakini mimi ninawasikitikia sana Polisi. nitoe mfano Polisi wa Mji Mkongwe kwanza kwa sababu mimi hata jimboni kwangu ninao Polisi Jamii lakini nitoe suala la Mji Mkongwe kwa sababu hawa wanajitahidi sana na tunapigiwa mfano hata wamepewa zawadi na Kamishna mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, lakini ninasikitika sana Mhe. Naibu Spika, hawa Polisi Jamii wetu wanakuwa wana hali ngumu lakini mimi nitoe ushauri au rai Mhe. Naibu Spika, ni jambo muhimu katika nchi yetu katika majimbo yetu. Hawa Polisi wanahitaji vifaa mbali mbali, lakini fedha zao zinakuwa kidogo hawana uwezo wa kupata fedha hizi, lakini ninawaomba Wawakilishi na Wabunge tutoe mchango kuwasaidia hawa Polisi Jamii hasa tuna vifaa mbali mbali vinavyotakiwa Mhe. Naibu Spika, kama wanahitaji rain coat, wanahitaji viatu, wanahitaji usafiri hawa watu, wanahitaji sare wanahitaji ofisi lakini naomba sana wapate huduma hiyo na wawezeshaji waweze kuweza ili kuweza kufanya kazi zao kwa umakini kabisa na kutulindia mji wetu ukawa mji mzuri kabisa na wenye sifa nzuri kabisa.

Kwa hivyo naomba sana wawakilishi na wabunge tuwasaidie hawa wenzetu hasa katika Mji Mkongwe ni mfano, ni sura ya nchi yetu lakini hawa Polisi Jamii wanapata tabu sana. Kwa hivyo Mheshimiwa Mwakilishi unanisikia sana ninakuomba uwaangalie sana hawa Polisi Jamii malalamiko yao tuweze kuwasaidia kupitia Mbunge na Mwakilishi mkiwa na mimi pamoja tutayashughulikia pamoja tuwasaidie Polisi Jamii.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 32 wa kitabu hiki cha Mhe. Waziri nije kwenye ujasirimali. Kama nilivyoona kitabu hiki Mhe. Waziri wameweza kusaidiwa wajasirimali 18 kwa vikundi vyao mbali mbali vya vijana, kikiwemo ushoni, kazi za amali, mapishi. Mimi Mhe. Waziri ninakupongeza tena kwa kazi hii nzuri sana kwa kuwasaidia hawa vikundi 18 vijana waweze kujikwamua na maisha magumu na wapate rizki zao za kila siku kwa kuwasaidia mambo tofauti ili kuweza kujikwamua na hali hii. Kwa hivyo naomba Mheshimiwa jambo hili jema na zuri tuige mfano kama Waziri wengine pia waweze kusaidia kama hivi na waone suala ni muhimu kwa vijana wetu kuwasaidia suala kama la ushoni, kazi za amali, suala la mapishi ni suala la muhimu sana katika nchi yetu.

Lakini nije kwenye swali jengine kumpongeza Mhe. Waziri suala hili la vikundi viwili vya sanaa vya muziki wamepatiwa msaada pia na Wizara hii. Kwa hivyo mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kuliona hili kwa vijana wetu kwani vijana ndio taifa la kesho, mimi nasema kila siku, taifa la kesho ni vijana. Kwa hivyo tukiwaangalia vijana vizuri wanamsaidia kuongoza nchi hii kwa nia njema na kwa kazi nzuri kabisa watakayoifanya, kwani wamepatiwa msaada vikundi viwili vya muziki.

Lakini Mhe. Waziri mimi nasikitika upande mwingine vijana wapo wengi hasa katika suala la muzuki wapo kwani muziki sasa hivi ni ajira wanafanya kazi zao vizuri na wanapata ajira sehemu mbali mbali kwa sababu ya mziki. Nawashukuru kwa kuwasaidia vikundi viwili lakini kuna wasanii wetu wa filamu hapa Zanzibar wapo ambao wana maisha magumu, wana hali ngumu na wanajitahidi kwa kazi zao nzuri za kuelimisha jamii. Mimi niseme mfano mzuri *ZBC* kuna vikundi vyetu hivi wanarikodi tamthilia mmoja anaitwa Mudi na wenzake wengine mmoja jina lake limenitoka ni mwanamke na anakaa katika jimbo langu, hivyo wana kazi nzuri wanafanya katika televisheni na watu wanavutiwa kuangalia. Mimi ni mmoja navutiwa sana kuangalia tamthilia zao nzuri zinafundisha maadili yetu kuhusu madawa ya kulevya na mambo mengine tofauti.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri na hawa tuweze kuwasaidia vikundi hivyo vya filamu hawa vijana wetu waliokuwa hapa Zanzibar ambao wanahangaika sasa hivi shida yao kubwa Mhe. Naibu Spika wanataka vitendea kazi kama *camera*, usafiri hawana wanahangaika kwa miguu utawaona mchana kurikodi hizi tamthilia zao. Hivyo Mhe. Waziri nakuomba uwaangalie vijana wetu kwani wanajitahidi sana na wanaweza kufika mbali, kama ninavyojua Zanzibar tuna historia ya wasanii, tunaweza kupata wasanii wazuri na kufanya vitu vizuri katika dunia hii. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri uwaangalie hawa vijana wetu.

Mhe. Waziri mimi niseme kwa upande wangu hawa wasanii wa filamu nina mpango wa kuwasaidia na nimeshawaambia si muda mrefu Mhe. Waziri nitawasaidia *camera* nzuri ambayo ni *HDMI*, filamu nzuri, picha nzuri, usafiri pia nataka niwasaidie vijana wetu ili wafanye kazi zao kwa urahisi. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri tushirikiane vizuri kuwasaidia vijana wetu kwani hii ni ajira moja kwao wao itakuwa hii na pia tutaisaidia serikali yao kwa kuipunguzia mzigo kwani sasa hivi ajira siyo utegemee serikali tu kupata ajira, aah kuna ajira nyengine ndogo ndogo za kupata riski zao na wakafaidika vizuri. Kwa hiyo, Mhe. Waziri tusaidiane kwa hili hawa vijana tuweze kuwaangalia vizuri.

Lakini Mhe. Waziri pia kuna malalamiko baadhi ya wazee, kuna wazee kwenye ripoti ya Kamati nimesikia kwamba kuna wazee wanalipwa shilingi 5000. Mheshimiwa kwa kweli shilingi 5000 ni kidogo sana sasa hizo fedha zinakuwa haziwasaidii kwa kuendesha maisha yao, kwa hiyo naomba uwaangalie sana hawa wazee wanaolipwa shilingi 5000 waweze kuongezewa kwani hali ya maisha yako juu na wao wanakuwa kidogo maisha yao yanakuwa ni duni.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa wa 33 katika udhibiti wa vitendo vya udhalilishaji kwa Mkoa kushirikiana na Kamati za Usalama za Mkoa na Wilaya umeendelea kuimarisha jamii juu ya upigaji vita udhalilishaji wa kijinsia. Mheshimiwa suala hili nimeshawahi kulisema hapa na hili suala linasikitisha na bado linaendelea, lakini kwenye kitabu chako cha bajeti Mhe. Waziri umeliandika nakushukuru sana na kukupongeza sana kuwa suala hili umeliona katika Shehia ya Fumba, Bweleo nashukuru suala hili umeliona kwani lipo na mimi nimeshawahi kuambiwa, lakini suala hili ni zuri na umefikia hatua nzuri bado isiwe mwisho lakini uendelee. Mhe. Naibu Spika, Bweleo, Fumba, Dimani, Kombeni kuna kesi 23 za wanawake, watoto wa kike na kiume katika udhalilishaji. Mheshimiwa naomba kesi hizi tuzisimamie vizuri na hatimae kupatikane ufumbuzi wa kupata adhabu hawa watu wanaodhalilisha watoto na wanawake katikak maisha wetu. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri suala hili ulipe kipaumbele sana na iwe funzo kwa wengine watakaofanya mambo haya ya kudhalilisha watoto na wanawake.

Mhe. Naibu Spika, niingie sasa kwenye ukurasa wa 37 kuhusu shughuli za elimu ambapo Mkoa umefanya ukaguzi wa skuli 20 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ufundishwaji wa masomo, mahudhurio ya wanafunzi, kukaguliwa vituo vyao vya mtihani hatimae watoto 62 wamesaidiwa sana Mhe. Naibu Spika. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri pale mwanzo nilimpongeza nazidi kumpongeza tena najua ana imani kwa nchi yetu, anajitahidi kusaidia watoto wetu hawa wa skuli, lakini mimi niseme Mhe. Naibu Spika suala hili zuri la kufuatilia watoto. Mimi nataka nitoe mfano mzuri na na wa kweli kabisa wa haki nakumbuka mwaka jana nilipopata kuchaguliwa kuwa mwakilishi nikaandaa usafiri wa basi kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka Bububu kuja Mjini.

Mhe. Naibu Spika, mahudhurio yalikuwa ni mabaya sana ukiangalia mwanzo utakuta watoto huzuiwa mpaka wanafika 40, wakienda wakafika 50, wakafika 60 kwa asubuhi sasa hivi wanafika watoto 250 mpaka 300 kwa mara moja kuwaleta mjini. Kwa hivyo, hilo jambo ni jema kabisa mimi nakupongeza sana Mhe. Waziri kwa suala hili la kuwashughulikia watoto wetu kuwashughulikia kufika skuli kwa wakati na kwa uhakika zaidi. Lakini tusiishie hapo na majimbo mengine pia Mhe. Naibu Spika nilikuwa naomba Wabunge na Wawakilishi wawaandalie watoto usafiri kwani wanapata tabu sana watoto hawa kufika skuli kwenda na kurudi kwa ajili ya usafiri unakuwa mgumu. Kwa

hiyo, Mhe. Waziri nakushukuru sana kwa kuwapatia watoto 62 sare kuwasaidia hili suala ni kubwa sana kwa ajili ya Taifa letu ni maendeleo makubwa kwa nchi yetu kufuatilia watoto wetu wakaweza kusoma, kwani dunia ya sasa hivi inakwenda na teknolojia huko mbele bila ya kusoma tutakuwa hatuna Taifa lilokuwa bora.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kuna rai moja alinimpa Mhe. Balozi, Mheshimiwa nilikwenda kwake akaniambia mimi jimboni kwangu nimetoa changamoto fulani watoto wa *form five* na *form six* watakaopasi kila mtoto atakayepasi aliwaambia watoto wale nitawapa shilingi 100,000/= kila mtoto mmoja. Mhe. Balozi akaniambia na wewe fanya hivyo hivyo waambie watoto wako wa skuli ya sekondari ya Bububu akipasi mtoto mmoja utampa shilingi 100,000/=. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, wazo hili limenisaidia na nilikwenda skuli ya Bububu kufika pale nikaulizia mwaka jana ilikuwa vipi? Nikaambiwa mwaka jana hajapasi mtoto hata mmoja Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli lilikuwa jambo la aibu na siyo zuri kwa watoto wetu wanavyofeli kabisa. Mimi nikasema sasa mwaka huu 2014 mtoto atakayepasi mmoja nitampa shilingi 100,000/= hilo wazo zuri alinipa Mhe. Makamu wangu wa Pili wa Rais alinishauri nifanye hivyo.

Mhe. Naibu Spika, nilitoa ahadi hiyo mwaka jana kwa skuli ya Bububu pale sekondari kwa kweli nawapongeza wanafunzi wale tena mara hii kwa kupasi watoto 52, na watoto niliwapa kila mtoto mmoja shilingi 100,000/= kama zawadi kwa wale waliopasi ili ziweze kuwasaidia uniform, viatu pamoja na vitabu vyao. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wazo hili ni zuri na sisi Wabunge na Wawakilishi tuliokuwepo tufanye kama hivi kama hii ni changamoto kwa watoto wetu ili waweze kupasi watoto wengi tupate watoto waliokuwa bora kabisa.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwenye ukurasa wa 38 hili suala la maji ambalo ni suala muhimu na suala hili katika nchi yetu ni tatizo kubwa linaendelea matatizo ya maji. Lakini katika kufuatilia uchimbaji wa visima tisa vya ziada vinavyofadhiliwa na Ras-il-Khema kati ya visima hivyo vitano vitachimbwa Kaskazini na vinne viko Kaskazini "B". Mimi nawashukuru sana wafadhili hawa kwani wameliona tatizo hili ni kubwa na kwa serikali yetu kuliona hili tatizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba tena wakitokea wafadhili kama hawa Mhe. Waziri pale kwenye Jimbo langu la Bububu kuna maji mengi sana Mwanyanya kwa nini kusichimbwe visima kama hivi vikachimbwa japo viwili au kimoja. Kwa sababu hawa Ras-il-Khema wanachimba visima wanaweka na tangi kubwa kwa ajili ya ku-*store* maji na wananchi wa pale wanafaidika kwa huduma hii ya maji. Kwa hivyo, naomba eneo lile pale lina maji ukichimba kisima kidogo unapata maji, kwa hiyo ukitokea mradi kama huu naomba Mhe. Waziri kwa faida ya watu wa Zanzibar visima vichimbwe japo viwili pale Jimbo la Bububu eneo la Mwanyanya kuna maji mengi sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa bado dakika tano.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante namalizia Mheshimiwa zinatosha hizo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasikitika tena wafadhili wamesaidia fedha nyingi kwa kuweka miradi kama hii, lakini usimamizi wetu unakuwa siyo mzuri hasa kwa suala hili la maji ukifuatilia hawa wenzetu wa *ZAWA* ufuatiliaji wao kidogo siyo mzuri sana, miradi ni mizuri, maji yanatoka kwenye vianzio vya maji ukifika sehemu husika maji mengi yameshapotea njiani.

Mhe. Naibu Spika, suala hili la mabomba nalo tuliangalie kwa serikali nzima ilivyokuwa miradi kama hii kupitia mabomba yetu kama kumeshachimbwa visima na wafadhili basi sisi wenyewe japo mabomba tujipige pige tutie mabomba mapya, siyo maji mengi yanapotea kutoka Mwanyanya mpaka kuja Saateni *liter* za maji sijui ngapi zinapotea kwa siku njiani. Kwa hivyo, naomba tuweze kulitatua suala hili kwa kuweka mabomba mapya kupitia serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, niingie kwenye ukurasa wa 16 katika Ofisi ya Usajili Kadi za Utambulisho imeanzishwa rasmi mwaka 2005 chini ya sheria Nam. 7 ikiwa na wajibu wa kuwasijili na kuwapatia vitambulisho wa Zanzibari wote.

Mhe. Naibu Spika, baadhi ya wananchi mpaka leo nasikitika hawajachukua vitambulisho vyao, lakini niseme tulikwenda Pemba siku moja na kamati katika Wizara ya Usajili wa Ardhi wananchi wengi hawajasajili ardhi zao, lakini ukiwauliza tatizo nini wanasema vitambulisho hawana. Lakini hapa Mhe. Waziri alitwambia kwamba

hawajenda kuchukua vitambulisho vyao kwa hivyo kuna baadhi wanadharau wenyewe halafu wanaitia doa serikali kama haitaki kutoa vitambulisho hivi.

Mimi naona Mhe. Naibu Spika, hili suala jengine wananchi wenyewe wanakuwa wanadharau haya mambo ya kuchukua vitambulisho vyao. Kuna vitambulisho karibu 1000 viko kwenye ofisi hii bado havijachukiliwa, kwa hiyo naomba hasa ndugu zangu wa Pemba wakachukue vitambulisho vyao ili waweze kusajiliwa. Kwa sababu vipo vimekaa tele lakini hawaendi kuchukua halafu inakuwa wanaisikitikia serikali hivyo jambo hilo siyo jema. Mhe. Naibu Spika, naomba waelewe serikali ina nia njema katika nchi na kwa wananchi wao sidhani kama Mhe. Waziri ana nia kuwanyima vitambulisho hivi kwani hii ni haki ya kila Mzanzibari kupata kitambulisho hicho.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala hili la vitambulisho vya wageni wanaoishi nje ya nchi yetu ya Zanzibar, vitambulisho vyao wao bado havijakamilika taratibu zao. Mimi naomba Mhe. Waziri suala hili ni zuri hawa wageni waweze kupata vitambulisho ili waweze kuja kwenye nchi yao na wazaliwa wa hapa waweze kutusaidia kwa uhakika kabisa. Kama tunajua kuna chama kimoja cha wa Zanzibar kipo Canada kinaitwa *ZANCANA* hawa watu wana nia ya kutusaidia na wameshatusaidia kwa kutuletea misaada mbali mbali katika nchi yetu hii. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri hili suala wapatiwe hawa ndugu zetu waliokuwa nje vitambulisho vya wageni process yao iweze kwenda haraka sana ili na wao wapate imani na kujua nchi yao ipo na waweze kutusaidia kwenye matatizo madogo madogo tuweze kuyatatua.

Mhe. Naibu Spika: Malizia.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi nije kwenye suala hili naolo ni muhimu sana Idara Maalum za SMZ majukumu ya kuratibu na kusimamia kazi za idara maalum za SMZ kama vikosi vya KMKM, JKU, Mafunzo na KVZ.

Mhe. Naibu Spika, hawa ndugu zetu wana kazi kubwa na kwa kusema ukweli wanajitahidi katika sehemu zao mbali mbali za ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Lakini nije kwa hawa ndugu zangu wa KMKM kwa kweli hawa jeshi letu la polisi wana kazi kubwa na wanajitahidi katika kuimarisha maendeleo ya nchi yetu. Nataka niwapongeze sana mimi ndugu zangu wa KMKM waliokuwa pale Kibweni kwa kujenga hospitali ikaweza kuwahudumia wananchi wetu mbali mbali, kuwasaidia matibabu na ni jambo zuri kabisa. Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kitu kimoja naiomba serikali iangalie vizuri pale KMKM wagonjwa ni wengi lakini utakuta wagonjwa wakiwa pale wengi wanapigwa na jua asubuhi mpaka mchana utakuta wazazi, watoto wako nje wanapigwa na jua sana, huduma inakuwa inachelewa. Kwa hiyo, naiomba sana wizara iangalie kwa kutia kipaa pale eneo la KMKM pale nje ili hawa wagonjwa waweze kukaa kwa amani na utulivu kabisa.

Mhe. Naibu Spika, muda wangu unaenda lakini nimalizie kidogo tu suala la Manispaa…

Mhe. Naibu Spika: Muda umemalizika, nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana asubuhi hii ya leo kupata fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nataka nianzie hapo anapomalizia rafiki yangu kuhusu usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Naibu Spika, suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi bado ni tete kama tunavyozungumza kama kuna wananchi ambao wanalalamika kwa sababu ya masharti ya hivyo vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa sababu Mheshimiwa kila siku tunazungumza kama kuna wazee ambao ni wazee kuwalazimisha kuwa na vyeti vya kuzaliwa ni tatizo na hata kwenda kuchukua hiyo karatasi Mahakamani pia inakuwa ni tatizo kwa sababu *affidavit* nayo ina masharti yake. Kwa hiyo, lazima uende na mtu pale anayekuzidi umri ndiyo utaipata nayo, kwa hiyo pia inakuwa ni tatizo Mheshimiwa naomba sana kwa nini tusichukue kama wenzetu wanavyofanya hawa wa *NIDA*. Wenzetu wa *NIDA* wao wanatoa vitambulisho masharti yao uende na vitambulisho wanaweka masharti ambayo yanawawezesha wananchi kupata vitambulisho, na ndiyo maana vitambulisho vile vya Tanzania vimetoka kwa wingi bila ya matatizo kwa sababu wao wanaweka masharti, ukienda na gamba la kuzaliwa, lakini hata gamba la mtu aliyezaliwa

hospitali ikiwa ana gamba basi hapati kitambulisho kwa mashati yetu sisi. Ukienda na vyeti vile vya zamani vidogo havitaki.

Kwa hiyo, Mheshimiwa masharti haya yapunguzwe ili wananchi wapate vitambulisho na hivyo vitambulisho mnavyosema kama vipo maofisini ni kweli viko lakini vitambulisho tumefanya utafiti sisi kwa sababu utafiti tulioupata tunashukuru sana baada ya mazungumzo na waziri aliyekuwa akishika hii nafasi Mhe. Mwinyihaji Makame tulifanya mazungumzo pamoja na yeye tukakaa na watendaji wake, wawakilishi, madiwani tukafanya mazungumzo nashukuru kwamba walitupa orodha zile ambazo ni za watu ambao vitambulisho vyao viko. Na vitambulisho vile tulipofuatilia kuna watu wana vitambulisho viwili mpaka vitatu na hii ilitokana na kwamba watu walikuwa wameshapiga picha za vitambulisho anakwenda mtu anataka kitambulisho chake hakipati, anapiga picha tena, akipiga picha tena anapata vitambulisho viwili.

Kuna watu wana vitambulisho viwili viwili tena wapo wengi, hivyo vitambulisho mnavyosema kama vipo tumewafuatilia watu mmoja baada ya mmoja ukifika unakuta kitambulisho anacho na kule kiko. Kwa hiyo, mjue kama kuna watu walisajiliwa mara mbili hivyo vitambulisho vilivyoko ni watu waliosajiliwa mara mbili. Kwa hiyo, ni kweli viko lakini kuna watu wamesajili mara mbili, hivyo Mheshimiwa bado tunazungumza kama suala la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ni haki ya kila mmoja tulipitisha sheria hapa kama mtu aliyekuwa hana kitambulisho afungwe mwaka mmoja, ndiyo ilivyo basi tuwafungeni watu tuwachukueni wote Wazanzibari waliokuwa hawana vitambulisho tuwafunge. Kwa sababu watu wanakosa vitambulisho na wakati ni haki yao.

Mtu hawezi kupata kitu chochote kila siku tunazungumza hapa, ukienda kwenye ajira kama huna kitambulisho hupati, ikiwa unataka udereva mimi nishakwenda na mtu ambaye ameshasoma udereva ameshakwenda mpaka pale ofisi ya leseni anataka leseni akaiokosa leseni kwa sababu hana kitambulisho. Kwa hiyo, leseni unakosa, kazi unakosa kuna watu jamani ni Wazanzibari kindakindaki wamezaliwa baba na mama hapa hawajaondoka mtu hapo na hapo hawana vitambulisho. Wanakuja watu ambao kuwa wanajisifu anakuja Mmasai anatoka Arusha amekuja mara moja tu basi ana kitambulisha, jamani tunawanyima watu haki zao kwa nini na kila siku suala hili tunalizungumza, kila siku tunazungumza basi jamani tuwahamisheni, kama si Wazanzibari hao wasiopewa basi tuwahamisheni. Mhe. Naibu Spika, tufanyeni bidii tuweke chao kisiwa tuwahamishe waende wakakae, kwa sababu tunawakosesha haki zao za msingi jamani kitambulisho cha Mzanzibari ni haki ya kila mmoja kwa nini tunawakosesha watu haki zao.

Mhe. Naibu Spika, masharti bado tunasema kama yapunguzwe kwa sababu masharti kama wanayofanya wenzetu yanaharibu nini, mtu ana leseni ameipata hapa Zanzibar ni Mzanzibari ana leseni ya kuendesha gari na anaendesha gari, kwa nini asipewe leseni yake. Mtu ana gamba la kuzaliwa la hospitali kwa nini asipewe, mtu ameshapiga kura ana vitambulisho sita vya kupigia kura akienda pia hapati, jamani tunataka ushahidi gani huo ushahidi mnaoutaka mpaka mtu awe ni Mzanzibari ni upi? Sasa tuhamisheni au mpaka mtu atoke Tabora aje ajiite Mnyamwezi ndiye ni Mzanzibari, basi na waje wajiite Wanyamwenzi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ninalotaka kulizungumza ni suala la vikosi, na mimi nataka niungane na wenzangu kuvisifu vikosi vyetu, walinzi wetu na naomba tuwathamini tuone kama ni walinzi kweli. Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko hasa kikosi cha KMKM, walizungumza na Waziri aliyepita na wakakubaliana kama watatoa pesa zao za likizo kila baada ya mwaka mmoja watapewa laki moja kwa ajili ya pesa za likizo. Hawapewi kwa nini hawapewi na ni haki yao? Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Waziri hili suala lishughulikie ili wapewe haki zao za pesa za likizo kwa sababu ni haki yao ya kila msingi na wapewe haki zao za msingi.

Suala jengine ni Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Tulizungumza kwamba kikosi hiki kinataka kipewe zana za kutendea kazi kwa sababu tumekipa jina la Zimamoto na Uokozi. Sasa kama ni Zimamoto na Uokozi lazima wawe na nyenzo za uokozi linapotokea tatizo wawe wanazo. Magari ya Zimamoto ni machache na tunaomba sana Mhe. Waziri mtu hujifunza kutokana na kosa linalotokea.

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi kwamba kipindi cha mwaka huu tulionao jimbo langu la Micheweni lilipata matatizo ya moto, Kikosi cha Zimamoto kiko Chake Chake wanapigiwa simu kushaingia moto Micheweni, wewe fikiria kutoka Chake Chake tena Uwanja wa Ndege mpaka ikifika Micheweni inakwenda kukuta nini? Kwa hiyo, mtu hujifunza kutokana na kosa, tunaomba hivi vikosi vya Zimamoto kila wilaya viwepo ili likitokea tatizo wawe wanaweza kukabilianalo. Lakini kikosi cha Zimamoto kiko Chake Chake anakwenda Micheweni atakuta nini, walipofika nyumba zote zishateketea, wananchi wameshashirikiana *Alhamdulillah* wameshauzima ule moto. Kwa

hivyo, tunaomba nyezo ziongezwe kwa vikosi hivi na halafu kila wilaya tuwekewe kikosi hicho kwa ajili ya kwamba likitokea tatizo waweze kulishughulikia.

Jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la Baraza la Manispaa ya Zanzibar. Watu wengi wamezungumza suala hili na mimi naona nilizungumze kwamba bado Manispaa ya Zanzibar haijatekeleza wajibu wake. Wajibu wake ni kutekeleza mji wetu tukauona kama ni mji unaopendeza, unaosifiwa, sisi tunatangaza Zanzibar ni njema atakae aje lakini wageni wanakuja wakija waone kama kweli Zanzibar ni njema atakae aje. Mtu kuiga jambo ambalo ni zuri si kosa, hata Mtume (*S.A.W*) alisema anampenda sana mwizi, lakini sio yule mwizi anayekwenda kuiba vitu vya watu, ni mwizi anayeiba mambo mazuri, anayeona jambo zuri watu wanakwenda wakikaa darasani wakisoma sana na yeye akaiga, anamuona mwenzake anasali sana na yeye akaiga, ndio wizi aliosema anaupenda. Sasa na sisi kuiga jambo zuri si kosa.

Mhe Naibu Spika, ukienda hapo Dar es Salaam tu utaona Manispaa mote mle kwenye *round about* wanaweka majahazi, wale tunawashinda kwa uvuvi, lakini wameweka majahazi, picha za samaki, kwa nini na sisi mji wetu usipendezeshwe? Halafu kwa nini kila unapopita mji wetu unaona kuna taka, hapa pana jaa, pale jaa, kwa nini wasitafute sehemu maalum ya kuweka jaa. Mimi nasema tena kwamba pale Darajani hapafai kuwekwa jaa kwa sababu pale ni uso wa mji na ni kitovu cha mji, jamani ukipita pale ndipo penye watu wote lakini hiyo harufu iliyokuwepo huwezi kukaa, hata kule kupita basi ni tatizo, kwa nini Manispaa wasijitahidi wakauweka mji ukawa na mazingira mazuri.

Hivi sasa tushaona kama zile taa ndio zimekwisha zote, lakini naamini labda wataweka nyengine mana wanachimbua chimbua. Kwa hiyo, Manispaa wajitahidi bado ni wajibu wao, pesa zinazokusanywa kwa ajili ya Manispaa zifanye kazi kwa ajili ya mji wetu, kodi zinazokusanywa tunataka kuona mji wetu ni mzuri na watu watakuwa hawana cha kusema.

Halafu suala la magari kutapakaa mji mzima, kwa nini hatuweki vituo kama wenzetu. Wenzetu wana vituo maalum isipokuwa vituo vya kushushia watu tu, lakini nani asiyejua kama kituo cha magari Dar es Salaam ni Ubungo. Kwa hivyo na sisi tungeweka sehemu maalum tukajua kama ni hapa, lakini sasa hivi mji wetu umetapakaa magari. Ukienda Baraza la Wawakilishi la zamani kuna magari, ukija Makao Makuu ya CCM pana magari, ukienda huko Darajani kwenyewe pana magari, ukienda Malindi ni kituo cha magari, kwa nini tusiweke sehemu maalum ya kituo cha gari ikajulikana kama hii ni sehemu ya kituo cha magari. Sasa tumeeneza mji umekuwa ni sokoto tu hujui kinachoendelea, mji wote uko wayuwayu kwa nini tunauweka hivi mji wetu. Kwa hivyo, naomba Manispaa wajipange vizuri Mhe. Waziri waweke sehemu maalum tujue kama hapa ndio kituo cha magari. Hilo ni moja.

Suala jengine wafanyakazi wa Manispaa mpaka leo hii nyongeza ya mishahara inayoongezwa wao hawajapata kwa nini? Hata kama hili suala ni la utumishi lakini kwa sababu wewe ndiye dhamana na msimamizi simamia uone Manispaa kama wanapata haki zao nyongeza ya mishahara, hawa hawajapata wapate mishahara yao na wao, nyongeza yao ni haki yao kila mmoja, Rais akisema ongeza kwa wafanyakazi basi ongeza kwa wafanyakazi wako wote sio kuna wengine wapate na wengine wasipate. Namuomba sana Mhe. Waziri na hili alisimamie wapate nyongeza yao ya mishahara.

Mhe. Naibu Spika, jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la Mabaraza ya Halmashauri za Wilaya. Kwanza 'Mcheza kwao hutunzwa', kwa hiyo nataka niwatunze watu wangu wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kukusanya mapato vizuri na kuongeza mapato wakapita yale malengo waliyokusudia. Walikusudiwa kukusanya shilingi 77 milioni lakini wamekusanya shilingi 99 milioni. Kwa hivyo, nawapongeza sana na nataka waendeleze kufaya juhudi zaidi kwa sababu mimi nikija hapa nikiona hivyo nafurahi.

Lakini wakati huo huo hawa madiwani kama serikali haitaki kuwalipa mishahara basi Mkurugenzi awasimamie aone kama wanalipwa pesa zao zile wanazozikusanya maposho mazuri ili yawasaidie. Lakini kama inawezekana hasa na wao ni bora kulipwa mishahara kama viongozi wengine wa kuchaguliwa wanavyolipwa mishahara.

Jengine ni kwamba bado madiwani hatujawapa dhamana zao, kwa nini hatuwapi fursa ya kuamua tunawanyima haki zao na wao wana haki ya kuamua. Mfano halisi ni kwamba mimi nalalamikiwa na madiwani, madiwani wote walioko Pemba wanasema kama Afisa Mdhamini Pemba amefanya kitendo bila ya kuwashirikisha, hata kama ni jambo zuri lakini kwa nini asiwashirikishe, angekaanao kitako wakapanga, wakakubaliana, lakini sasa aliamua tu peke yake alikaa yeye na Makatibu wa Halmashauri za Wilaya za Pemba wakapanga safari ya kwenda Tanga na

pesa hii haimo kwenye bajeti iliyopita, wakachukua pesa wakenda Tanga wakakaa siku sita kule, hata kama walikwenda kujifunza lakini kwa nini hawakuwashirikisha hawa madiwani wakakubaliana.

Kwa hivyo, wanalalamika kwamba wao hawashirikishwi na ni kweli hatuwashirikishi tunawanyima nafasi zao, wao wana haki kubwa ya kuamua. Hili ni kosa kwa sababu kama halimo kwenye bajeti wao wamekataa hivi sasa kuidhinisha pesa za bajeti hiyo kwa sababu hawakuzipitisha wao. Mhe. Naibu Spika, na hili ni tatizo madiwani lazima tuwape nafasi ya maamuzi tusikae tukaamua pekeetu bila ya kuwaambia na wao.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu hiyo hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, aliyekuwa katibu wa Halmashauri ya Micheweni alikwenda kusoma, bahati nzuri kenda kuongeza maarifa na ujuzi na kesharudi yupo, lakini wakati huo huo katibu aliyepo wa Halmashauri hiyo anakaimu. Sasa kukaimu huku kutakwenda mpaka lini na yeye keshakaimu muda mwingi? Namsifu hapa kama amekusanya vizuri sasa ule ukaimu tunataka uondoke pamoja na huyo aliyekwenda kusoma apangiwe sehemu nyengine awekwe afanye kazi zake.

Mhe Naibu Spika, mimi leo nilikuwa sitaki niseme sana nilitaka kusema kidogo tu. Kwa hiyo, baada ya kupata maelezo mazuri ya hayo niliyoyazungumza basi nitakuwa sina pingamizi na Mhe. Waziri. Lakini namuomba sana afanye jitihada Manispaa nao waendelee kufanya juhudi tuone mji wetu unang'ara. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante kwa kunipa fura hii na mimi kupata kuchangia kidogo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Kabla sijaanza mchango wangu kwanza napongeza hotuba hii kwa ilivyopangika vizuri sana na inatia moyo.

Mhe. Naibu Spika, navipongeza vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi zao wanazozifanya na jitihada zao. Naishauri serikali kupitia wizara hii kwamba vikosi vyote viangaliwe maslahi yao ili yawe mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika mchango wangu nakwenda katika ukurasa wa 73 ibara ya 187 Kikosi cha Zimamoto. Kikosi hiki kwa kwetu Zanzibar ni kikosi muhimu sana, lakini kikosi hiki bado kina ufinyu wa zana hasa magari, magari ni kidogo na kama tunavyoona kwamba mji wetu wa Zanzibar sasa umekua sana na hasa ukichukua Wilaya yetu ya Kaskazini ni wilaya ambayo imekua sana kwa majumba, mahoteli, lakini bado tuna vituo kidogo sana ukilinganisha hiyo Kaskamzini yenyewe na Zanzibar nzima. Kituo kwa Kaskazini ninachokiona kidogo sana kiko maeneo ya Nungwi, lakini kituo kama kile kama moto unatokea sahemu za Matemwe kule basi zinaweza kuungua nyumba zote haijafika gari ya Zimamoto. Kwa hivyo, naiomba serikali kupitia wizara hii vikosi vya Zimamoto viongezwe Zanzibar.

Vile vile kikosi hiki wakati kinapofika sehemu ya tukio wana matatizo ya maji, inabidi wakizima moto maji yanamaliza mpaka waje Makao Makuu. Sasa kutoka Matemwe mpaka Makao Makuu hata wakifika pale hiyo nyumba itakuwa ishaungua na watu washateketea, kama itakuwa nyumba mbili basi zitakuwa 50 zishakwisha. Kwa hiyo, naiomba serikali ihakikishe kwamba ndani ya vituo vyetu viwemo visima ili wale Zimamoto wakija wapate maji pale pale na kuweza kuendelea na kazi.

Mhe. Naibu Spika, niendelee na sehemu hii hii ya vikosi. Vikosi vyetu vinahitaji vijana kuajiriwa lakini bado kuna baadhi ya majimbo ajira za vikosi hazijafika kama inavyostahiki kama sehemu nyengine, hasa ukienda katika jimbo langu la Matemwe bado vijana wanahitaji ajira za vikosi lakini ajira hizo hazijafika. Kwa hivyo, naiomba serikali itupe na sisi ajira za vijana ndani ya vikosi vyetu vya SMZ kama KMKM, Zimamoto, na vyenginevyo.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika sehemu hizi za ajira, ijapokuwa serikali haijakuwa na nafasi zaidi ya kuajiri vijana, lakini serikali inaweza kufanya mpango wakawakusanya vijana ili kuwasaidia na kuwafungulia benki wakawakopesha fedha na kuweza kujiajiri wenyewe. Kwa sababu serikali haitakuwa na uzito mkubwa wa kuwaajiri watu wote, lakini serikali ifanye huduma ya kufungua mabenki kwa kuwakusanya vijana wakawakopesha fedha.

Nikiendelea katika mchango wangu kama wenzangu walivyosema sehemu yetu ya Manispaa ya Mji ni chafu. Kweli Manispaa yetu ya mjini ni chafu kimazingira ya biashara zinavyofanywa, chafu kimazingira ya magari yanavyowekwa, chafu hata ujenzi wenyewe hautambulikani. Kwa hivyo, naiomba serikali kwanza iwaangalie wale wananchi wanaofanya biashara ndogo ndogo kama mama ntilie, wauza machungwa, karanga, wahakikishe kwamba wanawekwa sehemu maalum ambapo hapo wanafanya biashara zao kwa vizuri. Kwa sababu biashara inawekwa barabarani na tunaambiwa sasa hivi mtu ni afya, wali unauzwa barabarani sasa afya hizi zitapatikana wapi wakati

huo mji wenyewe umewekwa kiuchafu. Kwa hivyo, serikali iangalie wale wauza biashara wahakikishiwe wanawekwa sehemu ambayo inaridhisha hata wageni wetu wakija wawe wanatamani kula.

Ukienda kwenye magari serikali naiomba kupitia wizara yako ihakikishe kabla ya watu kuwatimua watengewe sehemu ya kuwekwa tujue hapa wamewekwa, lakini sasa watu wanapewa amri waondoke bila ya kuwekwa pahala halafu inakuwa zogo, nchi yenyewe ni ndogo, mji wenyewe mdogo , magari yashakuwa mengi mara moja zinatokea ajali.

Kwa hivyo, ninaiomba wizara kwamba iwahakikishie wananchi kabla ya kuwaondoa wawatengee sehemu wajue kwamba hapa ndipo tulipowekwa. Haidhuru mtu wakati mwengine anaendeshwa kwa maarifa, anaendeshwa kwa magongo, lakini yale magongo mpige wakati ushamwambia hakusikia, sio hujamuelimisha mtu unakwenda kumvunja kwa magongo itakuwa tunakwenda vibaya sana wananchi wetu watatuelewa vibaya, tuwawekee sehemu, tuwajengee sehemu, tuhakikishe hapa pazuri wamekaa na ile afya binadamu anaweza kuwa nayo kutokana na sehemu anazowekwa. Sehemu ikiwa nzuri na mwanadamu anakuwa mzuri, sehemu ikiwa mbaya hata mwanadamu naye anachafuka. Kwa hiyo, mimi tukipinda pale mjini tunaona vituo kama pale Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi, Mnazi Mmoja, ukienda Darajani kule hujui unakwenda wapi.

Kwa hivyo, naiomba wizara na Mhe. Waziri awahakikishie wananchi sehemu za kuuza biashara ziwekwe pazuri ili wananchi wapate kupumua kidogo. Wananchi wanahangaika sana kibiashara, sisi tunawaonea huruma. Mhe. Waziri akija hapa atuhakikishie kwamba madereva wanawekewa sehemu gani, atuhakikishie mama ntilie wanawekwa sehemu gani, ili mji wetu uwe mzuri na unaoeleweka. Kwa sababu nchi yetu sasa hivi ni nchi ya kitalii, wanakuja watalii wengi sana na mtalii naye na hata sisi hatutaki ule uzuri! Tunautaka. Kwa hiyo, tujitahidi na nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi madereva kuwawekea sehemu ambayo itafaa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Pia nampongeza Mhe. Waziri kwa kuandaa hotuba hii pamoja na watendaji wake wote, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tawala, Wakuu wa Vikosi.

Mhe. Naibu Spika, nitachangia katika maeneo kama matatu hivi, nitachangia katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, katika Idara Maalum ya SMZ na katika Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ina jukumu la kuhakikisha amani na utulivu vinadumishwa na kuimarishwa. Hapa pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri na vikosi vyote kwa kudumisha amani na utulivu katika nchi yetu. Mheshimiwa amani ni thamani, Wahenga wamesema: "Bora kula ugali mkavu kwenye amani kuliko kula wali nyama vitani", naomba tudumishe amani yetu.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye Miradi ya Maendeleo katika hiyo hiyo Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kuna miradi humu imeorodheshwa mingi tu na hatua mbali mbali ambazo zimefikia miradi hiyo. Lakini kuna miradi ambayo mingi haijakamilika na pengine kuna changamoto ambazo zimefanya miradi hiyo kukamilika na hasa suala la fedha. Lakini hapa nilikuwa niiombe tu Serikali ichukue juhudi za makusudi ili kuikamilisha miradi hii. Kwa sababu ni miradi muhimu, miradi ambayo itawasaidia wananchi wetu, na pia miradi mingine itawasaidia kupata ajira vijana wetu.

Lakini pia hapa nitoe wito kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuhusu miradi ambayo imo katika majimbo yetu. Nilikuwa naomba kama kuna miradi ambayo Mwakilishi au Mbunge aliyepita pengine kauanza lakini kwa bahati mbaya hajarudi katika jimbo lake, ni vyema tungekuwa tunaiendeleza ile miradi kuliko kuanzisha miradi mingine mipya matokeo yake kwenye jimbo kunakuwa na miradi mitatu minne inakosekana kukamilika kutokana na ukosefu wa fedha.

Kwa mfano pengine Mwakilishi aliyepita kaanzisha mradi mzuri lakini hakubahatika kuendelea na kipindi kinachofuata nilikuwa nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi atakayeshika nafasi ile ya jimbo aendeleze mradi ule ukamilike halafu aanzishe mradi mwingine. Kuliko kila akija Mwakilishi au Mbunge analeta mpya, matokeo yake kwenye jimbo kunakuwa na utitiri wa miradi ambayo haikamiliki.

Ni vyema kuendeleza ile miradi ambayo imeachwa na yule Mwakilishi au Mbunge ambaye alikuwepo, na hiyo itasaidia kupunguza utitiri mwingi wa miradi ambayo inakuwa haikamiliki na kila mwaka utaikuta kwenye kitabu cha hotuba imo ambayo haikamiliki.

Mhe. Naibu Spika, nizungumzie Serikali za Mitaa katika suala zima la malipo kwa wazee. Mhe. Mwenyekiti, malipo kwa wazee wenzangu wameeleza ni elfu tano kwa mwezi. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna makundi mawili katika malipo hayo. Kuna kundi ambalo watu wanalipwa kutokana na daily paid ambayo wamefanya, wamefanya kazi miaka mingi lakini walikuwa hawajaajiriwa. Na kuna na wale wazee ambao wanapata kama msaada. Mimi nilikuwa nadhani Serikali iliangalie hili kwa sababu sasa hivi maisha yamepanda, elfu tano kwa kweli haitoshi. Najua Serikali ina nia njema tu lakini naomba kwa hili pia iwaangalie wazee hawa waongezewe hizi pesa ifikirie ni kiasi gani ambacho itaweza kuwasaidia kutokana na ukiangalia hali nzima ya maisha ilivyopanda.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye mapato ya Serikali za Mitaa. Kitabu kimeeleza kwenye kiambatanisho hapa mapato ambayo yamekusanywa katika Manispaa na Halmashauri mbali mbali katika Mikoa yetu. Na katika kiambatanisho hicho imeelezwa kupita malengo ambayo yalikadiriwa, karibu asilimia 82 ya mapato yamekusanywa. Hapa nina wito tu nilikuwa naomba hizi Halmashauri na Manispaa, hizi pesa ambazo zinakusanywa basi watumie pesa hizi kwa malengo yaliyokusudiwa na si vyenginevyo, ili kuleta ufanisi na maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hapa nitagusia kidogo katika mamlaka hii hii ya Serikali za Mitaa kuhusu suala zima la pale zinaposimama daladala Afisi Kuu ya Chama Kisiwandui. Naomba Wizara ijipange kuangalia suala hili. Pale sasa hivi kumekuwa ni tatizo, na ukiangalia hasa kuna ofisi yetu ni jengo la kihistoria, Rais wetu wa kwanza Marehemu Abeid Amani Karume aliuawa na kuzikwa pale. Kwa hiyo kumekuwa na muingiliano mkubwa wa harakati nyingi, na ukiangalia sasa hivi wafanyabiashara wanavamia sana sehemu ile.

Kwa hiyo ule usalama nao unakuwa si mzuri hasa kwa wanafunzi wetu wanaosoma pale Skuli ya Kisiwandui. Mimi nilikuwa nahisi Wizara ijipange katika hili iangalie sehemu nyengine ili kuweka hali nzuri katika sehemu yetu hii na kuwalinda wanafunzi wetu ambao watarithi. Wafanyabiashara nao kama unavyowajua wanaweza wakawapotezea mwelekeo mzima wa masomo yao. Kwa hiyo naomba Wizara ijipange iangalie nini itafanya kutokana na hali ile irekebishe. Kwa sababu wale wafanyabiashara wakizoeleka pale pia ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika Idara Maalum za SMZ. Mhe. Naibu Spika, wenzangu wameeleza hapa suala zima la kuwafikiria mazingira yao ya kazi. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Kwanza niwapongeze kwa kuhudhuria vizuri katika sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi wamefanya kazi nzuri vikosi vyetu. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, suala la maslahi liangaliwe, vitendea kazi, mafunzo kwa wafanyakazi, hawa ni watu muhimu katika nchi yetu. Naomba suala hili Mhe. Waziri uwafikirie na uwaangalie kwa jicho la imani kabisa.

Mhe. Naibu Spika, katika hiyo hiyo Idara Maalum nitazungumzia suala zima la uajiri wa vikosi vyetu hivi. Mhe. Naibu Spika, suala la uajiri ni muhimu lakini mimi hapa nilikuwa naomba Mhe. Waziri wanapofanya uajiri kuhusu vikosi vyetu hivi naomba wafanye uchunguzi wa hali ya juu. Nasema hivyo kwa sababu kazi hii inahitaji uzalendo, uadilifu, uaminifu na umakini wa hali ya juu. Kazi ya vikosi ni kazi muhimu sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kama askari wetu hatokuwa na uzalendo atakuwa mhalifu, kama askari hatokuwa na uaminifu atakuwa mwizi, kama askari hatokuwa na uadilifu atakuwa mzembe. Kwa hiyo nahisi sehemu hii ya ajira ya Tume ya Utumishi iangalie suala zima la ajira kwa vikosi vyetu hivi wawachunguze wajue wanawaajiri vijana wetu ambao wana sifa hasa za kuajiriwa.

Jengine pia naiomba Wizara najua inalifanya hili, na kama hailifanyi nilikuwa naomba ilifanye, na kama inalifanya naomba wazidishe. Iweke utaratibu maalum wa kuwachunguza hawa vikosi vyetu ili kuwapima uadilifu wao, uaminifu wao, utendaji wao kwa kila baada ya muda fulani. Hii itasaidia kuboresha mazingira mazuri ya watendaji hao, itasaidia kufanya kazi zao kwa uadilifu na kwa uaminifu.
Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika vikosi hivyo hivyo lakini kuna suala zima ripoti ya Kamati ilieleza kuhusu Kiwanda cha Viatu kwa wale vijana wa Valantia. Ni hatua nzuri ambayo imefikiwa lakini katika ripoti imeelezwa kuna changamoto ambazo ni suala zima la wataalam. Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri hapa achukue jitihada za makusudi ili kuona kwamba hichi kiwanda cha hawa vijana ambao wamejitolea wanafanya kazi hizo kiweze kuendelea, kiweze kuzalisha vizuri na hatimaye kupata soko ambalo litaweza kuwasaidia kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono asilimia mia moja.
Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye aliyetuwezesha leo hii kuwa watu katika afya njema. Lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii.

Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote ambao waliomsaidia kwa namna moja au nyengine ili kufanikisha kuleta hii hotuba ambayo mimi nasema katika Wizara moja wapo na hii ni Wizara nyeti kwa kweli kwa Serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, najua kwamba watu wamechangia lakini na mimi nitapita kwa baadhi ya mambo ambayo nayaona yanafaa kuyatilia mkazo. Mhe. Naibu Spika, kwanza nije katika vikosi vyetu vyote vya SMZ. Mhe. Naibu Spika, vikosi hivi ndio vikosi mama kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini pia niseme kwamba ukishakuita jeshi, basi huwa jeshi halifanyi maandamano, jeshi hali haligomi. Kwa nini nikasema haya. Ni kwa sababu nitaomba Serikali yetu kwa moyo mkunjufu kabisa Mhe. Naibu Spika, kwamba jeshi hili hivi vikosi vyetu vya SMZ viangaliwe tena upya kwa maslahi yao ya kuwaletea na wao. Kwa sababu ni vikosi ambavyo kwa kweli vinafanya kazi mno. Pamoja na yote lakini vinafanya kazi sana.

Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali kwa makusudi na siku zote tunalizungumza suala hili. Naomba safari hii Serikali ihakikishe kwa makusudi inawapatia maslahi yao, maslahi ya kijeshi hasa, sio maslahi ya mchezo. Wawe na nyumba nzuri za kuishi, wawe na vitendea kazi, wawe na mambo ambayo wewe ukishakiita kitu jeshi, basi ni jeshi la aina yoyote ile linaitwa jeshi. Nasema haya kwa sababu hawa kiutaratibu na kisheria hawaandamani wala hawagomi, wao ni kusonga mbele tu, amri ni amri tu. Kwa hiyo nasema hili kwa mkazo zaidi nakuomba sana Mhe. Waziri.

Lakini kuna vikosi nivisemee vile vile, kama kikosi cha KMKM. Mhe. Naibu Spika, kikosi hichi kinafanya kazi kubwa sana, na ukiacha kazi zao za ulinzi lakini pia hata wakati wa zao la karafuu kwa kweli watu ambao wanaifanya kazi kubwa sana ni KMKM. Naomba sana Mheshimiwa zile ahadi ambazo wanapewa wakati wa kulinda zile karafuu basi zitimizwe kikamilifu.

Hata Jeshi la Polisi pia na wao wanakuwa ni miongoni ambao wanafuatana na watu hawa ili kuhakikisha kwamba karafuu zetu hazivuki. Lakini kuna wengine hawapewi maslahi yao yale yanayokubalika. Kwa hiyo, namuomba sana Mhe. Waziri hili alitafakari kwa sababu ni miongoni binadamu ni binadamu hawa hawa wanaweza kugeuka wakasema aah! tuachie bwana hatupewi na sisi haki yetu karafuu tuziachie ziende zake. Mhe. Naibu Spika, hili nalisema kwa makusudi.

Lakini jengine nije Chuo cha Mafunzo. Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze sana chuo hiki jinsi wanavyohangaika kuleta maendeleo yao katika chuo chao. Kwanza niiombe Serikali, sasa hivi mimi napitia pale naona kwamba wametoa maduka upande wa mkono wa kulia kama unakwenda zako Kiwanja cha Watoto. Lakini nitawaombea kwamba na upande huu wa pili pia wapewe sehemu waendeleze maduka kama walivyofanya mwanzo. Kwa sababu hii ni mojawapo na wao kuwashajiisha kwa kujitegemea baadhi ya mambo sio kila jambo litegemewe na Serikali tu. Mhe. Naibu Spika, hilo namuomba sana Mhe. Waziri.

Lakini pia nimpongeze Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuweza kutoa ahadi siku aliyokuja akazindua hospitali ile ya KMKM, akatoa ahadi kwamba atasaidia vitanda na vitu vingi ambavyo kwa kweli vitaweza kuiendesha hospitali ile bila ya matatizo. Hapa nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza. Na pia nimpongeze na Mama Salma Kikwete kwa sababu na yeye Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano pia alisema na Mama Kikwete atasaidia hiki na hiki. Kwa hiyo hili nataka nijue je, yale mambo yamekamilika au bado.

Lakini pia nije katika suala zima la Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU). Mhe. Naibu Spika, hili tunaliita ni Jeshi la Kujenga Uchumi, sasa naomba Mhe. Waziri aje anambie ni mipango gani na gani ambayo wameipangia jeshi hili la kujenga uchumi kwa sababu tunasema ni Jeshi la Kujenga Uchumi. Lakini niseme tu kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo lazima tuyaweke kipaumbele. Kwa mfano wana mabonde yao wanalima hawa Chuo cha Mafunzo, na kuna mabonde mengine ambayo ni ya kutaka kumwagiliwa maji hebu tuwafanyie basi angalau haya mabonde tuwape na wao waweze kufanya mambo yao ya kilimo ipasavyo.

Lakini nije katika Kikosi cha Valantia. Mhe. Naibu Spika, mimi nasema bado kwa sababu sisi ni kikosi cha mwanzo kabla hata mambo hayajakuwa ya Vikosi vya SMZ. Naiomba sana Serikali kwa sababu valantia ni sawasawa na jeshi kwa maana na sisi tumeshapitia huko. Kwa hiyo naomba Serikali kwa makusudi ikiangalie kikosi hichi cha valantia ni kikosi ambacho kwa kweli kinajitahidi, lakini ni kikosi kimojawapo kipo nyuma sana kimaslahi, na kipo nyuma sana kwa mazingira yalivyo.
Naomba sana Serikali mtu hutoa sadaka nyumbani mwake kwanza halafu baadae ndio akatoa sadaka kwa wengine. Kwa hiyo, naomba hichi kikosi ni muhimu, hichi ni kikosi toka wazee wetu wamekifanyia kazi sana. Kwa hiyo niseme tu Mhe. Waziri pia katika mambo yako yote lakini hichi kikosi ni muhimu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije kwenye Zimamoto. Zimamoto watu wamesema, lakini kila siku tunasema hapa na tuliahidiwa kwamba yatafutwa magari ya Zimamoto. Lakini naomba Mhe. Waziri kwa sababu Waziri huyu ndio kwanza bajeti yake ya mwanzo toka kupewa hii Wizara, aje atufafanulie haya magari ya Zimamoto yako wapi tuliyoahidiwa hapa. Na Waziri wa Fedha mwenyewe alizungumza hapa akasema tunaagizia. Na kila siku tukikaa fedha jamani vifaa vinapanda mambo haya tutakuja kushindwa nchi hii sisi tutawaacha wananchi wetu wanakufa hivi hivi ovyo ovyo. Kwa hiyo na hilo pia namuomba Mhe. Waziri.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nije katika Baraza la Manispaa. Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na Mkurugenzi aliyepita akafanya utumbo. Sasa tuna Mkurugenzi huyu mwanzo ameonesha nia yake nzuri ya kutengeneza mambo, lakini sasa sijui hapa katikati kafikwa na maafa gani. Namuomba sana Mkurugenzi huyu ametutia moyo basi asituvunje moyo. Kwanza mimi kila nikisimama hapa kuzungumza Mhe. Naibu Spika, nasema jamani zile *by laws* za nyuma zilizokuwa zinafanya kazi vizuri kwa nini hatuzitumii. Zamani kulikuwa na *inspectors* kwa kila mtaa, kwa kila mji, na Manispaa ina wafanyakazi wengi sana wengine wanazurura tu ovyo. Kwa nini hatuweki taratibu za kwamba kila mtaa wakachaguliwa *inspectors* watatu au wanne kuhakikisha usafi wa mtaa ule na aliyekuwa anafanya kwa makusudi ni kupigwa faini. Na ndio maana *by laws* tukasema ziwekwe hizi maana yake ni vile.
Namuomba sana Mstahiki Meya pamoja na Mkurugenzi wake, pamoja na watu wetu hawa ambao wanaisaidia sana Manispaa, Madiwani.

Kwa sababu Madiwani ndio kiungo kikubwa sana cha kila Jimbo na kila Shehia. Naomba sana pia Mhe. Waziri Madiwani na wao walipwe japo pesa angalau iwe afadhali, na wa kulipa ni Manispaa kwa sababu ndio wanaowatumia Madiwani, na Madiwani ndio wanaoidhinisha fedha zote za matumizi. Sasa ikiwa mtu anaidhinisha fedha za matumizi yeye mwenyewe hapati chochote maana yake nini. Naomba suala hili Mhe. Waziri uje ulitafakari na ni imani yangu kwa sababu wewe hutaki jambo lako lisemwe. Ni imani yangu kwamba utaitengeneza vizuri sana Manispaa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, katika Manispaa hii hii nije kwanza Mkunazini. Mhe. Naibu Spika, Mkunazini ukitaka kwenda pale benki ni matatizo, kuna mikokoteni inawekwa pale pale kwenye barabara, gari zina-*park* huku na huku, ili mradi ni mchafukoge. Kwa hiyo naiomba Manispaa pale si pahala pa *parking* za gari kwa sababu ile njia yenyewe ni ndogo. Kwa hiyo wafanye kila njia kwamba huku na huku tusiwe na *parking* ya gari. Hilo namuomba sana Mhe. Waziri na wenyewe wananisikia Manispaa wapo hapa.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu suala la *Airport.*Kuhusu *airport* Mhe. Naibu Spika, hivyo kweli kuhusu *airport* mtalii akiteremka pale anakuja anaona uso wa *airport* upo vile pale, vibanda havifahamiki, urojo unauzwa pale. Kwa nini Manispaa hawatengi sehemu ile wakaijenga vizuri kisha wale wale waliokuwa pale wakaweza kukaa angalau ikaleta sura *airport* yetu. Mtalii au mgeni yeyote anapateremka pale akaona hii kweli, huu ndio uso wa *airport.* Lakini pale kuna kila aina ya balaa, aina ya balaa yote yapo pale. Mhe. Naibu Spika, mchafu koge. Mhe. Naibu Spika, naiomba wizara hii na Mhe. Waziri ninakuamini.

Mhe. Naibu Spika, lakini sasa nimalizie kwa kusema kwamba nije na Baraza letu haya katika Baraza la Mji la Wete. Mhe. Naibu Spika, mimi fahamu yangu pale soko la mji wa Wete, marehemu mama yangu na ndugu zake walikuwa na sehemu hizi mbili; moja imejengwa jumba la ghorofa upande huu wakanyang'anywa lakini na pale sokoni kwenye soko la mji wa Wete kulikuwa na hoteli zilikuwa upande huu huku, hivyo vilikuwa ni viwanja vya marehemu mama yangu aliyenizaa mimi.

Lakini leo ninashangaa wao wamenyang'anywa hawakuleta kesi wala hawakufanya chochote. Lakini sasa linalonishangaza pakapewa mtu mmoja anaitwa Mapete. Lile soko Mhe. Naibu Spika, ni la enzi na enzi, toka 1963.

Leo huyu Mapete kapewa kalizungusha mabati ambayo na pale pana soko la samaki, pana soko la kuuza mboga mbogo, lakini pia pale ni *stand* ya magari, kwa miaka yote Pemba pale ni *stand* ya magari. Toka mimi zijazaliwa mpaka nimezaliwa. (*Makofi*)

Sasa nimamuomba Mhe. Waziri hii bajeti yako itakwama kwa sababu huyu Mapete kazi yake ni uharibifu tu. Maana mimi ninamjua tumecheza pamoja, kazi yake ni uharibifu, alinunua meli imekaa meli imekwenda na maji. Sasa naomba hili uje unieleze vizuri ilikuwaje kuwaje mpaka akamilikishwa Mapete, kwa kitu gani wakati watu pale *years and years*, aje mtu ambaye kwa kweli aje achukue tu hivi hivi. Hilo Mhe. Waziri ninaliomba kwa sababu mimi pale mfano wake ni kwetu na katika mtaa huo huo niliozaliwa.(*Makofi*)

Kwa hivyo hili uje unipe maelezo mazuri. Waulize watu wako vizuri unije maelezo. Na maelezo haya hayakunitosheleza tutakwenda mimi na wewe Pemba mpaka nijue chanzo chake ni kitu gani. Kwa sababu pale wenyewe Baraza la Mji watanyang'anywaje na ile ni sehemu yao maisha yote. Kwa nini wanyang'anywe Baraza la Mji apewe mtu binafsi, kwa ubinafsi wake tu, kwa nini? Mhe. Naibu Spika, hili litalivalia njuga. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, nimezungumza mengi lakini niseme tu Manispaa wana kazi, nirudie tena maana nilisema ninayachangia haya yote ili yapate nafasi. Lakini Manispaa wana kazi na sisi, mimi nimeshasimama mara nyingi. Waje wachukue kwetu sisi hatutaki tulipwe, waje wachukue maoni ambayo tutawapa mipango mizuri, kwani kuna kitu gani, ukaja ukaniuliza tu Mhe. Asha Bakari Makame haya pale *airport* nipafanye vipi. Kwa sababu na wao wanasafiri kila siku. Sasa hawaoni kwa wenziwao wanafanya sehemu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hayo sitovumilia, hayo mengine ninayazungumza tu lakini kubwa ni hili suala la Wete. Kwa sababu niseme kwamba suala hili ni nyeti, si suala la kuchezea. Kwa hivyo Mhe. Waziri aje anieleze vizuri. (*Makofi*)

Baada ya kwisha kusema hayo, Mhe. Naibu Spika, ninasema sijui niunge mkono au ningoje maelezo lakini kama sikuiunga mkono nitakuwa hili suala la mji wa Wete halitopata ufumbuzi. Kwa hivyo ninaunga mkono. (*Makofi*)

Mhe Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Bakari Makame. Sasa nafasi ya Mhe. Rufai Said Rufai baadae Shadya Amour Mohammed na baadae Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe.Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Allah asubuhi hii kutuamsha tukiwa wazima na mimi nikapata nafasi hii kuweza kutoa mchango wangu mfupi ndani Ofisi hii ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza na Baraza la Manispaa. Mhe. Naibu Spika, hii ni taasisi muhimu ndani ya wizara hii. Ndani ya wizara hii, hii ndio roho Baraza la Manispaa kwa sababu nchi yoyote kitambulisho chake ni ule mji wake mkuu. Kama Zanzibar tumeshaeka mji wetu mkuu ni Darajani basi inatajwa Darajani inajukana kama hiyo ndio Zanzibar.

Lakini mpaka muda huu mji mkuu wa Zanzibar haujulikani ni wapi. Kwa hivyo hili ni tatizo bado. Lakini Baraza hili la Manispaa, mimi ninashukuru sana ama ni mahodari kweli kweli wa kukusanya mapato. Hili wanalifanyia kazi ipasavyo. Mhe. Naibu Spika, hakuna kichochoro kitakachosimama gari pale, gari hiyo ikakosa kutoa mapato, hata kwa siku ile tano kumi. Hakuna mfanyabiashara, hata yule wa shilingi ishirini wa mkononi wa njugu akawahi kuzunguka katika mji ule akakosa kutoa mapato ya shilingi elfu kwa siku.

Hakuna muuza mkate anakosa kutoa mapato ya shilingi elfu, hakuna mfanyabiashara yeyote ama wa duka au eneo jengine akakosa kulipa ada au kulipa leseni katika mji ule. Lakini pia hakuna mfanyabiashara aliyekosa kulipa fedha ya usafi, hakuna.

Mhe. Naibu Spika, haya ni mapato makubwa. Kama wananchi hawa wanatoa mapato, kwa nini mimi huwa ninajiuliza mji uwe mchafu hali kama hii. Ni sababu gani zinazosababisha huu mji uwe mchafu na wananchi wanatoa mapato. Jamani tatizo ni nini. Mimi ninajua tatizo. Tatizo ni kutokuwa na usimamizi uliokuwa imara. (*Makofi*)

Wananchi wanatoa mapato ya usafi, pesa zinakusanywa, Manispaa inapata fedha hizo lakini usimamizi hapana. Na nani msimamizi. Msimamizi ni kila mmoja wetu hasa katika yale maeneo ambayo ya Manispaa yaliyokuwa na wafanyabiashara wakawa wanasimamia katika ile biashara yale na ukusanyaji wa takataka zile. Mhe.Naibu Spika,

sisi tunatembea sana hapa mjini lakini hebu jaribu siku moja upite katika hizo garden za Manispaa zilizopo hapa *Barclays*, hebu ujaribu siku moja upite pale kwa miguu usikie hiyo harufu iliopo pale, kama moyo wako ni mdogo utatapika tu mbele ya watu.

Ile harufu mbaya iliopo pale na kwa nini. Mhe. Naibu Spika, hili ni tatizo. Mhe. Abdi Mosi Kombo hapa amesema kwamba nchi yetu inatembelewa na wageni, lakini na sisi wenyewe tunahitaji usafi. Sio kufanya usafi kwa ajili ya wageni tu, tufanye usafi kwa ajili yetu sisi wenyewe ili tuweze kuepuka maradhi na matatizo mengine mbali mbali. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hawa Manispaa hawatembei, hawafanyi ziara mbali mbali wakaona miji ya watu ilivyo. Kwa nini hatu-*quote* mazuri na kwa nini tunapokwenda katika Manispaa za watu wengine hatuwaulizi usafi huu ilikuwaje mpaka nyinyi mpaka mukawa wasafi kama hivi au tunatembea tu kwamba pana pesa ya ziada ipo twende na maeneo mengine ili tuzitumie hizi pesa tu. Lakini mule faida ya ziara zao hatuzioni, tunajifunza nini. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo hili ni tatizo. Kwa kweli mji wetu haupendezi kabisa. Mhe. Naibu Spika, lakini isitoshe upangaji huu uliowekwa ma-*stand*, kwa kweli baadhi ya maeneo tunahatarisha maisha ya wananchi wetu na mali za wananchi wetu. Mimi niseme hii stand hii iliyoekwa hapa barabarani Kisimamajongoo. Mhe. Naibu Spika, pale ni hatari, samahani pale ni Kisiwandui, ile pale ni hatari. Pale wakati wote pana msongamano wa magari, magari ya abiria, magari ya watu binafsi na magari ya serikali. Pia pale pana skuli, wanafunzi wanaingia na kutoka pale Mhe. Naibu Spika, inakuwa ni tatizo kubwa kabisa. Kwa kweli pale wakati wowote Mwenyezi Mungu atuepushie mbali lakini yanaweza yakaja kutokea matokeo makubwa. Kwa hivyo pale katika stand tumefeli, pale kwa kweli ni eneo moja baya sana tunahatarisha maisha ya wananchi wetu. (Makofi)
Mhe. Naibu Spika, lakini jengine kubwa pahali pakishakuwa na msongamano wa watu na pale kuna Ofisi ya Chama Tawala, ipo pale na ipo siku nyengine Mhe.Rais kile ndio chama chake, anahitaji kwenda kufanya vikao pale. Lakini leo watu wametawanyika pale, watu ni wengi na adui huwezi kumjua ni nani. Kwa hivyo pale Rais itakuwa hayupo katika eneo la usalama. Hivyo kuweka *stand* pale kwa kweli ni eneo moja baya sana katika eneo lililotengwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme kwamba Baraza hili la Manispaa katika kitabu chao hichi cha ufanisi wa kazi zao, wamesema katika utekelezaji halisi, wamejaribu kukata matawi ya miti na ukataji wa miti mibovu katika maeneo ya Mwanakwerekwe, Malindi, Darajani na ng'ambu imefanya hivyo. Lakini Mhe.Naibu Spika, bado hili tatizo lipo.

Ukitizama eneo la Maruhubi, hili eneo kwa kweli lina miti mibovu na tena mikongwe mno. Lakini mpaka yale matawi yake mengi yameinamia chini, yameingia barabarani. Isitoshe hivi sasa magari makubwa yanayobeba makontena yanapita katika barabara ile. Hasa huku ni kuhatarisha maisha ya wananchi na mali zao. Kwa hivyo yale maeneo ni maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa usafi ili kama haya magari makubwa yaweze kupita vizuri, lakini mpaka miundombinu ya simu na waya za umeme zipo karibu mno na barabara. Kwa hivyo mimi ningemshauri sana Mhe. Waziri, suala hili aweze kulisimamia ipasavyo kabla halijatokea la kutokea miundombinu hii iweze kuboreka.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka nije katika Ofisi ya Usajili wa Kadi za Vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, hii taasisi inajitahidi kufanyakazi zake hasa unapoingia katika ofisi yao pale, kwa kweli ukenda utaona mambo yameandaliwa vizuri vya kutosha. Tuliwahi kufanya matembezi pale wakawa wanaperuzi baadhi ya wale wananchi walioandikwa zaidi ya mara moja na wakatuonesha kwamba wapo baadhi ya watu wameandikwa zaidi ya mara moja na wanaanza kuwafutafuta.

Lakini Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba uko kwenye idara kazi inakwenda vizuri, lakini kwenye hizo taasisi zao ndogo ndogo walizoziweka mawilayani, hizi kazi haziendi vizuri. Na utendaji hawa waliopewa majukumu kuchukua zile risiti za wananchi na kupewa vile vitambulisho basi haziendi vizuri na kuna baadhi ya watendaji hawa, kama mwananchi amekuja kudai kitambulisho lakini kitambulisho kile kimechelewa huambiwa uoneshe risiti yake ni kwamba kweli muda wa kuchukua kitambulisho umepita.

Lakini akishatoa risiti ile baadhi ya wengine tunasema, basi stashahada zao zile hawarejeshwi tena. Na mwenyewe anapoomba jawabu anayopata au lugha anayoipata inakuwa sio nzuri. Lugha zile kwa kweli hazileti faraja kwa wananchi wetu na hazileti sura nzuri ya kuijenga hii Ofisi ya Vitambulisho.

Kwa hivyo, baadhi ya watendaji wenu lugha wanazowajibu wananchi, kwa kweli sio lugha nzuri na si lugha rasmi na baadhi ya wale zile risiti zao hawawarejeshi wenyewe, hilo linakuwa ni tatizo Mhe. Waziri ndani ya ofisi yako hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kuna tatizo la kutolewa vitambulisho na kupewa mtu aliyekuwa hahusiki na kitambulisho hicho. Haya yameshatokea katika ofisi hizi zetu, Tume ya Vitambulisho ya Mzanzibari Mkaazi na hapa. Lakini nitakupa mfano tu uliotokea katika ofisi hii ya pili ya *ZEC*.

Mimi binafsi nilifuatilian tatizo la mwananchi wangu kwamba kuna muda mrefu kitambulisho chake hajakipata. Nikakifuatilia na kwa bahati nikakuta ofisini kipo kitambulisho hicho na muhusika akaniambia mwezi wa tatu vitambulisho hivi vitatoka katika mawilaya yao. Lakini bahati mbaya mno Mhe. Naibu Spika, siku moja mtu mmoja mwenye kitambulisho hicho hicho nilichokifuatilia mimi, alikipoteza Wilaya ya Mkoani ndani ya usafiri wa kutoka Pemba kuja Unguja.
Vilipotea vitambulisho viwili; kwa bahati vikatangaziwa vitambulisho vile na bahati nzuri mtu aliyetoka Micheweni akawepo yupo na kwa bahati nzuri mtu huyo huyo anatoka katika Shehia hiyo ninayotoka mimi. Kwa bahati nzuri hicho kitambulisho anamfahamu huyo muhusika wa kitambulisho hicho. Kwa hivyo kikatangazwa pale, kilipotangazwa akasema mimi huyu mtu ninamfahamu ninamjua ni cha fulani. Kwa hivyo kitambulisho kile akakichua yeye akakifikisha Wilaya ya Micheweni.

Kwa hivyo, akamuagizia muhusika kwamba bwana nimekiokota kitambulisho chako Mkoani. Kijana alipofika akamwambia mimi bado sijachukua kitambulisho, bado kitambulisho kipo ofisi kuu. Akasema hapana, kitambulisho chako kipo kimeokota Mkoani nimekabidhiwa mimi hichi hapa. Kukitazama ni kweli ndicho kitambulisho chake na kitambulisho hicho bado kipo ofisi kuu.

Kwa kweli hili ni tatizo sugu Mhe. Naibu Spika, umekosekana uaminifu na sheria na Katiba, zimeekwa kamati hizi hata kushitakiwa usishitakiwe. Lakini uaminifu umekosekana. Vitambulisho vinatolewa na wanapewa watu waliokuwa hawahusiki katika vitambulisho hivyo. (*Makofi*)

Kwa kweli itafika pahala tuondoshane haiba. Sisi tumewaamini wenzetu, lakini badala ya kule kuamini kwao hawatekelezi ule uaminifu kwetu. Kwa hivyo, hili Mhe. Naibu Spika, ni tatizo sugu na kwa kweli sio jambo zuri, wakati nyinyi mmeaminiwa mkaondosha uaminifu kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba sana tatizo hili lipo na nina ushahidi nalo na bado linaendelea. Lakini tunawaombeni sana wahusika muweze kusimamia vizuri masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie. Japokuwa umetoa *quotation* asubuhi kwamba tusirudie rudie, lakini mengine ni lazima tuzidi kuyawekea njia vizuri. Wenzangu wengi wamechangia hapa kuhusu vikosi. Ni kweli vikosi ni vyetu, hivi vikosi ni vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kila mwananchi wa Zanzibar ana haki na wajibu, kwa sababu kila mmoja analipa kodi ya nchi hii na katika kodi hizo na hawa watu wa vikosi wanapokea kodi hizo katika mishahara yao, sare zao na mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri, Mhe. Waziri anajitahidi sana kuwaajiri hawa watu wa vikosi, lakini ndani ya hotuba yake alituambia kuna sare na sijui viatu kama pea 2,000. Hivi tukisema viatu pea 2,000 za vikosi na vikosi vyote vinahitaji kuvaa buti, vinahitaji kuvaa sare na hawa vikosi mimi sifikirii kama ni 1,000. Hawa watu ni wengi na wanahitaji matunzo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri jukumu ulilonalo ni kubwa, wewe ndio roho ya ulinzi wa Zanzibar na wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu kumkuta mlinzi kavaa buti lakini ile soli ya chini imekatika, hii ni aibu. Mlinzi atakuwaje na pea moja ya kiatu hii ni aibu Mhe. Waziri, hili ni jambo muhimu Mhe. Waziri la kuwajali na kuwaenzi hawa vikosi. Hawa ndio wanaotufanya sisi tulale vizuri, sisi kila mmoja analala nyumbani kwake kwa wakati na muda anaotaka mwenyewe, lakini wao wanaukosa usingizi kwa wakati wake. Mtu analinda usiku anakuja kulala mchana, wakati mchana sio wakati wa kulala ni wakati wa kutafuta maisha, lakini yeye inabidi alale mchana ili usiku ahakikishe anafanya doria nzuri katika nchi. Kwa hivyo, kwanza ni kuwajali hawa kimatunzo ya sare na viatu ili waweze kufanya ulinzi vizuri.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala la mavazi ni suala muhimu kwa vikosi vyetu. Mhe. Subeit Khamis amesema hapa, kwamba hata anapokwenda likizo ile shilingi 100,000 hawapewi, halafu wewe unataka ulale vizuri na ulindwe

vizuri. Jamani kwa hivi hatufiki kabisa, wanapo kwenda likizo hawa vikosi basi wapewe maposho yao ya likizo. Kwa hivyo, tusiwafanye mpaka wakajihisi kama serikali inawadharau, hawana dhamani na hawana faida yoyote, hivi tutakuwa hatujawafanyia wajibu wao.

Kwa hivyo, tunawaombeni sana serikali jitahidini na hilo sana, kwa sababu kinachompa mgu nguvu na moyo ni lile jasho lake analojituma na akalipwa kwa wakati, tuwalipe kabla jasho lao halijakauka, maslahi ni kitu wajibu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, hilo nilikuwa nataka kulitilia mkazo sana, ili walinzi wetu hawa waweze kufarajika na matunda ya Mapinduzi yao.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa mkakati wa Halmashauri zetu za Pemba dhidi ya Afisa Mdhamini wao. Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Spika, kitendo hiki cha Afisa Mdhamini kujipangia matembezi kwenda Tanga kinyume na vikao vya Mabaraza ya Halmashauri, kwa kweli huku ni kuvunja katiba. Mhe. Waziri hili suala usije ukalifumbia macho, Halmashauri zimo katika mpangilio mzuri wa kuleta maendeleo katika wilaya zao, lakini sasa kuna watu wameshajifanya wao ndio wakubwa wa maamuzi ya mwisho, badala ya vikao kuwa ndio vyenye maamuzi, wakubwa sasa ndio wanaojitia maamuzi. Kwa kweli huku ni kuvunja mwenendo mzima wa halmashauri zetu.

Mimi nawapongeza sana halmashauri zote, lakini Halmashauri yangu ya Micheweni naipa hongera mara mia, kwa kusimamia vizuri ukusanyaji wa mapato na kujali mapato yanayopatikana ili kuweza yale ambayo yanastahiki wananchi wafikishiwe maendeleo yao na hilo wanajitahidi nalo. Zile halmashauri nyengine zote tunaziomba wafanye Micheweni ndio kiyoo chao ili waweze kufikia hatua ambayo wamefikia wenzao wa Halmashauri ya Micheweni. Lakini kusimama mtu akajiona yeye ndiye mwenye maamuzi, kwa kweli hili ni kosa kubwa katika madaraka mliopewa.

Kwa hivyo, nawaombeni sana Mhe. Waziri hili tatizo tuona kwamba umelisimamia na kulifanyia kazi. Naunga mkono hoja.

Mhe. Shadya Mohamed Suleiman: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kuwapongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwa kuvuka malengo. Vile vile Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii kuwaomba ndugu zangu wa Wilaya ya Chake Chake na wao wazidi kujitahidi, kwani mwaka huu wameweza kupata asilimia 98. Kwa hivyo, na wao nawaomba wazidi kuongeza jitihada.

Mhe. Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumuuliza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri ile nia ya serikali ya kuondosha msongamano wa wafanyabiashara wadogo na waendesha magari kwa kujengewa majengo ya kisasa eneo la Darajani yamefikia wapi, naomba Mhe. Waziri utakapokuja unieleze suala hili limefikia wapi, kwani naamini serikali inawapenda wananchi wake na inataka sana kuwaletea maendeleo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri utakapokuja unieleze suala hili limefikia wapi.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, naomba nigusie kidogo mradi wa mitaro. Hapa nataka nimpe tahadhari Mhe. Waziri, utakapoanza huu mradi Mhe. Waziri naomba uhakikishe umewapa wakandarasi wenye uwezo na waadilifu, kwani mradi uliopita Mhe. Waziri ulichakachuliwa na mradi ukakosa sifa na ukawa hauna ubora. Kwa hivyo, naomba mara hii wakandarasi watakaopewa wawe na ubora na sifa.

Mhe. Naibu Spika, nikimaliza hapo kwenye mtaro, nataka nizungumzie na mimi kuhusu vikosi. Mimi naunga mkono mawazo ya wajumbe wenzangu kuviangalia vikosi kwa jicho la huruma, katika suala zima la maslahi na suala zima la makaazi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, nyumba za askari wetu hawa kwa kweli haziridhishi, sio nzuri na hazina hadhi ya kukaa askari. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili serikali waliangalie kwa kina sana. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri kuhusu suala la posho zao za likizo. Pesa za likizo vikosi hawapatiwi na ilikubaliwa kwamba kila mwaka wapewe pesa zao za likizo. Likizo ni haki ya mfanyakazi Mhe.

Waziri, huu unafika mwaka wa tatu vikosi bado hawajapewa pesa zao za likizo. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri suala hili ulifanyie kazi kwa bidii kubwa sana.

Pia Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie kidogo kuhusu Kikosi cha Zimamoto. Mhe. Naibu Spika, kikosi hiki kwanza kimeonesha jitihada kubwa na kwa wepesi wake wa kufika katika majanga ya moto pale yanapotokea. Lakini kuna tatizo Mhe. Naibu Spika, kunapotokea majanga ya moto makubwa wanatumia maji na wanapomaliza maji basi kuna ugumu, kwa sababu inakuwa ni muda mrefu kurudi katika maeneo yao kuchukua maji.

Kwa hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri anieleze, ni lini yale maeneo yaliyotengwa kwa dharura, ya kupata maji kwa magari ya Zimamoto yatarudi kutoa huduma kama zamani. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja unieleze suala hili, yale maeneo ya kujaza maji kwenye magari haya yaliyotengwa kwa ajili ya kwenda kuzima moto.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mchango wangu utakuwa sio mkubwa sana. Nataka nimalizie kwenye vitambulisho. Mhe. Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Mkurugenzi wa Vitambulisho, kwa kazi nzuri aliyoifanya ambayo imeweza kuondoa malalamiko na kuondosha manung'uniko kwa muda mrefu, kwa kuweza kuwapatia vitambulisho kwa kila mwenye haki yake na mwenye sifa. Nampa pongezi sana Mkurungezi wa Vitambulisho.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia, ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Shadya Mohamed kwa mchango wako, sasa nafasi tunampa Mhe. Salma Mohammed Ali, baadaye Mhe. Mgeni Hassan Juma, anafuatia na Mhe. Omar Ali Shehe na muda ukibaki Mhe. Abdalla Mohammed Ali utamalizia. Tujali muda.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa jinsi alivyosoma hotuba yake kwa ufasaha mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza mchango wangu kwa kuanzia nyumbani Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Naibu Spika, mkoa huu naupongeza sana kwa mashirikiano makubwa waliyonayo wananchi pamoja na viongozi wao.

Mhe. Naibu Spika, sasa nataka niende kwenye mji wa Chake Chake kwenye soko la Chake Chake. Kwa kweli soko lile limezidiwa na huko nyuma kulikuwa na dhana ya kujenga stendi pamoja na soko jipya katika maeneo ya Michakaeni. Dhana ile wananchi wa Mkoa wa Kusini Pemba waliipokea kwa matumaini makubwa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atueleze tumefikia wapi, kwa sababu hali hairidhishi na ahadi ile ilitolewa hapa Barazani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atufahamishe pale stendi ilipo na soko lilipo kwa kweli Mhe. Naibu Spika, ni vurugu tupu, ingawa Mhe. Waziri aliwahamisha wafanyabiashara pale akawapeleka soko la Qatar, lakini kutokana na stendi ile ilivyo ndogo, hali bado ni mbaya na wala hairidhishi na imepelekea katika mji wa Chake Chake kuwa kila eneo lina stendi ya gari. Sasa namuomba Mhe. Waziri atufahamishe, hii ndio hali ya mji inavyotakiwa. Kwa sababu ukifika Benki ya Watu wa Zanzibar pale Chake Chake, ambapo benki ni pahala panapotakiwa pawe na utulivu, lakini pale pana stendi ya gari za Vitongoji, nyuma kidogo palipokuwa na jengo la hoteli ya utalii kabla hujafika, pana stendi ya gari za Gombani, lakini pale pale kushotoni kwake ambako ndiko Mhe. Saleh alipopigwa kumbo na mpaka leo mkono wake unamuuma, pana stendi ya gari za Mkoani.

Sasa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atufahamishe huo ndio utaratibu wa mji, wewe ukikaa pahala pamoja unaona stendi tatu, Vitongoji, Gombani na Mkoani. Mhe. Naibu Spika, atuambie Mhe. Waziri ikiwa haiwezekani pale Michakaeni, wametafuta eneo gani la kujenga stendi ya magari na soko.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo namuomba Mhe. Waziri kidogo anisaidie ni njia inayotokea Hospitali ya Chake Chake ikapita kwenye soko la Qatar na kupandishia Kibirinzi. Je, wizara yake pamoja na Mkoa wa Kusini Pemba, ina lengo gani kuwaondolea wananchi wa mji wa Chake Chake usumbufu katika eneo lile, kwa sababu ile njia ni mbovu sana na hasa katika eneo lile la soko na hapa namuomba Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndio waziri anayeshughulika na mji, hata kama ile barabara iko kwenye *UUB*, ana mawasiliano gani na *UUB* kwa sababu pale ikitengenezwa ndio ule mji utang'ara, halafu isitoshe na yale makusanyo yataendelea zaidi kukusanywa.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa pale sokoni Qatar ukienda una gamu siku za mvua. Kwanza kwa mashimo na matope ya ile barabara, halafu wewe una wasi wasi kutoka meza hii kwenda nyengine kama utafika salama hujaanguka kwa hali iliyoko pale. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atuambie wizara yake na huu mkoa wa Kusini Pemba ambao pia ni mkoa unaokusanya mapato mengi, je una msaada gani kwa wananchi katika barabara ile.

Mhe. Naibu Spika, sehemu nyengine ninayotaka kuzungumza ni kuhusu vikosi. Mhe. Naibu Spika, na mimi navipongeza sana vikosi kwa kazi kubwa na moyo wa kujitolea. Mhe. Naibu Spika, nasema moyo wa kujitolea kwa sababu tunajua kwamba maslahi wanayopewa vikosi hayatoshi, lakini bado wanaendelea na kazi yao ya ulinzi na wala hawarudi nyuma.

Vile vile naiomba serikali iwaangalie sana hawa vikosi, lakini pia katika vikosi hivi kuna kikosi kimoja ambacho nataka pia Mhe. Waziri anisaidie, ni kikosi hiki cha Zimamoto. Mhe. Naibu Spika, mimi nilipokuwa katika kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, tulifika katika eneo la Kituo cha Zimamoto kilichopo *Airport*, kwa kweli makazi yao hayakuwa mazuri na katika bajeti iliyopita nilisema. Lakini lililonisikitisha zaidi na ambalo mara ile sikulichangia ni zile nguo wanazovaa kwa ajili ya uokozi, sijui tuziite nini, lakini ilimradi ni zile sare zao wanazovaa, tulizikuta pale Mhe. Naibu Spika zimetundikwa na tukaulizia, wakatuambia hizi ni msaada sijui kutoka nchi gani, lakini lililoniuzunisha mimi ni ile nguo moja iliopo hiyo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, naomba mnadhimu wangu anisamehe, nataka kumtumia yeye, waunganishwe watu wawili ndio atavaa mtu huyo mmoja. Sasa nauliza kweli pale serikali iko makini, ikiwa wewe unataka kwenda kwenye uokozi nguo haikufai ni ya kushikilia unamkusudia yule atuokowe au akajiangamize na yeye. Mhe. Naibu Spika, hapa namuomba Mhe. Waziri anipe majibu mazuri.

Mhe. Naibu Spika, kweli mambo mengine ni msaada, lakini tuchukuwe msaada ule ambao unatufaa, tusichukuwe msaada wa kufyetuka kama hapa ni jaa au wazipeleke kwa fundi zile nguo zikatengenezwa.

Suala jengine Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu Zimamoto ambalo namuomba Mhe. Waziri anisaidie pia. Katika Baraza hili mara nyingi huwa linazungumzia kujengwa vituo vya Zimamoto kila wilaya. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili ni tatizo na sijui serikali imejipanga vipi. Kwa mfano hivi karibuni kulitokea moto Micheweni, hivi kweli Mhe. Naibu Spika, tutizame gari ya Zimamoto itoke Wilaya ya Chake Chake ikazime moto Micheweni, kwa kweli hiyo inakwenda kuzimamoto au inakwenda kushuhudia jivu.

Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali mambo mengi iyape vipaumbele. Kituo cha Zimamoto kuwepo Chake Chake kikaenda kuzima moto Micheweni au Mkoani, pengine sehemu za ndani, kwa kweli ni tatizo na hasa ukiyatizama magari yenyewe ni mabovu halafu litoke mwendo wote huo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hapo anisaidie.

Lakini pia kuna jambo moja ambalo naomba kidogo Mhe. Waziri anieke sawa ni hili suala la uajiri katika vikosi, Mhe. Naibu Spika, naona suala hili haliko wazi na hii ni jambo ambalo nataka ufafanuzi ni utaratibu gani unaotumika kufanya ajira katika vikosi vya SMZ, je hakuna ajira ya kujitolea ambayo vijana wanatumikishwa kama askari wa kujitolea kwa miaka mingi na baadae inapotokea ajira wakaajiriwa wengine wao wakaachwa, namuomba hapa Mhe. Waziri anipe maelezo kidogo nipate kujua na hili nalisema kwa sababu katika ziara hizo hizo za kamati tulikwenda kikosi cha JKU Msaani na tuliwakuta vijana hawa, na wakawa wana manung'uniko kwamba wanaajiriwa wapya wale waliopo pale waliojitoleya hawaajiriwi. Kwa hivyo namuomba Mhe, Waziri ni utaratibu gani unaotumiwa au wale waliowekwa pale wamewekwa kwa ajili gani wamekwenda kwa moyo safi tu kujitolea na wanahakikisha kwamba kujitolea kule ni kwamba watapata manufaa, lakini leo wanachukuliwa watu wengine wale wanaachwa pale pale.

Mhe. Naibu Spika, pale nyuma nilizungumzia mambo ya stand ya Chake na lini lakini sasa hapa leo nimeshapata mshtuko na kusikia kwamba eneo la Stand ya Wete pamoja na soko ameuziwa mtu, je Mhe. Waziri na pale pia panapo paki gari barabarani tuseme hichi ni kituo cha Kote, hiki cha wapi sijui ndio tulivyokusudia pengine Mhe. Waziri kaona ule mji wa Chake kwa kupanga gari vile barabarani umependeza sasa na lile eneo la kule wanaliuza ili na Wete wafanye kama vile. Mhe. Waziri nakuomba hapa ukinyanyuka utufahamishe kwa nini lile eneo likauzwa na ikiwa lishauzwa kuna sehemu gani ambayo itawekwa standi pamoja na soko. Na vile vile wale waliohamishwa pale kwa kupewa mtu ile nafasi wamewekwa wapi Mhe. Waziri naomba unisaidie na hapa.

Lakini kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika ukurasa wa 88 kiambatanisho namba 2 kwa kweli hapa nawapongeza sana wafanyakazi wa baraza la Mji la Chake Chake, Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake, Baraza la Mji la Mkoani na Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani kwa kuvuka kiwango katika makusanyo kwa kweli nawapongeza sana, lakini lililonishutua ni kiambatanisho ukurasa wa 89 matumizi ya Serikali za Mitaa kule wamekusanya wamevuka lengo lakini na matumizi pia wamevuka lengo. Sasa Mhe. Waziri hapa nataka nifahamishwe hivyo kweli mie katika nyumba yangu najipangia kuzalisha elfu 15 kwa siku na matumizi yangu ni elfu 10 kwa kuwa nimezalisha elfu 25 ndio matumizi yazidi zaidi. Mimi kwa kweli hapa sifahamu mimi niolivyokuwa nikidhani kile kilichokusanywa labda ingelikuwa akiba kwa shughuli za maendeleo ya wananchi lakini kwa kuwa tumekusanya kingi tutumie kingi na hayo matumizi sijui vipi.

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika (Makofi)

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa usahihi na mimi ya kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na na Idara maalum za SMZ, wawali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu subhanahu wataala aliyetujaalia hapa tukija tukiwa wazima kabisa wa afya na kuweza kutekeleza majukumu yetu tuliyopangiwa.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake kwa kweli kwanza kwa utayarishaji wa hutuba ambayo ametuletea hapa mbele yetu lakini vile vile kwa kazi zao ambazo wamekuwa wakizifanya katika hotuba ya mwaka 20013/2014 samahani Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitakuwa na mengi sana ya kusema kwa sababu mengi yamezungumzwa lakini kubwa ninalotaka kulisema ambalo nimelichukua kwa wenzangu wengi sasa kwa sababu na mimi ni hilo hilo ninalotaka kulizungumza ni kuhusiana na mipango ya utekelezaji wa katika maeneo mbali mbali ya Manispaa zetu, pamoja na Halmashauri zetu. Mhe. Naibu Spika, napata wasi wasi kwamba kuna tatizo linalojitokeza hasa katika mipango ambayo tunaipanga, kwa sababu utekelezaji wake mara nyingi sana unakuwa ni mbovu, na mabadiliko ambayo tunahitaji kuyaona kwa kweli ni madogo sana na hili linasababishwa na usimamizi mzuri.

Mhe. Naibu Spika, ukitizama katika kupanga tunapanga mambo mengi ambayo ni mazuri lakini ukiangalia na ukienda ndani kabisa utaona kwamba kila mmoja anafanya anavyotaka na hili ni kosa kubwa, na mimi najiuliza hivi yoyote yule ambaye anayekuja anafanya lake Mhe. Marina alizungumzia hapa wawakilishi na wabunge wakija waendelee na miradi ile, lakini sio wawakilishi tu na wabunge, wakurugenzi hata Mawaziri wenyewe kila mmoja ana lake ambalo analisimamia zaidi kuliko jengine wakati mipango ile tunakuwa nayo tayari, nafikiri hilo ni kosa linalofanyika na ndio maana mara nyingi sana tunakuwa tunashindwa kutekeleza mambo yale ambayo tunayapanga.

Mhe. Naibu Spika, nazungumzia suala zima la mzadi wetu wa ZUSP mradi huu ulituletea matumaini makubwa sana, mradi huu ulipigiwa debe sana na Serikali hii yetu lakini kwa bahati mbaya sana mradi huu haukutekelezeka vizuri, tuliambiwa hapa mradi huu utashughulikia taa za barabarani, mradi huu utashughulikia michirizi, mradi huu utashughulikia mitaro ambayo tunayo katika miji yetu. Lakini kwa bahati mbaya sana kazi iliyofanywa ni ndogo mno. Sasa mimi namuuliza Mhe. Waziri, tatizo limejitokeza wapi katika mradi huu ambao sote tumeupigia debe Serikali pamoja na sisi Wawakilishi tukuwapa matumaini wananchi wetu kwamba mradi huu utaleta mabadiliko makubwa katika mji wetu hili tatizo liko wapi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza sana Wizara kwa kununua vifaa vingi vya usafishaji lakini vifaa vingi hususan magari na vifaa ambavyo vinatumika kwa usafishaji, lakibi bado mji wetu mchafu, miji yetu michafu, nasema hilo kwa sababu mimi nakaa mjini maeneo ambayo kila siku unatembea ni machafu sasa hivi vifaa ambavyo tulitegemea kwamba vimenunuliwa na vimeletwa vifaa vinafanya nini.

Mhe. Waziri nenda Michenzaji ukaona hali ya Michenzani ukipita kwa mifuu inabidi ukanyage taka ambazo zimekusanywa ukipita kwa gari inabidi gari yako ipite kwenye taka taka hii ni aibu, mimi ningewaomba sana Manispaa hebu wapite hao watu wetu ambao ni wasimamizi katika meneo yao waone hali ni mbaya mbaya sana uchafu ni mwingi, ikiwa kwenye jaduweli lako inaonyesha kuna gari zimenunuliwa pamoja na vikapu vya kutilia takataka na mambo mengine lakini kazi hii haifanyiki kwa nini hilo mimi nafikiria ni kero.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kwamba ningemuomba habu tufanye kama wenzetu wa Ruwanda ambao waliamua kuna siku maalum kila mwezi wananchi wote pamoja na Rais wao wanatoka kwenda kusafisha mji wao, kwa sababu

Mheshimiwa elimu ambayo inatolewa kwa wananchi kuhusiana na masuala ya usafi haijawafika, haiwezekani kama imewafika leo tukaona bado tunaishi katika mazingira machafu, sisi wenyewe tukitoka hapa leo mwezi mmoja tu tukienda katika nchi ambayo ina utaratibu mzuri wa kusafisha mji wao ukirudi unaona tabu hata kuchukua ile karatasi ukaitupa, kwa sababu imeshakuingia ndani ya system yako kwamba usafi ni wewe mwenyewe unaanza kwako. Sasa tunaambiwa kwamba elimu inatolewa hii elimu inamfikia nani, ambayo inatolewa inayohusiana na usafi lakini ushirikishwaji wa wananchi bado ni mdogo mno wananchi wanahitaji kushirikishwa, kuna vikundi vya vijana.

Mimi nakumbuka vizuri sana wakati wa kujitolea wakati ule wengine watakuwa hawajui mimi bado nakumbuka, sote sote mpaka Rais anatoka kuja kujitolea hakuna mkubwa hakuna mdogo, kwa sababu sisi ndio tunaoishi katika mazingira yale sio tu wafanyakazi wa Manispaa tunawaonea tunawasema sana wafanyakazi wa Manispaa tunawaonea. Wao wana fungu lao katika usafishaji lakini na sisi wananchi tuna fungu letu tusitegemee kwamba kila siku Manispaa kila kitu watakifanya wao.
Mhe. Waziri nakuomba sana ushirikishwaji wetu pamoja na Wizara yako ndiyo italeta mazingira mazuri na safi katika nchi yetu, bila ya hilo haiwezekani.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana katika kipindi hichi na kwa kuwa inaonyesha dalili kwamba vifaa vipo basi katika maeneo ya mji wetu Mjini pasafishwe ile mirundiko ya taka taka zilizokaa sasa zimefanya kama nini iondoshwe, hebu tuangalie kwa kipindi cha mwezi mmoja tu tutizame kama tunasema kwamba sasa tunakwenda kuusafisha mji wa Zanzibar na tuone sisi nafsi zetu zitakavyofurahi kuishi katika mazingira mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo moja kwa moja nakwenda kwenye Idara Maalum za SMZ, Mhe. Naibu Spika, wengi wamesema mimi nilikuwa kwenye kamati ya Kusimamia viongozi wakuu hali ya vikosi vyetu naijua, kwa kweli hali ni mbya kwanza vile vivutio vya wao kuwafanya waweze kufanya kazi vizuri havipo vitendeya kazi hamna, Zimamoto wapo tu kwa sababu ni jina Zimamoto lakini utakwenda kwenye seksheni ya Zimamoto hakuna kisima cha maji au maji hamna au maji hayatoshi kuna matatizo, Mhe. Waziri kwa kweli kuna matatizo kwenye Zimamoto lakini vifaa hamna wanahitaji nguo za kazi hawana, sijui kama mpaka sasa hivi tayari vimeshapatikana lakini hamna tumekwenda Pemba sisi tumeona. Maeneo mengine ya kuwekea vifaa vyao yanavuja.

Ukienda kwenye KMKM hali kadhalika KMKM wenzangu wamesema wanafanya kazi nzito wanafanya kazi nzuri sana nawapongeza sana kwa kweli wanafanya kazi nzuri lakini pia vifaa hamna, lakini vikosi hivi vina uwezo mwengine uwezo wa kujenga uchumi, tuna kikosi cha kujenda uchumi tumekwenda kuangalia wana uwezo wana skills nyingi sana wanachonga fanicha ambazo hata wenzetu wa Tanzania Bara wanazichukua, lakini leo hawana vifaa vya kuchongea na kutumia vifaa hamna tuliiomba Serikali wawapatie vifaa hapa ndio pa kutia nguvu kwa bahati nzuri sana hawa wanajeshi wetu kwa sababu wana moyo wa kufanya kazi kwa nidhamu wanafanya vitu vizuri. Lakini sasa matokeo yake Serikali haivest humu ndio sehemu za kunvest na tukajenga uchumi. Mhe. Waziri mimi ningeomba sana bado naiombea Idara yako ya Vikosi maalum kwa kweli kuingalia na kuhakikisha kwamba wanapata vifaa ambavyo vitaweza kusaidia katika shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na hayo tu ya kusema sio mengi sana lakini jengine ambalo nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri ni kile kituo chetu ambacho kimeondosha Darajani na kweli tumefurahika kwa sababu pale ilikuwa ni kero, lakini Mhe. Abdi Mosi alizungumza mnapoondoa watu pahala muwatayarishie sehemu nyengine ambayo ni bora, sijui wale wafanyabiashara kwa sababu watu wameondoka kuna baadhi ya wafanya biashara pale wameondoka hawana pa kwenda, lakini sasa hivi kuna gari zinapaki pale jengine gari ndio hizo hizo zinafanya biashara pale pale, sasa wameondoshwa wale wenye miguu maskini ya mungu wamekaa wengine ambao wana gari zao Mheshimiwa hili litazame wapo wafanya biashara wanakaa pale pale wanafanya biashara zao wakiwepo pale pale, wengine wameondoshwa maskoni.

Lakini jengine Mhe. Waziri, ambalo linanikera sana kile kituo pale kilipowekwa sasa hivi sipo pale Mheshimiwa sipo pale, kwa sababu kama ulisema kwamba ulisema juzi lilielekezwa ukasema lipo mbele pale hapakai pale kwenye jumba namba nane hawakai pale na polisi wapo, polisi wapo kwa nini polisi hawawaelekezi kwenda kukaa wanawaachia wanakaa chini pale, kuna watoto wetu pale wanapita wanakwenda Skuli ya Kisiwandui na ni walemavu zimeshatokea ajali pale kwa nini hawasogei mbele wanaachiwa hilo ndio tatizo, haiwezekani pahala popote hakuna nchi inayokwenda bila ya utaratibu jamani na sheria lazima zifuatwe, pale wanapokaa tumeshasema kwamba sipo kwa nini wanaachiwa na polisi wanakwenda pale na wanawaachia inasikitisha. Mhe. Waziri

waondoshwe pate kama hawawezi kufuata amri ya Wizara pale aondoke pakini wanapokwenda kukaa wanakaa kwa kweli wanasababisha ajali.

Na polisi wetu kitu kinachoshangaza wanaaachia nasema inasikitisha kwa sababu walimu wameshatulalamikia wameilalamikia kamati yetu ya ustawi wa jamii, wanasema pale ni hatari kwa watoto kwa wanafunzi hasa kwa vile pale kuna skuli ya walemavu, Lakini Mheshimiwa mimi najuiliza pale mbele Mnazi MMoja pana nafasi ya kutosha hivi tuna tatizo gani, ule Mnazi Mmoja kuna nusu inaweza kutumika kwa mipira kuna sehemu ambayo Serikali inaweza kupatengeneza pale ikawa kituo cha dala dala kuna tatizo gani, mimi naogopa sana Mheshimiwa, naogopa kwa sababu kuna watoto wetu wengi wapo tayari na tayari zimeshatokea ajali pale. Mhe. Waziri lishughulikie hilo aidha wajue pahala pa kwenda au waondoke kabisa pale.

Mheshimiwa baada ya hapo ninafikiri sina zaidi la kusema kwa sababu wenzangu wengi wameshasema na wamechangia yale ambayo mimi nilikuwa ninafikiria kuyachangia, mimi niseme tu kwamba naunga mkono hotuba yako kwa asilimia mia moja, lakini ningeomba sana kwamba haya ambayo nimekuomba uyatekeleze ili sasa tuone ufanisi wako pamoja na watendaji wako.

Ninakushuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa usimamizi wa Wizara na kwa namna alivyowasilisha hotuba yake hii. Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza bajeti hii ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum, tutakuwa tunajikita katika maeneo mawili kwa matatu ambayo kwanza itakuwa tunaangalia bajeti katika Tawala za Mikoa, Pili tutaangalia Idara zetu maalum bajeti zake na la tatu tutaangalia ile ya Idara ya Vitambulisho.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na upande wa Tawala za Mikoa. Mhe. Naibu Spika, hii Tawala za Mikoa ni nadharia ya kupeleka madaraka mikoani ambayo ilianzishwa kati ya miaka ya 1970. Na maana yake hasa ilikuwa nini? Maana yake ilikuwa ni kutofautisha majukumu baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Na hili lilikuwa na lengo la kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maendeleo ya haraka na maendeleo endelevu kupitia serikali zao za mitaa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa upande wetu Zanzibar licha ya kwamba nadharia hii ilikuwepo muda mrefu kama nilivyosema miaka ya 1970 lakini bahati mbaya sana kwa upande wa Zanzibar tumefeli. Wenzetu wa Bara kwa kweli wao wameweza kupiga hatua kubwa na ushahidi sasa hivi uko wazi, Zanzibar bado tuna tatizo sana katika utekelezaji wa hili na Mhe. Naibu Spika, viongozi wetu wengi wa serikali wanakweda ziara mara mara duniani. Na sehemu zote wanapokwenda, eneo moja wanalokwenda kujifunza ni maendeleo yatokanayo na hizi serikali za mitaa katika nchi hizo. Hata Marekani eneo hili liko, Uingereza eneo hili liko Uchina liko kwahala kote utazikuta Serikali za Mitaa ambazo zinafanya kazi vizuri sana katika kuleta maendeleo ya wananchi na maendeleo ya miji yao.

Ni kitu cha kusikitisha kama nilivyosema Zanzibar tumekuwa na ugonjwa katika hili, ni kitu cha aibu kwamba tangu mimi nilipoingia katika Baraza hili mwaka 2005 Mhe. Naibu Spika, serikali imekuwa ikizungumzia juu ya sera, sera za marekebisho, maboresho ya serikali za mitaa. Tangu 2005 nasikia neno hili na matarajio yangu mimi ilikuwa nilidhani kwamba itakapoingia awamu hii basi kitu cha kwanza ambacho kitafanyiwa kazi ni suala zima la sera zihusianazo na maboresho ya Serikali za Mitaa. Lakini leo serikali hii ya awamu ya saba keshokuta inamaliza muda wake bado inaendelea kutupa hadithi. Mimi ninasema serikali katika hili hamjawa makini katika kufikiria maendeleo ya wananchi. Na kwa fikra yangu tatizo hasa nini?

Mimi nadhani tatizo kubwa linalokwamisha kwanza siasa kwa sababu eneo hili moja kwa moja linaambatana na siasa. Kwa hivyo siasa kwa fikra yangu inakuwa ni kikwako lakini kikwazo cha pili ambacho kinatukwaza inaikwaza serikali ni tatizo zima la vyanzo vya mapato. Kwa sababu kadiri utakavyoweza kuwa na maboresho ya Serikali za Mitaa ndipo pale ambapo utatakiwa utenge vyanzo mahsudi katika kuziendesha serikali za mitaa kitu ambacho serikali yetu kwa upande wake hilo ni tatizo. Kwa sababu tunakumbuka miaka ya nyuma vile vyanzo vilivyokuwa vikitegemewa na Serikali zetu za Mitaa katika miaka ya karibuni hapa vyote vimechukuliwa takriban asilimia kubwa vimechukuliwa na kuja kwenye Serikali Kuu. Tukichukua mfano kama *road license* yote hayo yalikuwa ni kwenye Serikali za Mitaa na yote yamechukuliwa sasa hivi ni tegemeo la mapato ya Serikali Kuu, hili ni tatizo.

Sasa Mwenyekiti, mimi nadhani Waziri juzi alisema kwamba tunaleta sheria tatizo letu si sheria. Kwa sababu sheria katika Srikali za Mitaa hivi sasa tunazo na zimeeleza. Tatizo letu ni kuwa na sera, sera ndio itakayotoa *definition* ya mamlaka na majukumu katika ngazi moja na nyengine. Mhe. Naibu Spika, mathalan sasa hivi ukitathmini utaziona hizi Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Ofisi za Wakuu wa Mikoa kazi yao nini? Kwa sababu umuhimu wa kuwepo lazima ziwepo lakini kazi yake ni nini? Katika serikali unakutia kuna *dublication* ya kazi utaikuta Wizara kazi yake ni hii jambo hilo linafanywa na Wizara na jambo linatakiwa lisimamiwe na Ofisi ya Wilaya. Katika nukta hii Mhe. Naibu Spika, nataka nitoe nukta moja na hii naomba serikali waizingatie.

Serikali inapata hasara kubwa, serikali inaingia gharama kubwa katika miradi ambayo haku uratibu katika suala zima la miradi katika mawilaya yetu. Mathalan sasa utakapokwenda Wilayani kila mmoja mambo ni shaghala baghala tu, utakuta mtu leo Wizara inajenga njia, kesho Idara ya Maji inakuja inakata njia inapitisha bomba. Keshokutwa mtu wa *cable* atakuja na yeye atakata pake atapitisha cable. Keshokuwa mtu wa wa umeme nay eye atakuja kuvunja, sasa mambo kwakweli ni shagahla baghala mambo hayaeleweki.

Sasa wazo ambalo ninalolitoa katika nukta hii, naomba serikalihaa katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa ama katika Ofisi za Wilaya pamoja na marekebisho atakayoyaleta lakini wajaribu kuangalia suala zima la kuwa na uratibu wa miradi ya wananchi hasa inayokwenda huko mawililayani ili kuepuka mambo kama hayo. Sasa hivi kila mmoja anajifanyia vyake tu hakuna usimamizi mzuri katika masuala haya.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwenye suala hilo sasa naomba niingie katika Halmashauri Manispaa pamoja na mabaraza ya Miji. Mheshimiwa kama nilivyosema mwanzo kwamba hizi Halmashauri zetu Manispaa pamoja na mabaraza ya miji huku ndiko ambapo tulikukuwa tunategemea maendeleo ya miji wetu pamoja na maendeleo ya wananchi. Na hilo lingewezekana iwapo tu watakuwa na uwezo mzuri wa kukusanya kodi ni bahati mbaya kwa kosa lile lile narudia tena kwa kosa lile la kutokuwa na sera limepelekea kwa kweli hata hizo Serikali zenyewe za Mitaa kwa maana ya Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Miji, Serikali Kuu kuziingilia kitu ambacho Serikali Kuu zilikuwa hazitakiwi ziingilie taasisi hizo.

Leo Madiwani wetu wamekuwa kwa kweli hawana mamlaka yoyote. Na kwa mujibu wa sheria madiwani ndio wenye vyombo hivi. Utakuta Katibu ambaye kateuliwa na Waziri kila kitu anafanya yeye mwenyewe, mifano mingi tayari ishatolewa hapa. Kwa hivyo Mhe. Spika, hili ni tatizo moja ambalo tunashindwa kuzipa mamlaka Serikali za Mitaa na kushindwa huko maana yake tunashindwa kwenye kukusanya na wanaposhindwa kukusanya matokeo yake ni kutoa huduma mbovu na huduma zisizoridhisha kwa wananchi ambao wamezichagua serikali zetu hizi.

Mhe. Naibu Spika, pametolea pongezi hapa kwa makusanyo yaliyopindukia. Lakini mimi nataka nitoe elimu moja, tusizipongeze Halmashauri zetu hizi kwa kuvuka lengo sio kweli nisikilizeni mimi. Maana mtu hawi ana uwezo wa kukusanya hamsini lakini akajikadiria kukusanya arubaini ili akikusanya arubaini tano aendelee kusifiwa sio kweli hiyo siyo sahihi. Na hili si tatizo la Halmashauri na mabaraza ya miji hili ni tatizo la serikali nzima, tuna tatizo la *projection* ya mapato katika serikali. Na tunafanya hivyo kwa sababu serikali hakuna *policy* maalum ya kukisia mapato na katika hili ni muhimu sana Mhe. Naibu Spika, *projection* yetu kwa serikali hata serikali kuu msingi wake ni kuangalia mapato yanayotokana na bajeti iliyopita sio sahihi. Huwezi ukasema kwamba mwaka jana tulikusanya mia mbili kwa hiyo mwaka huu tukisie tutakusanya 202 kwa sababu mwaka jana tulikusanya 200 hiyo siyo *realistic* mambo hayatakiwi serikali iendeshwe kwa mambo ya kubahatika uganga wa kienyeji.

Kitu pekee ambacho kinatakiwa kiwe base *line* katika ku-*project* mapato ni suala zima kwanza ukuaji wa vyanzo vya mapato huo ndio msingi mkubwa kwanza unaotumiliwa. Lakini jambo jengine ambalo ndio msingi linalotumika ni kuangalia *market value* katika vyanzo hivyo vya mapato. Leo sisi hatuangalii *market value* ya kila mwaka tunachoangalia ni *book value* tu kitu ambacho sio sahihi ndio ukakuta mapato mengi tunayokusanya Mheshimiwa msingi wake ni wa kuyapigia ramli katika uganga wa kienyeji.

Kwa hivyo msisitizo katika hili Mhe. Naibu Spika, tunaomba tujirekebisho, serikali kuu yenyewe ijirekebishe kwa maana ya Wizara ya Fedha lakini vile vile sasa tupewe msukumo kwa watendaji wetu katika Halmashauri ili makisio yao ya mapato yawe ni *realistic* sio iwe ni mambo ya kubabaisha baisha ili hapa wakija wakitwambia kwamba ni zaidi ya asilimia moja ili wapate kupigiwa kofi, lazima watupe kitu ambacho kwa kweli ni chenye uhalisia.

Naomba niipongeze serikali kwa kuanza kupeleka wahasibu ambao wana viwango katika Halmashauri zetu, mtu apewe sifa yake. Serikali wameliona hili, wamelianza hili na katika hilo naomba niwapongeze lakini nawaomba niwashauri tena, kwa sababu kwenye Halmashauri na kwenye mabaraza ya miji huko ndiko kwenye kodi za wananchi ndogo ndogo basi kadiri wanavyokusanya na matumizi yao yawe ni sahihi. Na hayawezi kuwa ni sahihi kama hakuna wakaguzi wa ndani Mhe. Naibu Spika.

Moja katika ya kosa ambalo bado linaendelea licha ya kuwapeleka wahasibu ambao wana sifa Halmashuri zetu na mabaraza ya miji kwa kweli zinakosa *internal auditor. Internal auditor* anayetumikani wa Wizara. Naomba nikushauri Mhe. Waziri alau Pemba katika taasisi hizi uweke mmoja kule ashughulikie maalum katika eneo hili na hapa Unguja awepo mmoja ashughulikie katika eneo hili. Mhe. Waziri wa Fedha tulimwambia na hili changamoto hasa kwa mabaraza maana yake unasikia kwamba Baraza la Manispaa wanahitaji kuongezewa *subvention* hilo halikubaliki.

Tunasema kwamba *management* yoyote itakayoshindwa kuwa na makusanyo ya uhakika kwa sababu sasa tunakoelekea ni kuhakikisha kila mwaka serikali inapunguza ruzuku kwa mabaraza. Kwa hivyo haiwezekani kufeli kwako wewe uitie serikali gharama, ikiwa wewe umeshindwa kukusanya kodi zaidi usitegemee kwamba serikali itakupa kodi sisi hatutoweza kulikubali hilo. Kwa hivyo kila manager katika management yake katika Halmashauri ama manispaa ahakikishe kwamba anakusanya kwa wingi ili kila mwaka serikali iendelee taratibu kupunguza ruzuku katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niondoke hapa kwenye Halmashauri kwa kuja katika mji wa Chake Chake na Mhe. Waziri naomba utakapokuja unambie nini hatma ya njia ya Msingini. Msingini ina Shehia mbili, Shehia ya Msingini na shehia ya Chachani lakini barabara yake kwa kweli sasa hivi haipitiki hata ukiwa na punda wachilia mbali gari. Sasa kwa sababu ile njia yenyewe ni Baraza la Mji, naomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja nieleze ni nini hatma ya njia ya Msingini ambapo Mwakilishi naye anatakuwa tayari kusaidiana na Baraza la Mji tuone walau tunafanya huduma ya mwanzo katika kuifanya ile njia ipitike.

Jengine ilikuwa ninaulizia suala zima la barabara ile ya ingawa tushazungumza na Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rai njia ile ye Muembe karata na Mguye jukumu hili liko kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ninaamini kwamba atalishughulika vyema.

Mhe. Naibu Spika, jengine sasa naomba niingie eneo la Vikosi vya SMZ. Ni kweli kwamba kipindi cha nyuma sisi kwa upande wetu tulikuwa tukivisema sana vibaya vikosi vya SMZ na hatuna maana kwamba leo kuvisifu basi kwamba viendeleze sifa yake ile ambayo tulikuwa tukiilalamikia hatuna maana hiyo. Tuna maana kwamba tunavisifu kwa sababu, sisi ambao tunaamini Zanzibar kuwa na mamlaka kamili, hatuwezi kusema kwamba Zanzibar yenye mamlaka kamili kama hatuna vikosi vyetu wenyewe hiyo ndio nadharia yetu na huo ndio msingi waheshimiwa uliotupasa sasa tuvitetee kwa nguvu zote vikosi vyetu hivi, kwa sababu hii ndio hazina yetu na hii ndio jeuri yetu kama Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, huo ndio msingi uliopelekea leo kusimama hapa na kuvitakia vikosi hivi maslahi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli vyombo vyetu hivi viko katika hali mbaya sana, na kwa maana hiyo tutakuwa sasa mara kwa mara tukiibana serikali kuhakikisha vikosi hivi vinapatiwa maslahi, askari hawa ambao ndio tegemeo letu wanapatiwa maslahi mazuri, mishahara yao inaboreshwa, wanapatiwa mafunzo pamoja na makaazi. Maana yake makaazi ya askari yetu ni stahili yao. Kawaida ya askari, askari hakai mitaani askari hukaa kambini. Kwa hivyo na hili ni eneo ambalo tunahitaji serikali ianze kulifikiria. Lakini hii tabia ya kuajiri kila mwaka tusivifanye vikosi hivi kuwa ni kimbilio la ajira zetu katika serikali haipendezi.

Majeshi ya sasa duniani kote serikali zote zinajitahidi ku-*minimize* idadi ya askari, askari wawe wachache waliofunzwa vizuri, wanaolipa maslahi mazuri lakini haina maana kwamba kila mtu anayetaka ajira akimbilie kwenye vikosi haina maana. Tutakuwa na askari waliokuwa kwa kweli hawakufunzw vyema, waliokuwa wana njaa, waliokuwa hawashibi na hilo sio lengo. Tunahitaji tuwe na askari wachache, askari wakakamavu, askari walioshiba, askari wenye *uniform* na askari wenye makaazi bora. Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio sera ambayo inaweza kuvifanya vikosi hivi Mhe. Naibu Spika, viwe ni vikosi vya kisasa vikosi vyenye jeuri ya kuilinda nchi yao.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa niingie kwenye Idara ya Vitambulisho. Katika idara hii pamoja pamoja na makosa mengi, matatizo mengi Mhe. Naibu Spika, nataka nilalamike kwamba Idara ya Vitambulisho ina matatizo

Mhe. Naibu Spika: Bado dakiaka tano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Haya na tatizo kubwa lilioko kule ni udhibiti, mimi binafsi nilikwenda kubadilisha *ZID* yangu katika Ofisi iliyoko Chake Chake pale lakini jambo la kunisikitisha juzi alinijia Mhe. Haji Faki Shaali MBM na kile kitambulisho ambacho nilikwenda kukikabidhi kwenye Ofisi ya Vitambulisho inakuwaje? Na yeye kapewa na mtu ambaye kakiokota sasa inakuwaje, tujenge imani gani kuna kitu gani. Mimi binafsi maana yake sisemi nani wala nani mimi binafsi nilikwenda kukipeleka kitambulisho changu kule, leo kitambulisho changu kinaokotwa okotwa tu mitaani, Mhe. Haji Faki Shaali kaja kunipa mimi kitambulisho changu sasa inakuwaje? Kunakuwa na utaratibu gani wa kuvitunza vitambulisho hili? Hili linatupa wasiwasi, lakini bado tunarejea tena Mhe. Naibu Spika, kwamba tunapozungumzia uchaguzi tunazungumzia na suala la upatikanaji wa vitambulisho.

Bado hoja yangu ni ile ile kwamba serikali ina wajibu wa kubadilisha sheria ya upatikanaji wa ZID ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi ambao wana haki ya kuipata haki yao hii. Lakini vile vile waheshimiwa tusichukulie na jazba kuwapa vitambulisho watu ambao hawahusiki. Leo kosa hili hatuwezi tukaliona lakini baada ya miaka 20 inayokuja Mhe. Spika, tatizo hili linaweza likaja likatugeukia wenyewe na likatudhuru wenyewe Mhe. Naibu Spika. Kumpa mtu haki ambayo si yake na baya zaidi mtu mgeni pengine hata si mtanzania, maana yake ni afadhali umpe mtanzania kulikoni kumpa mtu ambaye ni Mburundi au Mmalawi au mtu mwengine hili ni tatizo. Baadae tutakuja ndani ya ardhi yetu hii hata sisi wazaliwa tutakuwa hatuna haki.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho niseme katika nukta hii wananchi wanaendelea hata wale ambao tayari wamesha-*qualify* kupata hizo vitambulisho vyao bado wanapokwenda kule kwenye ofisi wanapata tatizo hilo.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mkoa wa Mjini karibuni iliratibu zoezi la ufungwaji wa CCTV Camera katika eneo la Mji Mkongwe na kuna kampuni hapa ambayo ni ya kizalendo *Zest Group* waliuchukua hata uongozi wa Mkoa Mjini Magharibi, Jeshi la Polisi na kwenda kuwakaguza kazi zao kama kule Dubai pamoja na Nairobi. Bahati mbaya sana katika kutoa kandarasi ile Serikali hawakuwazingatia hawa wazalendo ambao wana uwezo mkubwa. Hata wakubwa wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Jeshi la Polisi kuchukuliwa nje ya nchi kwenda kuoneshwa aina ya kazi lakini baya zaidi serikali iliwapa Kampuni ya Romania.

Sasa Mhe. Waziri atakapokuja naomba aje anieleze ni sababu gani zilizopelekea kuwanyima kandarasi hii wazalendo ambao ndio wangelitoa ajira kwa watu wetu na kwenda kuwapa Waromania. Au kama hilo halitoshi basi kama ikiwa haikuwezekana kuwapa hao wakandarasi basi kwa nini wasingelifanya japo kuwa ni *consultant* ili wananchi wetu wa ndani wakanufaika. Ni sababu gani naomba Mhe. Naibu Spika, atakapokuja Mhe. Waziri aweze kunijibu hilo, na naomba niunge mkono baada ya Mhe. Waziri atakaponijibu majibu maridhawa ambayo yatawafurahisha wananchi wangu wa Jimbo la Chakechake. Nashukuru.

Mhe. Abdallah Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa vile leo pengine niwe mchangiaji wa mwisho, mengi yameshasemwa sijui kama yangu mimi yatakuwa mapya mapya au yatakuwa yanatia kalafati tu tena.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kuniona na kunipa fursa ya kuchangia wizara ambayo kwa maoni yangu ina umuhimu wa pekee katika nchi hii, tofauti na wizara nyengine. Mhe. Salmini juzi alisema ni kioo na kioo mara nyingi huwa tunatakiwa tukitunze kwa sababu kupasuka kwake kunakuwa ni mara moja zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na Seriakali za Mitaa na kwa ujumla hotuba hii imetuonesha kwamba tunatarajia kufanya maboresho mengi katika idara hii. Mimi napenda niseme kwamba moja katika maboresho hayo basi yangewaangalia wale madiwani kulikoni kuja na sera tu hapa ambazo watu wale hazitowaangalia. Na katika hili Mhe. Naibu Spika, ningelithubutu kusema kwamba nafikiri sasa serikali ina wajibu wa kukaa kitako kuangalia upya hivyo katika uchaguzi unaofuata wa mwaka 2015 tukijaaliwa kuna haja ya madiwani kuwaingiza katika uchaguzi tukachagua madiwani?

Nafikiri Mhe. Naibu Spika, kama tutawaita wataalamu wa kisiasa na wa uchumi basi hawa kwa maoni yangu wangelikuwa hawapo, hatuna haja ya kuingiza fedha kwa ajili ya uchaguzi wa madiwani. Kwani nahisi mimi kwamba hata hiyo serikali hivi sasa watu hawa imeshaanza kuwadharau na inaendelea kuwadharau, haiwi kwamba sisi tunachukua juhudi za kuwaweka watu hawa katika Katiba kwamba tuwachague lakini leo inapofika wakati wa kufanya kazi wao hatuwatambui, hatujawawekea hata posho lolote la kwamba na wao ni watendaji katika serikali

hii. Kwa hiyo, mimi nahisi Mhe. Naibu Spika tungeondoa zile katika bajeti ya uchaguzi ya kwamba watu hawa nao tutawachagua iwe haipo angalau serikali pengine ingepata fungu la kuongeza katika ununuzi wa *city scan* na mambo mengineyo muhimu hospitali, lakini madiwani wakaondoshwa katika uchaguzi mkuu kwa sababu kazi yao mimi siioni imetawaliwa zaidi na masheha katika maeneo yetu.

Lakini juu ya hayo tumeoneshwa kwamba Serikali za Mitaa zina jukumu la kukusanya mapato, mimi nahisi bado wanayo fursa kubwa sana mapato haya wanaweza wakayaongeza mara mbili kunahitajika uadilifu mkubwa na uelewa, na naamini katika bajeti ya mwaka jana tuliambiwa kwamba kuna vijana hasa wahasibu na watunza fedha wamepelekwa katika idara hizi. Wangetumia utaalamu wao wa kuhakikisha kwamba fedha inaongezeka katika idara hizi.

Mhe. Naibu Spika, wengi hapa wamezungumza kuhusu Manispaa, mimi kidogo nilibahatika Mhe. Naibu Spika kutembea tembea nchi nyingi huko na nimeona mengi kwa sababu tuliambiwa kila tukitembea tutajifunza mengi. Sasa mimi nimuulize Mhe. Waziri tu mwaka jana na mwaka juzi 2012/2013 watendaji wengi wa serikali walipatiwa fursa za kwenda kujifunza na ma-*comrade* wenzetu wa China walitusaidia kutupatia fursa za kuwapeleka watendaji wetu wakuu kwenda China kuona ili wakija hapa watekeleze yale waliyoyapata kule wayatekeleze katika nchi yetu. Sasa sijui huyu mkurugenzi najua yeye ni mpya yeye kaipata fursa hii au hajaipata? Kama Mhe. Waziri Mkurugenzi wetu mpya huyu hajaipata fursa basi nakuomba umpatie aende nae akajifunze kwa sababu hivi sasa sijui tunaishi katika mji gani.

Mimi sitambui tunapanga vipi Mhe. Naibu Spika, wauza magari wako katikati ya miji, wauza magari wapo chini ya kwapa za mama ntilie, madaladala hatujui kituo kiko wapi. Hivi sasa Zanzibar tumebahatika sijui niseme hivyo kwamba na sisi tuna *safal marwa* wanaotoka Bububu wanataka kuja Chukwani watoke Malindi waende wakapande daladala Baraza la Wawakilishi kongwe na wanaotoka Baraza la Wawakilishi wanakuja Malindi.

Kwa hiyo, imekuwa pale kati kati pana *safal marwa* huyu anatoka huku, huyu anakwenda huku. Hakuna mpangilio wowote lakini hata zile boda boda tulizokuwa tukizisikia kule Dar es Salaam kwamba kuna boda boda pia zimeshaanza katika mji wetu, kwa sababu hawa wengine waliokuwa hawaendi kwa miguu basi inabidi wanachukua honda wanapelekwa kutoka Baraza la Wawakilishi kongwe mpaka Malindi. Sasa hii inasababisha hatari barabara zinakuwa hazipitiki kwa magari na hata hao watu wenyewe, sijui Mhe. Waziri hii ndiyo mwisho tushafika kwamba pale ndiyo itakuwa vituo vyetu vya mwisho. Kwa sababu pale Michenzani ninavyoona ni nyumba za watu sasa tunachukua vituo vya daladala tunakwenda kuviweka katika majumba ya watu, mji huu unapangwa vipi.

Mhe. Naibu Spika, mwaka juzi tuliambiwa hapa sijui mwaka jana tuna miradi ya *ZUSP* ya mipango ya miji tutazoa taka, taka hizi tutazibadilisha ziwe umeme, sasa tunazirundikiza mpaka ule mradi wa *ZUSP* uwe ushakuwa tayari ili ukija ukianza zile taka tuwe tunazo humu humu mjini, haiwezekani Mhe. Naibu Spika. Hivi sasa ni aibu tunasema tunaboresha utalii mimi wengine huwa nawauliza huko vipi kivutio chenu kikubwa hasa hapa Zanzibar nini? Wengine wanakwambia unajua huko kwetu sisi hatujaona taka lakini tulipokuja Zanzibar *alhamdulillah* kila unapopita ikinyesha mvua ndiyo haisemeki kabisa.

Sasa hii mipangilio ikoje huyu mtu mpeleke China Mhe. Waziri nakuomba huyu mtu aende akasome akajifunze aje aangalie miji inakuwaje. Mhe. Naibu Spika, leo kuna mayadi katikati ya mji watu wanauziana magari katikati ya miji, zile bustani mnatwambia mara mmeweka bustani, mara sijui mnaweka nini, hii ni aibu huu ni mji na mji ni kivutio kikubwa kwa watu hadi hii leo hatujui tunafanya nini tumekwenda kuweka *park* pale sasa sisi wengine tunaopita na miguu, wengine ni walemavu tutapitisha vigari vyetu wapi, mji umekaa sijui kama uko wapi. Maana kuna miji mengine kule India ikizimwa ile traffic light vile vituktuk vinaweza vikapita elfu mbili au elfu moja *one hour*.

Sasa na sisi tuingie katika utaratibu huo tunataka tuone mabadiliko katika mji hao wanaokuja hawaji kutizama mambo tofauti tofauti tu na mji lazima tuutunze na sisi wenyewe kwa afya zetu. Ukienda sokoni hee! Sijui wengine wanafunga pua Michael Jackson hakufanya kosa kumbe alipokuja Afrika akasema yeye afunge pua yake kwa sababu ya uchafu. Haya tunayataka wenyewe Mheshimiwa magari yapo na nina imani uwezekano wa kupata fedha upo na fedha zipo magari yatiwe mafuta kila leo yazowe taka.

Mhe. Naibu Spika, Manispaa tumeambiwa hapa katika kitabu chao kwamba wamekusanya mapato na wengi waheshimiwa wamesifia kwamba Halmashauri pamoja na Manispaa zilizoko Pemba wamekusanya na zimesifiwa.

Lakini kinachonishangaza Mhe. Naibu Spika kwamba hii Manispaa ya Unguja haikufikia hata asilimia 50. Mimi ninavyofahamu kwamba vianzio vya mapato katika nchi hii vilivyo vingi na vilivyo vikubwa vipo hapa mjini. Sasa Mhe. Waziri inakuwaje inafika kwamba hapa mjini pana vyanzo vikubwa na vidogo wasifikie hata asilimia 50. Na sijui hizi jawabu ambazo umezileta katika kitabu hiki, wewe zimekuridhisha kwamba wakienda wadai kodi hawalipwi, wewe Mhe. Waziri umeridhika nazo hizi jawabu zilizomo katika kitabu.

Micheweni ambako tunakusifia ndiko kuliko na umasikini na wao wamefikia lengo. Sasa najua wewe ni mpya katika wizara hii lakini nakuomba hili ulifuatilie kweli Mji huu usifikie hata asilimia 50, Mji wa Micheweni ufikie asilimia 68? Yaani mantiki haionekani, sasa hili nakuomba uje uniambia ni sababu zipi au ulifanyie kazi ili tujue ni kwa nini hatukufikia hata asilimia 50 katika Mji wetu huu au vyanzo ni vikubwa na vipo kwa wingi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, najua muda unasonga, jambo jengine nataka nilisema ni kuhusu Idara ya Kadi za Utambulisho. Najua Mhe. Waziri Kiswahili unakifahamu na najua una *dialect* wale waliosoma lugha Kitumbatu ni moja katika *dialect* za lugha ya Kiswahili lahaja unafahamu. Najua idara hii inatoka kwa Mhe. Mwinyihaji Makame yeye tulimwambia kwa lugha nyingi hapa sasa sijui kwamba kuondoshwa kwake kumetokana na kwamba ameshindwa ile kazi au kuondoka kwake amepumzishwa kwa sababu amefanya vizuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, moja katika kero zilizopo kwa wananchi ni hapa katika vitambulisho vya Wazanzibari na vitambulisho vyengine. Sasa mimi nataka nikwambie jambo moja na nikukumbushe lakini nitakupeleka kwa Mwenyezi Mungu.

Sisi Mwenyezi Mungu ametuumba na alitusifu sana kwamba sisi ametuumba katika watu tulio bora zaidi maumbo yetu kwa sababu katupa macho ili tujue kwamba lile ni jekundu na lile ni jeupe, akatupa na masikio na fikiri lugha tunazozisema ushaanza kuzisikia na wewe kama alivyoanza kuzisikia Mhe. Mwinyihaji. Nashukuru baada ya maneno mengi alipita katika ziara ikabakia watendaji wake tu ndiyo waliokuwa na makosa, lakini yeye alijitahidi.

Sasa kwa nini tulipewa mambo hayo tukapewa na moyo ili tuweze kutofautisha hili ndilo na hili silo. Kwa mambo hayo Mwenyezi Mungu kwa vile katupa vitu hivyo hawezi kutuhukumu. Sasa ukishindwa kuvitumia vitu hivyo basi Mwenyezi Mungu ndipo anapofika huko atakuhukumu, kwa sababu umeshindwa kuvitumia vitu hivyo. Kakupa macho hukuweza kujua jekundi na jeupe, akakupa masikio ulioambiwa hukutaka kuyasikia, akakupa na moyo hukuweza kupambanua lipi baya na lipi jema. Sasa Mhe. Waziri mimi nakukumbusha wengine wamesema kuna vitambulisho havichukuliwi, kila mmoja kaja na lugha yake kwa sababu Kiswahili ni lugha yetu kila mmoja na maneno hayanunuliwi kusema sema tu wewe, chukua unganisha na ndiyo sifa ya lugha, sema. Lakini bado naendelea kukwambia kwamba katika sekta hii kuna matatizo, umekuja ni mpya tunakuomba hapa pana matatizo uyashughulikie.

Leo ukienda bandarini unaambiwa husafiri kama hujapewa kitambulisho, ukipita ile tiketi anakwambia nipo na kitambulisho, tiketi tayari unayo kitambulisho mimi idara ile haijanipa nifanye nini. Nimekufikisha kwa Mungu nakuomba ujitahidi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe muda uliosalia ni mdogo sana kabla sijaahirisha nina matangazo mawili, kwanza nawashukuru kwa ushiriano mlionipa tangu asubuhi na michango mizuri.

Tangazo la kwanza nimearifiwa na Mnadhimu wa *CUF* kwamba waheshimiwa mkimaliza hapa kuna kikao cha dharura ukumbi wetu wa juu, Wajumbe wote wa *CUF*.

Tangazo la pili kanipa Mhe. Balozi Kiongozi wetu wa Serikali katika Baraza ana shida na Waheshimiwa wawili, Mheshimiwa wa kwanza Jimbo la Kojani na Mheshimiwa wa pili Jimbo la Ole muonane ofisini kwake katika ukumbi wetu wa Baraza hapa ndani.

Na mwisho niwatangazie kwamba tumebakia na wachangiaji kumi na tano wa jioni natanguliza wachangiaji watatu wajihimu ili tuweze kuanza nao wa kwanza ni Mhe. Prof. Ali Mzee Ali, wa pili Mhe. Hija Hassan Hija na wa tatu Mhe. Salim Abdalla Hamad waliosalia tutaendelea nao kidogo kidogo. Baada ya matangazo hayo naakhirisha kikao chetu hadi saa 11:00 za jioni.

(Saa 6:55 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kumaliza kikao chetu cha asubuhi kulikuwa na wachangiaji 12 na watatu walitakiwa kuanza mwanzo, lakini kila nikitizama hapa katika hao namuona Mhe. Hija Hassan Hija. Kwa hiyo, tunaze na Mhe. Hija Hassan Hija baada ya yeye atafuata Mhe. Salum Abdalla Hamad.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukushukuru wewe kwa jinsi ulivyonipatia nafasi ya mwanzo badala ya yapili na naamini kwamba utaniongeza dakika za motisha kwa sababu nilikuwa najiandaa kwa ajili ya nafasi ya pili.

Mhe. Mwenyekitini, nianze kumshukuru sana Mhe. Waziri kaka yangu Mtumbatu halisi na leo nataka niseme kwa nini mimi nimekuwa nikisema Mtumbatu. Mimi ni Mtumbatu kama Mtumbatu ambaye kama waziri huyu, tofauti yake yeye ni mtoto wa mwanamke mimi ni mtoto wa mwanamke. Kwa hivyo, ingelikuwa ni ndoa basi Mhe. Waziri angekuwa mimi ni mke wake halisi. Kwa sababu yeye ametokana na Kheir Omar na mimi Patima Omar ni familia kindakindaki ambapo Mhe. Waziri ni kaka yangu. Mwenyezi Mungu amjaalie asinioe amjaalie uwezo mkubwa wa kuongoza nchi na kwamba asimamie wizara hii aliyopewa kwa uadilifu wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema hayo kwa sababu ni waziri ambaye kwa kweli anajitahidi kusimamia majukumu yake licha ya ufinyu wa bajeti ambao tumekuwa tukiuona. Mchango wangu wa kwanza nianze kwenye suala zima la bajeti. Mhe. Waziri ametuonesha hapa kwamba makusanyo ya mwaka 2013/2014 yalikuwa ni shilingi 4.8 bilioni kwa wastani wa 8.6 kwa mwezi, lakini kwa miezi tisa hadi Machi Mhe. Waziri ametwambia kwamba amekusanya shilingi 2.93 bilioni asilimia 61, yenye wastani wa shilingi 366.03 milioni kwa mwezi. Sasa ambacho wamekipata kwa miezi tisa hiyo, miezi mitatu ni shilingi 1.85 bilioni wastani wa shilingi 616 milioni kwa mwezi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mahesabu haya ni kweli miezi tisa Mhe. Waziri amevuka lengo maana yake ana asilimia 61 ya miezi tisa, lakini kile ambacho kilibakia miezi mitatu ni shilingi 1.85 bilioni wastani wa shilingi 616 milioni kwa kweli ni pesa nyingi. Sasa naomba Mhe. Waziri anambie hii miezi mitatu ya Aprili - Juni ambayo angepaswa akusanye 1.85 bilioni vipi atafanikiwa kuzipata wakati wastani wake ni shilingi 616.4 milioni kwa mwezi badala ya shilingi 326 milioni kwa mwezi. Lakini mwaka huu 2014/2015 Mhe. Waziri ametwambia atakusanya shilingi 5.16 bilioni kwa mwaka wastani wa shilingi 379.24 milioni kwa mwezi, ongezeko la shilingi 430 milioni ya bajeti ya mwaka jana.

Sasa wasiwasi wangu Mhe. Waziri kwamba mwaka jana hakufikia lengo lakini ameongeza shilingi 430 milioni makusanyo. Kwa hivyo, atwambie anafanya nini ili kufikia lengo hili wakati mwaka jana hakufikia lengo halisi kama alivyotuahidi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee na hoja ya pili suala zima la mageuzi ya Serikali ya Mitaa. Jambo hili limezungumzwa karibu miaka 10 tangu tuko Baraza kongwe Kikwajuni tumekuwa tukizungumza habari ya marekebisho ya Serikali za Mitaa, imekuwa ni hadithi ndefu ambayo kwa kweli Wawakilishi imekuwa ikitupa tabu sana, lakini fahari yetu kuona kwamba *Local Government* zinafanyiwa marekebisho ya hali ya juu ili zichangie uchumi wa nchi na pato la mwananchi wa kawaida. Lakini tumekuwa tukipewa hadithi ambazo kwa kweli zinatusikitisha sana. Mhe. Waziri amesema hapa kwamba Serikali za Mitaa zimeajiri wataalamu wazuri. Mimi naomba nimpongeze sana, kwamba ukilinganisha miaka mitatu nyuma na mwaka huu wa 2013/2014 kwa kweli wameajiri angalau wahasibu wenye sifa katika Serikali za Mitaa kwenya Halmashauri zetu za Unguja na Pemba. Ilikuwa nasabu yetu ni wahasibu ambao uwezo wao mdogo lakini sasa hivi angalau wana wahasibu wa digirii ya kwanza katika Serikali za Mitaa Halmashauri za Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri pia amesema kwamba wameongeza mapato, lakini pia wamesimamia nidhamu ya matumizi ya fedha. Sasa hapa ndio nataka mimi nipingane naye, Mhe. Waziri licha ya kuajiri watu wazuri wenye kiwango kizuri cha elimu, na licha ya kwamba ameongeza mapato ya Halmashauri zetu za Unguja na Pemba lakini nidhamu na matumizi yao imekuwa ni hali ngumu sana. Na mimi nimuombe kwamba kama lengo ni kusimamia Serikali za

Mitaa, basi asimamie nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Wenzetu hawa wanadhani kwamba fedha inayoingia kwenye Serikali za Mitaa ni fedha ya watendaji fulani.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano, mwezi huu wa Mei Mhe. Rais wa Zanzibar alifanya kikao na wenzetu hawa wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum na aliwakanya sana na kuwaonya juu ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Mimi nilitegemea kwamba wenzetu wa Pemba hasa Ofisi Kuu Pemba, wangechukua yale maelekezo ya Rais wakajifunza kwamba Rais anakataa ubadhirifu wa fedha za umma. Lakini mwezi huo huo baada ya kurejea kwenye kikao cha Bangokitita waliandaa safari isiyo rasmi ya kwenda Tanga, walitumia kiasi ya shilingi milioni nane mpaka kumi bila ya idhini ya Mabaraza ya Manispaa za Unguja na Pemba. Mhe. Waziri kwa heshima kubwa kwa kuwa nimesema mimi ni ndugu yako wa damu naomba nithikutishe nizuie fungu la Ofisi Kuu Pemba kwa sababu walitumia matumizi ya fedha za Halmashauri za Pemba bila ya idhini ya Mabaraza ya Halmashauri ya Pemba. Tupate maelezo Afisa Mdhamini alipata wapi ruhusa ya kutumia fedha nje ya bajeti iliyotengwa na Mabaraza na kuamua kufanya ziara ambayo haikutengwa na Baraza kwa ajili ya safari ya Tanga ambayo iko nje ya bajeti ya 2013/2014.

Kwa hiyo, nipate maelezo hayo kwa nini Afisa Mdhamini alithubutu kukiuka maelekezo ya Mabaraza ya Pemba yale wakati iko miradi ya maendeleo Pemba haijatekelezwa lakini aliamua kufanya safari ya Tanga bila ya kibali cha Mabaraza ya Pemba, kwa nini alitumia fedha hiyo naomba nipate maelezo na naomba nizuie fungu hili ili tupate maelezo ya kina kwa nini alikiuka maagizo ya Mabaraza ya Pemba wakati ndio wenye mamlaka ya kuagiza matumizi na mapato ya serikali kupitia Halmashauri hizo.

Mhe Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye Mradi wa *ZUSP*. Mradi huu ni fedha za mkopo kwenye Benki ya Dunia. Mhe. Rais mradi huu alipouzindua kwa kweli aliwapa matumaini wananchi na kuwaambia kwamba mradi huu utaimarisha taa za barabarani na kuimarisha taa kwa maeneo ya mitaa mbali mbali *stop light*, sambamba na kuimarisha utendaji mzuri wa Halmashauri zetu na Mabaraza ya Miji ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa taka na kuondoa uchafu katika miji.

Lakini Rais amezungumza kauli hiyo na tayari fedha imetolewa, lakini jambo hili limekuwa ni baya zaidi sasa uchafu umeongezeka, kasi ya udhaifu wa Mabaraza yetu yameongezeka na lao hapa tumeambiwa asubuhi mradi huu moja ya component yake ni matengenezo na ujenzi wa Soko la Wete, soko ambalo ramani inaonesha kwamba sehemu ya soko hilo tayari ameuziwa Bwana Battash.

Sasa wakati mradi una ujenzi wa soko la Mapete, mradi una sehemu ya ujenzi wa Soko la Wete lakini sehemu ya soko hilo tayari watendaji wamemuuzia Mapete. Sasa mnawadanganya Wazanzibari au mnawadanganya Wazungu waliotoa pesa zao.

Kwa hivyo, na hapa nazuia fungu, kwa nini mmeandika mchanganuo kuomba fedha za umma Wizara ya Fedha wakajenga hoja wakatafuta fedha kumbwe sehemu ya eneo hilo la Soko la Wete tayari mmemuuzia Mapete bila ya kibali cha serikali kuu. Naomba nipate maelezo kwa nini wakachukua maamuzi hayo huku wakijua kwamba sehemu hiyo ya Soko la Wete tayari imeomba fedha za Benki ya Dunia na kweli Wizara ya Fedha hizo na fedha ziko kwenye *account* za serikali lakini huku mnauza mali ambayo kwa kweli hakuruhusiwa na Serikali Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, hili Mhe. Waziri naomba pia anipe maelezo na nawaomba sana waheshimiwa Wawakilishi wenzangu kwamba mradi huu wa soko la Wete ni mradi ambao fedha za serikali zimeidhinishwa na wahisani kupitia Benki ya Dunia na na kwa nini wenzetu wakamuuzia Mapete bila ya ruhusa ya Serikali Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka niliseme ni suala zima la Vikosi vya SMZ. Watu wengi wanashangaa hasa *CUF* wanapowasifu vikosi vya SMZ. Hivi kama Mwakilishi tunaamini kwamba hivi ni vikosi halali vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vipo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na sheria zetu. Ingawa wakati mwengine hutupiga bakora sana vikosi lakini ni vyetu. Kwa hivyo tuna haki ya kuwatetea pale wanapoonewa na kuna haki ya kuwaambi hivyo sivyo pale ambapo wamefanya makosa. Kwa hivyo, vikosi vyetu Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alikuwa Waziri wa Utumishi wa Umma mwaka jana hapa, na tulimwambia kwamba wewe ni waziri wa Utumishi wa Umma una haki ya kutengeneza maslahi ya vikosi, wakati ule labda ilikuwa hatuelewi kwa sababu alikuwa ana dhamana ya serikali nzima ya utumishi wa umma, leo Mwenyezi Munmgu amempeleka kwenye vikosi anaona ugumu wa vikosi vyetu vinavyokula tabu.

Mhe. Mwenyekiti, juzi vikosi hivi baadhi yao vimehamishwa Pemba kuja Unguja hata posho la uhamisho limeshinda kupatikana. Askari wetu wale wamekuwa wakihangaika kama vile omba omba mitaani, kwa kweli si sura nzuri lazima serikali ilinde masuala ya vikosi na wawafanyie haki kwa maslahi yao, na hawa tukiwadhalilisha watakuwa wanavunja ile ari yao waliyonayo ya ulinzi na wanaweza wakasababisha madhara makubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *scheme of service* ya vikosi naomba tuelezwe limefikia wapi, licha ya kuambiwa kwamba iko mbioni inarekiebishwa lakini haijulikani hatima yake. Mishahara ya wenzetu hawa askari wa Vikosi vya SMZ kwa kweli ni midogo sana, tumekuwa tukichungulia wamekuwa wakitwambia maslahi yao binafsi ambayo kwa kweli ni madogo sana na ya kutisha tena ni vikosi vyote vya Zanzibar, humjui Mkuu wa Kikosi, humjui askari wa kawaida, humjui askari mwenye cheo cha kati; maslahi yao ni madogo sana jambo ambalo kwa kweli linavunja haiba ya vikosi vyetu kama walinzi wa raia na mali zao hapa Zanzibar.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri nimuombe sana kaka yangu kwamba atupe maelezo kwa nini maslahi ya vikosi hayajazingatiwa ipasavyo. Kuna tofauti kubwa baina ya mtumishi wa vikosi na mtumishi wa serikali wa kawaida juu ya maslahi wakati kazi hii ya ulinzi ni kazi ngumu, ni kazi ya kuriski maisha ya watu na ni kazi ambayo kwa kweli wanahitajika kupewa maslahi mazuri kama walinzi wa Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nimuombe kwamba maslahi ya vikosi tupate maelezo ya kina ikiwa ni pamoja na masuala mazima ya *scheme of service*.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni suala la mikoa, sehemu ya mwanzo ambayo nataka nizungumze ni suala zima la Mkoa wa Kaskazini Unguja. Mkoa huu umekuwa ukishutumiwa sana kwa usalama wa raia na mali zao, wenzangu wamekuwa wakizungumza hapa juu ya wimbi la uingiaji wa wageni, uhalifu na mambo ambayo hayapendezi.

Lakini hivi karibuni tumesikia mgogoro baina ya watu wa Tumbatu ya Kisiwani na Tumbatu ya juu, kwa maana ya Tumbatu ya kisiwani na Tumbatu ya Kivunge. Mgogoro ambao baada ya kufuatilia tumegundua kwamba ni ahadi tu ya Serikali ya Mkoa imeshindwa kuwatimizia ahadi Watumbatu wa juu na hatimaye sasa wamekuwa na mgogoro na Watumbatu wa kisiwani. Ninavyowajua mimi Watumbatu si watu wa shari ni watu wastaarabu sana, mpaka Mtumbatu anaamua kuchukua hatua maana yake jambo limemfika kifuani. Sasa naomba Mhe. Waziri atueleze kulikoni kwa nini Serikali ya Mkoa ikasababisha matatizo kati ya Watumbatu wa Kivunge na Watumbatu wa kisiwani jambo ambalo hawa ni ndugu wa familia moja na ni watu wanaopendana, kama kuna tatizo ni tatizo gani. Naomba Mhe. Waziri atueleze na lifanyiwe dawa haraka ili watu hawa ndugu waweze kuelewana na kufikia ufanisi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hoja nyengine ambayo naomba nichangie ni suala zima la Ofisi ya Usajili na Vitambulisho vya Mzanzibari. Wanaozungumza kwamba ofisi hii imefikia ufanisi mzuri mimi nakubaliana nao, lakini wanaozungumza kwamba ofisi hii imekuwa ni chanzo cha matatizo kwa haki za watu pia wako sahihi. Mhehsimiwa ni jambo ambalo halina siri, licha ya ofisi hii kutoa kadi za uraia kwa Wazanzibari Wakaazi wengi, lakini bado Wazanzibari Wakaazi wenye haki wamekuwa wakinyimwa haki hii bila ya sababu za msingi. Mhe. Waziri sisi ni viongozi na kiongozi lazima awe kioo na hapa duniani Mhe. Mwenyekiti, watu wote wanapitalazima walinde haki za watu bila ya utashi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Waziri mwaka jana Dr. Mwinyihaji Makame alifanya kazi kubwa, alitupa orodha ya watu wa Unguja na Pemba wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi lakini bado uchunguzi wa kina watu wale walipewa vipande ambao si halali ni vitatu, vinne mpaka vitano; wale wenye haki hasa mpaka hii leo hawajapatiwa haki yao jambo ambalo watu wanadhalilika. Nataka kusema kwamba vipande hivi si kwa ajili ya kura tu, vipande hivi ni kwa ajili ya maisha, ni kwa ajili ya masuala ya benki, ni kwa ajili ya masuala ya mikopo ya elimu ya juu, masuala ya usafiri na mambo mengine. Kwa hivyo, unapomnyima Mzanzibari mkaazi haki hii sio kwamba unamnyima kupiga kura tu, lakini unamnyima haki zake za msingi kwa maana ya usafiri, matibabu, benki na hata elimu. Mhe. Waziri nikuombe sana utimize uungwana kama ulivyokuwa muungwana kutatua tatizo hili la vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi ili Wazanzibari wote wenye sifa wapate haki hii. Vile vile apige vita wale wote ambao si Wazanzibari halali kupata haki hii.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Waziri na wasiwasi sisi Wawakilishi wake tuko tayari kumsaidia maelezo kwa nini kuna watu wamepewa haki hii na si Wazanzibari wakaazi, kwa nini serikali imethubutu kufanya hivyo, kuna watu

wanapewa vitambulisho hivi wakati hawana sifa za ukaazi na wale wenye sifa za ukaazi wamekuwa wakinyimwa haki hiyo ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala zima la Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, niipongeze sana wilaya yangu hiyo kwa kuongeza mapato. Lakini bado nawaomba niwaambie kwamba mapato waliyoyapanga ya shilingi 75 bilioni nadhani yanaweza kufikiwa kwa kiwango kikubwa. Ni wajibu wao sasa kama watendaji wazuri wajipange na watafute vyanzo vizuri zaidi waongeze mapato ili Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mkoani iwe ni kigezo kama ilivyo Wilaya ya Kaskazini 'B', Kaskazini 'A' na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa niseme kwamba bajeti ya vikosi ni bajeti moja kubwa sana ukilinganisha na bajeti nyengine za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya na wizara nyengine. Lakini tumepata malalamiko ya watendaji wetu wa askari kupata mishahara midogo, sisi hatuoni sababu ya msingi. Kwa hiyo ningemuomba Mhe. Waziri asimamie sana maslahi ya wafanyakazi wetu wa vikosi ili manung'uniko na udhalilishaji wa vikosi vyetu yaweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo Mhe. Waziri akinipa maelezo ya fungu la Ofisi Kuu Pemba ya matumizi ya fedha zaidi ya shilingi milioni kumi nitaunga mkono hoja hii na asiponipa hoja hiyo nitazuia fungu la Pemba kwa sababu wametumia fedha za Halmashauri za Pemba bila ya idhini ya Mabaraza, naomba anipe maelezo hayo Mhe. Waziri. Nashukuru sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii jioni hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri ngangari, Waziri kijana ambaye ataiongoza Wizara hii kama tunavyotegemea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nizipongeze Halmashauri zote kwa Unguja na Pemba kwa kufanya kazi zake zote vizuri, lakini niseme kwamba Halmashauri hizi bado zinahitaji kupatiwa elimu na pia kupatiwa vitendea kazi ili ziweze kufanya kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kupatiwa elimu na semina kwa Halmashauri hizi, Halmashauri zinahitaji vyanzo vyengine vya mapato licha ya kutegemea vyanzo vya kutoka kwa wananchi.
Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba sitokuwa mwema wakati sitoisifu Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mkoani pamoja na Baraza la Mji la Wilaya ya Mkoani kwa kuvuka lengo la asilimia 177.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza sana Wilaya yangu hii ingawaje wengine wanajiuliza kwamba kuna sababu zipi hata kufikia hivyo. Lakini naamini kilichoandikwa humu ndicho kilichotendeka katika Wilaya hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Madiwani. Mhe. Mwenyekiti, Madiwani ni viongozi kama viongozi wengine, na wao wanahitaji kutendewa haki kama wanavyotendewa viongozi wengine.

Mhe. Mwenyekiti, Madiwani wanafanya kazi kubwa mno katika Wilaya zao, lakini ukiangalia mishahara hawana. Kwa hiyo nimuombe Mhe. Waziri awaangalie sana Madiwani jinsi wanavyofanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara ya Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu kubwa sana la kuratibu wananchi wake waliomo katika Wilaya zao. Lakini pia niseme kwamba Sheha yupo chini ya Mkuu wa Wilaya, lakini pia Sheha ana wajibu wa kuwa pamoja na wananchi wake. Sheha huyo huyo Mhe. Mwenyekiti, si vyema kusikia kwamba anawabagua baadhi ya wananchi wake. Lakini pia nishukuru kwa sasa hivi kwa Sheha wetu wanayo afadhali na tunaungana vizuri tu. Lakini baada ya kusifiwa Mhe. Mwenyekiti, wasije wakalitia tembo maji. Vile vile niseme kwamba Masheha hawa hawana haki ya kuwa wao wanashiriki katika migogoro, hasa migogoro ya ardhi. Masheha hilo si jukumu lao isipokuwa wao wawe pamoja na wananchi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika vikosi kama walivyosema wenzangu. Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kuvisifu sana kwa sababu vikosi vimesifiwa sana na vimeombewa sana, kwa hiyo na mimi niseme kwamba hivi vikosi vinahitaji kusaidiwa sana.

Lakini vile vile niseme katika Kambi ya Kangagani. Mhe. Mwenyekiti, nilikwenda Kambi ya Kangagani tukiwemo mimi na wewe pamoja, tukaiona hali ya askari wetu waliopo Kangagani, jinsi ya makaazi yao yalivyo. Mhe. Mwenyekiti, askari hawa tunawaonea sana. Analala askari anahesabu mwezi na nyota, juu nyumba inavuja pa kulala

hana. Je, kweli askari huyu tunamtendea haki? Kutwa nzima anafanya kazi mtu kama yule halafu anarudi nyumbani anataka apumzike, pa kupumzika anachuchumaa. Hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie sana kwa askari wetu hawa ili na wao wapate makaazi yaliyo mema. Kwa sababu tukisema askari tunawafanyia kama hivi hili ni tatizo kubwa sana. Askari wetu kama wanavyotulinda sisi na wao wanahitaji walindwe kwa makaazi yao na kupata mahitaji yao yaliyo mema. Wanalinda viongozi mchana wa kutwa, wananchi nchi mchana wa kutwa hawalali, kucha nzima wao wapo njiani wanasimama kulinda nchi yetu na raia wake pamoja na viongozi wao. Kwa hiyo na wao wana haki ya kulindwa; wana haki ya kufanyiwa kila lililo na haki kwa askari wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika soko la Kangani. Namuuliza Mhe. Waziri, kinachozorotesha soko la Kangani ni kitu gani, mpaka hii leo ikawa soko hili bado halijamaliza kujengwa na watu bado wanauza samaki chini. Namuomba Mhe. Waziri akija hapa aje anipe maelezo ya soko hili la Kangani.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Mkoa huu kuwa mkubwa na ongezeko la watu, na kutokana na shughuli nyingi za maendeleo, na kwa kuwa Mkoa huu ni kioo cha Wazanzibari. Mhe. Mwenyekiti, naona haukutendewa haki Mkoa huu kupata asilimia 54; ambayo Mkoa huu ndio jaa lote linalouegemea Mkoa huu. Namuomba Mhe. Waziri Mkoa huu aufikirie zaidi kutokana na makaazi ya watu walio wengi na shughuli nyingi zinazotendekana katika Mkoa huu, lakini vile vile kupata asilimia 54 ni kuuzorotesha huu Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kikosi cha KMKM. Nakipongeza kikosi hichi kwa kuendelea na doria katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba na kuweza kudhibiti bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Mkoa wa Kusini Pemba ukurasa wa 53 kifungu cha 129. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi kinasema kwamba "Mkoa umefanikiwa kutoa mafunzo juu ya mbinu za kijikinga na VVU na athari za kutokana na Ukimwi. Pia Mhe. Mwenyekiti, mafunzo haya yalitolewa kwa wafanyakazi 74, wanawake 37 na wanaume 37. Na Masheha 62, wanawake 6 na wanaume 56. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wafanyakazi hawa waliojitolea kupima virusi vya Ukimwi kwa ridhaa zao na bila ya kulazimishwa. Lakini vile vile niseme kwamba niwaombe watu hawa wasiishie hapo tu, bali wazidi kujilinda na kuelimisha jamii ya wale ambao hawajui nini VVU ili waende kupima.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 17 kifungu cha 40 Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi kinasema "Ofisi imesajili Wazanzibari wakaazi 24,379 waliotimiza masharti ya usajili. Imetengeneza vitambulisho vipya 25,078 vilivyomaliza muda wake wa matumizi, na imetengeneza vitambulisho 3,236 kwa wananchi waliopoteza na walioomba kufanya marekebisho halali ya taarifa zao binafsi".

Sasa niseme Mhe. Mwenyekiti, hawa Wazanzibari wakaazi 24,379 waliosajiliwa vitambulisho vyao vimetengenezwa vingapi. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifahamishe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niseme nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia chochote katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.
Mhe. Mwenyekiti, nianze na Ofisi ya Usajili na Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kakabidhiwa Wizara hii, Wizara kubwa, Wizara nyeti yenye watu wataalamu, Wizara tunayoitegemea kwa kutoa haki kwa mujibu wa Katiba. Wizara tunayoitegemea kwa kuweka ulinzi na usalama katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya haki ya Wazanzibari ni kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Na hii imeelezwa katika Sheria Nam. 7 ya mwaka 2005. Mhe. Mwenyekiti, katika sheria hii kifungu cha 5 ambacho kinaeleza Mkurugenzi wa Vitambulisho na Kazi zake japokuwa imeandikwa kwa Kiingereza lakini tafsiri yake ni kuwa “Mkurugenzi wa Vitambulisho atafanya kazi kutokana na maelekezo ya Waziri husika”. Hii kutokana na maelekezo katumia neno “*directives”* za Waziri ndio ninayoizungumzia.

Kwa sababu kumeingizwa kifungu hicho ina maana Mhe. Waziri ndie mwenye mamlaka ya kazi za vitambulisho ifanywe vipi katika kusajili watu wapya, kuwaingiza katika daftari la majina na kadhalika kama sheria ilivyoeleza.

Nashukuru sana na katika Wilaya nyingi baada ya hili kulizungumza na Waziri aliyekuwepo Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa makusudi akafanya ziara Zanzibar nzima. Tumeshirikiana na *Alhamdulillah* kwa baadhi ya sehemu Mikoa mingine kazi inakwenda vizuri sana. Lakini bado tuna masikitiko makubwa na wala Mheshimiwa asiniambie nimtajie, akionana na mimi nitampa majina na orodha hasa, kuwa kuna baadhi ya sehemu Masheha hawatoi kabisa, na kwa bahati mbaya hata wale ambao wamepewa barua halafu wakapewa vile vyeti vya kwenda kuchukulia vitambulisho siku zikifika wapo baadhi wamenyang'anywa. Kwa hiyo nasikitika kuwa kumkosesha mwananchi haki yake ni kwenda kinyume na Katiba.

Mimi namjua Mhe. Waziri ni mtu mzuri na hili linamuuma, kwa hiyo namuomba alitolee ufafanuzi ili katika uandikishaji wa mwisho utakaofanywa kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 iwe kila Mzanzibari anayestahiki kupiga kura awe ameshapata kitambulisho cha Mzanzibari na atapata kuandikishwa kama mpiga kura. Namuomba sana Mhe. Waziri kwa hilo, akitaka kujua ni wapi na wapi *inshaallah* tukionana nitamuelekeza.

Halafu jengine Mhe. Mwenyekiti, niingie katika Halmashauri za Wilaya pamoja na Mabaraza ya Miji. Tukifungua kitabu hichi cha bajeti ukurasa wa 88 na 89 kumetolewa taarifa kuhusu mapato ya Serikali za Mitaa Zanzibar kwa kipindi cha miezi 9, yaani Julai, 2013 hadi Machi, 2014. Na maelezo haya yamegawika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni makusanyo, na sehemu ya pili ni matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, nimekiangalia hichi kitabu nimeona kuna mambo ambayo mimi mwenyewe hayakuniridhisha na kwa maslahi ya shughuli za kiserikali ziende sawa nimewajibika nieleze kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Baraza la Manispaa na Halmashauri za Wilaya ya Magharibi, Wilaya ya Kaskazini "A", Wilaya ya Kaskazini "B", na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini, hata Wilaya ya Kati, wao nashukuru katika makadirio ya makusanyo kwa kipindi cha mwaka mzima wameweka idadi angalau inayoelekea. Ni kuanzia milioni 2,000,000/= kwa kule juu, halafu milioni 800,177/= na kadhalika. Lakini ukienda Baraza la Mji Mkoani, Halmashauri ya Chake Chake, Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani, Halmashauri ya Wilaya ya Wete, Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni, pamoja na Baraza la Mji Wete, Mkoani na Chake Chake hali ni mbaya sana.

Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, mfano Halmashauri ya Wilaya ya Kati iweke makadirio ya kukusanya shilingi milioni 200, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake milioni 48 tu. Halmashauri ni za aina moja japo visiwa mbali mbali lakini tofauti hii iliyopo kutoka milioni 200 mpaka 48 inasikitisha.

Sasa tukiangalia hapa Baraza la Mji Chake Chake ni milioni 100, lakini Baraza la Mji la Wete ni milioni 65 tu. Sasa mambo kama haya yanasikitisha, yanaonesha wazi kuwa wenzetu na wengi katika Halmashauri za Wilaya ziliopo Pemba hawapo *serious* katika kukaa pamoja na wakaona vipi tunaweza kukusanya fedha kutokana na vyanzo vyetu ambavyo wanavijua ni vya muda mrefu na ni maarufu. Sasa matokeo yake ambayo ni ya kusikitisha.

Baraza la Mji lilitakiwa kukusanya kwa mwaka mzima milioni 40 tu, lakini kwa sababu hesabu haikuwa sahihi kwa makusanyo ya robo tatu tu imepita ile milioni 42 imekuwa milioni 52. Baraza la Mji Chake Chake milioni 100, baada ya robo tatu tu za makusanyo imepita imekuwa milioni 107, hiyo ni asilimia 136.

Baraza la Mji Wete walitakiwa kukusanya milioni 42 kwa robo tatu na walikusanya milioni hizo hizo 42.

Lakini tukija Halmashauri ya Chake Chake ambayo ilikadiriwa kwa robo tatu kukusanya milioni 36, imekusanya milioni 47. Tukija Halmashauri ya Mkoani ambayo ilitakiwa kwa robo tatu ikusanye milioni 38, imekusanya milioni 74 sawa na asilimia 195 yaani mara mbili. Na Halmashauri ya Wilaya ya Wete ambayo ilitakiwa kwa robo tatu ikusanye milioni 51 na kidogo, imekusanya milioni 67. Na tukimalizia Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni ambayo ilitakiwa kwa robo tatu ikusanye milioni 65, imekusanya milioni 69 sawa na asilimia 1.152. Hapa ninasema vipo vyanzo vya mapato na wenzetu kama wangekuwa kweli wanachukua umakini katika kuweka makisio katika vikao vyao, wangeliweka hali ikafanana kama zile zilivyo Halmashauri za Wilaya za Unguja. Kwa nini huku Kisiwani Unguja mambo yawe mazuri kule watu wakadirie mambo kidogo lakini wakusanye mengi.

Kwa hivyo mimi siwasifu kwa kuvuka lengo, mimi ninasema hawakuwa *serious* katika kukusanya mapato. Mhe. Mwenyekiti, halafu Halmashauri hizo hizo zimeekewa makadirio ya matumizi kwa robo ya tatu. Sasa mfano Halmashauri ya Wilaya ya Mkoani ambayo ilikaridiwa kufanya matumizi ya robo tatu milioni 36 na kidogo, imetumia milioni 45 Wilaya ya Chake-Chake.

Wilaya ya Mkoani milioni 38 na kidogo imetumia milioni 70, Wilaya ya Wete milioni 51 imetumia milioni 57 na Micheweni milioni 68, imetumia milioni 99, imetumia sawa na asilimia 152.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hata yale matumizi waliyoekewa watumie, watumie zaidi. Kwa hivyo kwa takwimu hizi ninasema kuwa ningeliomba Mhe. Waziri afanye kila inavyowezekana hawa watu wafanyiwe semina ili waieleze hali halisi ilivyo kama wenzetu wa Kisiwa cha Unguja walivyofanya. Hilo ni jengine.

Mhe. Mwenyekiti, halafu mimi nianze kuzungumza kidogo kuhusu masoko. Kwa ufupi tu tunajua tuna Soko Kuu liliopo Darajani. Mhe. Waziri anasema kuwa linafanyiwa matengenezo lakini soko lipo katika hali mbaya, soko lipo kwenye mji, soko ni kielelezo kwa hali yetu halisi ilivyo. Naomba lile soko kuwekwa na uchafu kama vile, kuuzwa samaki mpaka nje, unapopita pananuka vumba, tena kati kati ya mji na hali ya ndani ilivyo mbaya, azidi kujiimarisha ili soko hili liwe kivutio na kielelezo kwa wanaokuja kutembea.

La pili nishukuru kuwa tulikuwa tukizungumza sana kuhusu soko la Mwanakwerekwe kuwa limezidiwa, na lile soko la Mombasa ninashukuru likafunguliwa rasmi ili lifanye kazi na hivi sasa hali yake *alhamdulillah* inaridhisha. Lakini kwa bahati mbaya ukiingia katika soko la Mombasa si siku za Kaskazi na zaidi siku za mvua halikaliki lipo katika hali mbaya sana. Wakati wanaofanya kazi zao za kujitafutia maisha wanalipia kodi kama kawaida. Kwa hivyo ninaiomba serikali lile soko iliangalie, usafi upatikane kwa sababu hizo zinazouzwa ni bidhaa na sisi ndio tunaotumia. Kwa hivyo liwe katika hali ya kustahiki.

Mhe. Mwenyekiti, halafu tukija pale Wete ili kurudia usione vibaya. Tuna soko lile la Wete la matunda na soko la samaki, yote lile ni eneo moja tokea enzi na enzi. Mwenyezi Mungu amuweke mahala pema Mhe. Hamad Khamis alitueleza katika kipindi cha bajeti kilichopita kuwa pale pana mpango wa kujenga soko kubwa sana, na fedha tayari zimeshaombwa zimeshapatikana, na kwa maana hiyo hata wengine waka-*engage* pale wafungue milango ya kufanya biashara za maduka kwa sababu alisema kutakuwa na milango hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kuwa eneo la soko lile hivi sasa tunasikia limeuzwa na limeuzwa baada ya yule mzee kufa. Basi sijui kulipita nini mpaka soko lile likauzwa. Sasa kuna sehemu tayari imeshazungushwa mabati. Wale watu waliokuwa waki-*pack* magari yao ya abiria pale kama watu wa Gando, Mtambwe na kadhalika ndio hawana pa kuyapeleka. Kuuzwa kwa sehemu ile kama ni kweli naona serikali haikufanya jambo jema hata kidogo. Kwa sababu katika mji wa Wete pale ndio pahali nyeti, tunalihitaji hilo soko, tunaihitaji ile stendi ambayo hivi sasa tayari imeshakuwa ndogo lakini ikiwa hata eneo limeuzwa, mimi nitakuwa mgumu sana wa kukubali kupitisha bajeti hii kama sikupata maelezo ya kuridhisha. Kwa nini soko lile liuzwe badala ya kukuzwa tukapata faida sote.

Mhe Mwenyekiti, halafu tulishuhudia hivi karibuni kuwa ile stendi pale ya magari ya abiria pale Darajani iliondoshwa, na nitoe pongezi kwa vikosi vyetu vya ulinzi, wao ni watu *alhamdulillah* ni walinzi wanafuata amri, walikaa pale na ilikuwa hapana hata gari moja inayopita. Kuondolewa kwa kituo kile, kimetokea kwa mtawanyiko wa vituo ambavyo havikuwa rasmi. Sasa katika mji ule ni balaa tupu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina maswali mawili. Swali la kwanza, hasa tulikuwa na dhamira gani kuondoa pale kile kituo wakati tokea enzi na enzi ndio pahala petu palikuwa pachafu tukapiga makelele pote pakawekwa saruji safi pakaondolewa. Hasa kuna dhamira gani.

Halafu baada ya kuondoa, mbona sasa panawekwa gari zinakuja pale gari pale zina-*pack* na zinalipia mapato. Hivyo kuweka gari moja kwa shilingi mia tano ni bora kuliko kutoa huduma kwa wananchi wanaotoa kodi katika nchi yao. Naomba nipate maelezo vyenginevyo vile vile sitoweza kukubali hivi hivi. (*Makofi*).

Halafu huu mtiririko wa mtu kuweka kituo pale anapotaka, ukienda Baraza la Wawakilishi kongwe magari mpaka pale kwenye krosi hatari tupu, ukienda Afisi Kuu ya chama, Chama Tawala sasa inakuwa afisi kuu ya vurugu. Pale pana watoto wa skuli wanapata dhiki. Sasa kwa nini tunaondoa hatuweki pahala ambako ikaonekana sasa hii ni nchi ya amani, utulivu, ustaarabu na yenye mipango, tukaondoa tukaacha watu wakatawanyika kama nzige. Huu si utaratibu mzuri. Kwa hivyo naomba nipate maelezo ambayo yataridhisha, kwa nini pale pakaondolewa na badala yake zogo likawa kubwa zaidi kuliko tulivyokuwa tukitarajia. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa mujibu wa kifungu nambari 24 (2) cha sheria ya fedha ambayo sheria hii ni nambari 12 ya 2005. Sheria hii inazitaka taasisi zote za serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hesabu za mwaka; ambazo hesabu hizi zinajumuisha mapato na matumizi ya taasisi husika. Aidha kifungu nambari 8 cha kifungu hicho hicho cha sheria kinawataka wasimamizi wa fedha katika taasisi husika kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hesabu zao za mwisho wa mwaka miezi mitatu baada ya kukamilisha kipindi cha mwaka.

Sasa basi kwa bahati mbaya tukiangalia kitabu hichi cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za 2011/2012, inatupa picha halisi ya baadhi ya taasisi ziliomo katika Wizara hii ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maaluma za SMZ ilivyokuwa haziendi kwa mujibu wa inavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikuarifu kuwa katika taarifa ya kitabu hichi, Halmashauri zote za Wilaya...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika 2.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Aah!. Halmashauri zote za Wilaya za Pemba na Unguja hakuna hata moja iliyowasilisha. Halafu kuna taasisi mfano Kikosi cha KMKM, Kikosi cha Valantia, Jeshi la Kujenga Uchumi, Kikosi cha Zimamoto, Chuo cha Mafunzo, Mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa Kusini Unguja, Mkoa wa Kaskazini Pemba, Msajili wa Vitambulisho na kadhalika. Na hawa wote walipeleka kinyume na wakati, yaani walicheleweshe, walipeleka wakati umeshapita.
Kwa hivyo ndio tuliyorithi katika kitabu kilichopita, hatujui kinachokuja kwa ufanisi mzuri wa kazi, ninaomba Mhe. Waziri ahakikishe kuwa hizi taasisi zake zinapeleka mahesabu kwa wakati, kwa sababu kutopeleka kwa wakati ni kusababisha serikali isiwe na hali halisi ya mahesabu kama inavyotakikana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu umenipa muda mfupi na sipendi niendelee tena, ijapokuwa sikuridhika vizuri sana kwa sababu wakati ni mdogo. Ninashukuru kwa hiyo nafasi niliyopata. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Nimekupa muda wa dakika 20 Mheshimiwa si mdogo kama wenzio. Mhe. Ali Mzee Ali baada hapo Mhe. Fatma Said Mbarouk na baadae Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana kunipanga mimi baadae Mhe. Fatma Said Mbarouk. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii. Na nitangulie kwa kusema ninaiunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia, na ninawaomba Wajumbe wa Baraza hili tuunge mkono aweze kutekeleza tuliyomuomba.

Waheshimiwa wengi; Mhe. Ismail Ismail Ladhu na wengine wameonesha imani ya hali juu kwa Mhe. Haji Omar Kheri. (*Makofi*).

Mimi ninakubaliana nao Mhe. Haji Omar Kheri kwa sababu ninamuelewa, mzoefu, amekuwa mwakilishi kwa miaka 15. Kipindi hichi sasa hivi amekuwa waziri, kwa hivyo ni mtu ambaye anaelewa na anafahamu.

Mhe. Waziri ninakuomba umekabidhiwa wizara hii mwezi wa Agosti, mwaka bado. Ninakuomba sana upokee michango yote uliyopewa, ushirikiane na Wajumbe wa Baraza hili, ushirikiane na Tume mbali mbali zilizoundwa kwenye sekta yako, hasa Manispaa, kwa pamoja tufanye kazi tuweze kusonga mbele katika wizara hii. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii tumeipitisha, ni bajeti ambayo ni finyu sana lakini atakapofika Waziri wa Fedha siku yake, tutazungumza zaidi. Hali ya fedha inafahamika lakini yapo mambo yanawezekana kufanyika tukishirikiana; sisi Wajumbe wa Baraza na wewe Mhe. Waziri tutafuzu na tutafika mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze na nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza kwa ukamilifu sera za Chama cha Mapinduzi na sera ya serikali. Mhe. Rais hajabahatisha alivyofanya uteuzi wako Mhe. Haji Omar Kheri kukupa wizara hii. (*Makofi*).

Mhe.Mwenyekiti, nimepata faraja kubwa sana katika maisha yangu wiki hii. Mimi nipo miaka 14 humu ndani. Tumepitisha sheria nyingi humu ndani za Masheha, za Valantia, na nyenginezo. Leo ninapata faraja kila anayesimama anazungumza juu ya vikosi vyetu, anazungumza sasa hivi pengine juu ya Masheha wetu wanaanza ku-*improve, alhamdulillah*. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vikosi vyetu na mimi ninaungana na wenzangu kwamba vikosi vyetu kwa ujumla vyote vitano au sita, hivi ni vikosi vyetu sisi wananchi wa Zanzibar. Naomba nimnukuu Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi kwa ruhusa yako, "Hivyo saa nane za usiku wa Jumamosi kuamkia Jumapili tarehe 12 Januari, 1964 nguvu za wanyonge zilipasua na kuvunja boma zilizokuwa zimefungiwa, zikamilikiwa, zikakumbwa, zikaondoa na kusafisha milele uchafu na aibu ya kutawaliwa kwa mabavu na hadaa katika karne ya leo". Haya ni maneno aliyasema Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi wakati anahutubia Baraza la Wawakilishi mwaka 1980. (*Makofi*).

Sasa ukombozi huo Mhe. Mwenyekiti uliofanywa, hivi karibuni tulisherehekea miaka 50 ya Mapinduzi. Walioyalinda, kuyatetea na yakafika miaka 50, hakuna wengine isipokuwa ni vikosi vyetu. Vikosi vyetu ndivyo vilivyofanya kazi hiyo bila ya kujali mshahara, uzalendo ndio uliowafanya waweze kufanya kazi hiyo. (*Makofi*).

Sasa miaka 50 imemalizika vikosi vyetu vipo, ninaungana na wote waliosema kwamba wakati umefika sasa tutizame maslahi ya vikosi vyetu. Vikosi vyetu vilipata nasaha za Mzee Karume aliwaambia hivi, "Poteza maisha yako kwa kuokoa nchi yako, tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako, tukuza Taifa lako katika uhai wako". (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, vikosi vyetu, hiyo ndio misingi yake. Mhe. Haji Omar Kheri nipelekee salamu kwa Kamanda Mkuu wa jeshi letu. Tusome Katiba katika sura ya 10 Idara Maalum. “Rais atakuwa Kamanda Mkuu wa Idara Maalum na atakuwa na uwezo wa kufanya chochote kile anachohisi kwa maslahi ya Taifa letu". Sasa Kamanda Mkuu wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ndiye kamanda wa vikosi vyetu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri tupelekee salamu zetu aendelee kuvilinda, kuvienzi na sisi tupo nyuma yake. Hiyo niliona niseme kuhusu hivi vikosi. Mengi yamesemwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumze hali ya kuwa kuna sheria inayoitwa *Regional Administration Authority Act* ya 1999. Sheria hii ilitiwa saini na Dkt. Salmin Amour Juma. Sheria hii nimeipitia na nikatizama sheria zote sijaona kufanyiwa mabadiliko. Kwa hivyo ni sheria halali. Lakini sheria hii ni sheria kibogoyo, kwa sababu sheria hii inaweka *Regional Development Committee*, Kamati za Maendeleo.

Anasema, Kamati hizi za maendeleo zinaongozwa na mkuu *Regional Development Committee, Regional Commissioner, District Commissioner, Planning Officer, District Council, all members of parliament in the region,* Wajumbe wote wa Bunge, Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, Meya, *chairman* wa *town planning,* Mkurugenzi wa Manispaa, Karani wa Manispaa na *Head Officer,* wote watu wa Idara. Sasa hii ndio Kamati ya Maendeleo. Sheria imetungwa tangu mwaka 1998. Mimi huu ni mwaka 13, sheria hii inaniruhusu nialikwe, lakini niliwauliza wenzangu wengine wakanambia hakuna aliyealikwa. Sasa sheria hii kama imekuwa kibogoyo, wakati umefika Mhe. Waziri ipe meno ili iweze kufanya kazi. Kwa sababu kazi zake ukizisoma ni kazi muhimu sana.

Niliona jambo hili nilieleze, maendeleo haya. Nchi hii Mhe. Mwenyekiti, imejengwa kwa kujitolea. Walianza kujitolea watu tarehe 12, tukaendelea miaka 50 tukajenga Michenzani, tukajenga mabarabara, ndio, ni kujitolea, sasa turudishe moyo ule wa kujitolea pale ambapo panafaa kujitolea.

Mhe. Mwenyekiti, leo tunasema mji mchafu, sasa mji mchafu, nani afanye? Manispaa, manispaa hawezi kununua hata hiyo *slash*. Sasa sisi wenyewe nyumba zetu tunazoishi, sisi wenyewe mazingira tunayoishi tuanze kufanya usafi, inatia aibu. Ukitoka Uwanja wa Ndege mpaka ukifika Boznia sijui pale, huku na huku kuna majumba na yote yamejaa majani na yamejaa uchafu, isipokuwa nyumba ya Mhe. Ali Mzee Ali, hiyo ni aibu! *(Makofi)*

Mhe. Waziri, narudia tena tushirikiane, yale tunayoyaweza tuunde kikosi sisi cha Wawakilishi cha usafi, tizama nchi iliyojengwa, tujitolee mwezi mara moja tusafishe mji wetu, haya mambo ni muhimu tujenge nchi yetu, tusaidiane.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu mashirikiano; ambacho ni kitu muhimu sana. Marehemu Mzee Idrissa Abdul-Wakil alipokuwa analihutubia Baraza hili. Unajua Mhe. Mwenyekiti, hili Baraza lilianza mwaka 1980, tayari Baraza

hili sasa hivi lina miaka 34, lakini sio 34 ni miaka 50 kwa sababu lilianza la Baraza la Mapinduzi. Humu ndani Mhe. Haji Omar Kheri, Mhe. Ali Abdalla Ali na Mhe. Shawana Bukheti Hassan hawa waliingia mwaka 1995, waliowakuta wao wote leo humu ndani hawamo, Sisi tuliingia mwaka 2000 nusu yetu hawamo, lakini sisi tuna wajibu, ukiwa Mwakilishi ndani ukiwa nje basi tuna wajibu.

Mhe. Mwenyekiti, Wawakilishi sisi kasema Mzee Jumbe ni ngome ya wananchi na ni sauti ya wananchi, na mawaziri ni sehemu ya serikali, ni lazima tushirikiane. Anasema naomba nimnukuu kwa faida yetu sote, anasema hivi; Tarehe 22/01/1985 Mhe. Ali Hassan Mwinyi alilihutubia Baraza hili kwa kufafanua wajibu wa mwakilishi.

"Mimi napenda kutumia nafasi hii kuwakumbusha hasa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwanza kila Mwakilishi ndiye askari, kila Mwakilishi ni ngome. Wawakilishi wasingojee, wakiona jambo akangojea atapeleka swali. Amfuate Waziri, na waziri asimpuuze amsikilize". Sasa turejeshe hii *spirit*, tusingojee kuleta swali. Swali tulete, lakini jambo ukiliona nenda kamwambie waziri, waziri ukiambiwa sikiliza halafu fuatana naye.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwenye kamati yetu ya viongozi waliona kama mzaha, alisema wizara hii kubwa, Rais kama unanisikia, Dkt. Mwinyihaji mpelekee salamu, Rais wetu msikivu katekeleza ndio akafanya mabadiliko ya hii wizara kidogo kuipunguza na kufanya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Rais msikivu sana, na mawaziri wetu wasikivu hawana kiburi.

Mhe. Ali Abdalla Ali alikuwa waziri humu ndani kwenye wizara hii, leo tunaye huku tunashirikiana. Mhe. Haji Omar Kheri miaka 15 tulikuwa naye huku, leo kaingia mwenzetu huko. Sasa ukishakuwa huku usidhani ndio milele na maisha, hapana. Tunapeana peana tu huyu na huyu, huyu na huyu. Sote tuna jukumu la kujenga nchi hii, hizi ni kazi tunagawana tu basi.

Mimi ni mteuzi wa Rais, Mhe. Balozi ni mteuzi wa Rais, Mhe. Mohammed Aboud mteuzi wa Rais, Mhe. Omar Yussuf mteuzi wa Rais, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban mteuzi wa Rais, Mhe. Zaynab Mohammed mteuzi wa Rais, Mhe. Marina Joel Thomas ni mteuzi wa Rais, sisi tuko kumi; sote Rais katuteua. Wala Rais hajatupa mtihani tukafanya, kisha akatwambia wewe baki Mwakilishi na wewe kuwa waziri, hapana, ni mamlaka yake. Kwa hivyo, wale wateuzi wanane aliyowapa uwaziri ni mamlaka yake, na sisi huku sote tushirikiane tujenge nchi yetu, tujenge taifa letu hili, ili yapatikane maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena tushirikiane na ninaamini Mhe. Waziri kama tutashirikiana, basi mwezi Januari tukija hapa, tutaona maendeleo mengi, mambo mengi tumefanya. Kamati ile Teule ya Manispaa, ina Mheshimiwa Mnadhimu wa chama, ina Mheshimiwa Ismail Jussa, ina Mhe. Asha Bakari Makame. Tumesema mengi juu ya Manispaa, kaa nao tutamaliza. Kama nyengine *ZECO* na kwengineko. Sasa tukikaa pamoja tukashirikiana, sisi sote tuna wajibu wa kujenga taifa hili, na sisi sote tuna wajibu wa kufanya kazi kwa pamoja ili kujenga nchi yetu hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi niliona nitie ubani kwa hayo maneno machache. Lakini Mhe. Mwenyekiti, narudia tena tushirikiane, tupendane na tujenge nchi yetu, hizi kazi tunagawana tu. Kwa hivyo, yadumu Mapinduzi yetu, udumu Muungano wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wananiuliza hapa Wajumbe wenzangu Muungano wa serikali ngapi? Sera ya Chama cha Mapinduzi ni serikali mbili. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Makamu wa Pili wa Rais kwa kuongoza Baraza hili, pamoja na waziri wake. Nimpongeze Makamu wa Kwanza ambaye yuko nje ya Baraza hili. Lakini Makamu wa Pili wa Rais alitwambia hivi, tuache siasa za matusi, tuache siasa za ubaguzi. Kesho Mwenyezi Mungu akiniweka hai, Wizara ya Katiba na Sheria nitaomba tena nizungumze hayo niliyoyasema leo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sisi sote humu ndani tuna kiongozi wetu, na yeye ni Makamu wa Pili wa Rais; ndiye kiongozi wa Baraza hili humu ndani kwa mujibu wa Katiba.

Kifungu cha Katiba cha 43(5) kinasema hivi

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera ya serikali kwa ujumla, na mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais,watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar".

Sote tuliapa pale tukashika Katiba na tukashika msahafu, tutekeleze haya tuliyoapa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kukutakia wewe mafanikio na kheri, na naunga mkono na nawaomba Wajumbe wenzangu wote, tuichangie, tuichambuwe na hatimaye tuipitishe. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Mzee Ali na ndio maana tunakuita *professor* kwa sababu nafasi ya u-*professor* haipatikani ovyo. Kwa hivyo, tunakushukuru sana na ninafikiria muda ambao nimekuongezea una thamani yake ndani ya busara ambazo umezitoa. Tunakushukuru sana Mhe. Ali Mzee Ali *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na Mhe. Fatma Mbarouk Said, baadaye anafuata Mhe. Mohammed Haji Khalid, na baadaye ajitayarishe Mhe. Salma Mussa Bilali.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii. Vile vile na mimi nashukuru baada ya Mhe. Ali Mzee, kama alivyosema kwamba alipenda kupangwa baada ya yeye nikawa mimi. Hiyo ndio historia ilivyo; kwamba baada ya Sayyidna Ali anakuja Fatma, nashukuru kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niende moja kwa moja na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa vile idara hii ina majukumu makubwa. Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na kutathmini miradi, kuratibu na kusimamia uandaaji wa matukio ya sera, sheria na mambo mbali mbali kama inavyoonesha katika ukurasa namba 9.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa idara hii ina majukumu mengi na muhimu na ndio idara mama, ningeiomba serikali ikaliangalia hilo kwa kuipatia bajeti ambayo itakidhi mahitaji haya. Kwa upande wa idara yenyewe ihakikishe ile mipango ya maendeleo inakuwa endelevu na kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa zinatumika kama zinavyotakiwa, kwa kuzingatia thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma *VFM*, kwa jina jengine *Value for Money.*

Mhe. Mwenyekiti, na hili ni jukumu la kila taasisi kuhakikisha baada ya kuidhinishiwa bajeti zao, kinachofuata ni kuzitumia bajeti zao kwa mujibu wa vifungu kama walivyoviombea.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bajeti ni makisio basi ni vizuri kwanza kuandaa mpango kazi ambao utajipangia kwa mwaka huu nahitaji hiki na hiki chenye thamani hii. Mhe. Mwenyekiti, kuzitumia fedha hizi pia ni lazima kuwa na *procurement plan* ambayo ni *guideline* katika kuzitumia fedha hizi, kwa sheria ile namba 9 ya matumizi ya mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye hii Ofisi ya Vitambulisho na Usajili. Mhe. Mwenyekiti, ofisi ya usajili na kadi za utambulisho ni taasisi muhimu kwa serikali na pia kwa kila Mzanzibari mkaazi anapofika umri wa miaka 18 hii ni haki yake kupata kitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, mimi siamini kwamba ofisi hii inafanya makusudi kuwanyima wananchi vitambulisho, ikiwa ni moja ya utekelezaji wa kazi zake na kufanya kazi zake kwa uhakika. Kwa hivyo, tusiibebeshe lawama ofisi hii, tuanzie kwa Masheha, Sheha ndiye mtu wa mwanzo kwa masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze ofisi hii kwa kutunza taarifa za waliosajiliwa katika *database*. Mhe. Mwenyekiti, nimuulize Mhe. Waziri kwa mwaka 2013/2014 ni kiasi gani malengo yake aliyojipangia yametekelezeka kama kitabu chake kutoka ukurasa namba 16 hadi ukurasa namba 20.

Mhe. Mwenyekiti, niende ukurasa namba 55 wa kitabu hiki mpaka namba 58, ingawaje Mhe. Ali Mzee Ali ameshalizungumzia, kuhusu Idara Maalum za SMZ. Idara hii ina majukumu mengi na mazito. Moja ni kusimamia mwenendo wa kiutumishi, maslahi ya maofisa wapiganaji na kuwajengea uwezo wa kiutendaji na kuratibu masuala ya michezo ya pamoja ya idara maalum za SMZ na SMT.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wenzangu waliizungumzia idara hii maalum kwa jazba na kwa kuvitaka vikosi hivi viwe mbele kwenye sherehe za Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, mimi naona suala hili ni moja ya kero ambayo ni ya kikatiba, na kwa sababu vikosi hivi viliguswa katika moja ya Zanzibar kuvunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, ningewaomba Wajumbe wenzangu humu ndani huu ni wakati muafaka kwenda kuviingiza kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano. Rasimu ni mapendekezo tu, mule muna kasoro nyingi ambazo hata hiyo Tume wenyewe hawakuiangalia. Sisi tunaangalia mfumo wa serikali tu, hili halitusaidii, hili kama ni kero twendeni kwenye Bunge la Katiba kuna hoja ya wengi na pia wachache wanasikilizwa.

Mhe. Mwenyekiti, sio nia yangu kujibu hoja za Mhe. Waziri, lakini niseme kwamba nashangazwa sana na hata yale ya Wajumbe wa Tume ile kusema yaliyomo mule ndio yameshakuwa ndio maamuzi. Tunajadili ni sawa, lakini sio kuwa tusikosoe.

Mhe. Mwenyekiti, ile Rasimu kwenye hiyo serikali ya shirikisho iliyotajwa mule kuna kasoro nyingi tu. *CAG*, mule katajwa *CAG* mmoja tu ambaye atakuwa ni wa ile serikali moja ya Muungano, lakini shirikisho, zile nchi shirikishi hazikutajwa kabisa sijui kama zile nchi shirikishi zitakuwa na uwezo gani, au hesabu zake zitakaguliwa na nani. Mimi ninaloliona ni kwamba tukae, twende turudi Bungeni kwa sababu mna kasoro nyingi twende tukaziangalie na tuweze kupata katiba ambayo tunaitaka.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niende kwenye Jeshi la Kujenga Uchumi limeanzishwa kwa sheria namba 6 ya mwaka 2003 lina jukumu la kutoa mafunzo kwa vijana katika nyanja za kuimarisha uchumi kwa kupitia kilimo, mifugo, uvuvi, ufundi kazi za amali na mafunzo ya uzalendo na ulinzi wa nchi yao, dhana hii ni nzuri lakini naomba sana mafunzo ya amali ni mazuri kwa kuwapa vijana wote wanaoingia pale kwani ni kwa ajili ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe.
Serikali haiwezi kuajiri watu wote isipokuwa mafunzo ya uzalendo na ulinzi wa nchi iwe kwa wale ambao watakuwa na uhakika wa kuwaajiri kuwapa mafunzo ya upiganaji na baadae kuwaacha hili ni tatizo tena tatizo la kuwaacha kuranda mitaani bila ya kazi ni kuwafanya wajishirikishe kwenye vitendo vya kujihatarisha wao wenyewe na kuihatarisha jamii inayowazunguka.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ina majukumu mengi kupitia taasisi zake mbali mbali ukijumuisha mabaraza ya miji na mikoa yake pamoja na Halmashauri, mimi ni tofauti na wenzangu na kwa bahati Mwenyekiti wangu alinitangulia mimi ni mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, Halmashauri zinapokusanya zaidi itwambie ni kwa nini na inapopungua pia itueleze ni kwa nini, kwani inawezekana kuwa Halmashauri zikawa na uwezo zaidi lakini kwa sababu ya makisio madogo ambayo wamekisia. Mhe. Mwenyekiti hii sera ya kuanzishwa kwa Halmashauri na Serikali za Mitaa ni muhimu kwani lengo ni kuziletea maendeleo endelevu kupitia vianzio vya mapato, kama tutakuwa na kufuata misingi ya utawala bora na uwajibikaji na uwazi hizi Halmashauri zinaweza kujiletea maendeleo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ., baada ya hayo nakushukuru kwa kunipa wakati wako huu na kuchangia bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kueleza machache juu ya Wizara hii iliyoko mbele yetu, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kuwasilisha kwake kuzuri sana hotuba yake hii ya Makadirio na Makisio na Mapato ya Wizara yake, pamoja na watendaji wake bila ya taka ndio maana akaweza kwenda vizuri kama alivyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianzie na Afisi ya Usajili wa kadi za vitambulisho kabla sijaendea kwengine, miongoni mwa afisi muhimu katika Wizara hii ni hii inayohusika na vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi, Afisi hii ni muhimu na umuhimu wake ni kuwa inatoa vitambulisho vya kumtambulisha kuwa huyu ni Mzanzibari mkaazi na kumpatia haki nyengine zote pale ambapo Mzanzibari atakuwa kakosa kitambulisho hicho itakuwa bado Uzanzibari wake kisheria haujakamilika. Mhe. Mwenyekiti, dhana ya kuanzisha vitambulisho ni dhana kongwe sana huko nyuma miaka ya Mheshimiwa Rais wa Kwanza yeye hakuweka kitambulisho, lakini alitoa kadi ambazo aliziita kuwa ni kadi ya uraia hiyo ilikuwa na ukubwa huu, hii ni pasi ya uraia kwa wati huo ambayo hii ni ya kwangu mimi mwenyewe ndani yake mna kitu kinaitwa stakbadhi ambayo inaitwa Idara ya Uandikishaji Uraia na wakaazi, hii ina maana kuna watu walikuwa wanaitwa raia na kuna watu ilikuwa wanaitwa wakaazi.

Kwa wakati huo raia ni nani kwa wakati huo ni wale Wazanzibari wenyewe hao walikuwa wanaitwa raia wa Zanzibar na wakaazi ambao walikuwa wanapewa kitabu kama hichi lakini rangi nyengine wao walikuwa wanaitwa ni wakaazi wale ambao wamehamia Zanzibar kwa kukaa tu lakini si kwao hawa ndio walikuwa wakaazi. Kwa hivyo kulikuwa kuna tofauti raia wa Zanzibar na mkaazi wa Zanzibar, baadae dhana hii ikapotea tukawa tunakwenda tu hatujui kuwa raia, wakaazi au tuko nani.

Katika miaka ya 2000 dhana hii ikazuka tena kulizuka na kijitambulisho kidogo kama hichi ambacho hichi huku mbele ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini nyuma imeambiwa *This is to sulfides that the bear the of this card is a citizen of Zanzibar* yaani kwa wakati huo kitabu chao hiki hakikutambulikana kwa dira ya Wazanzibar lakini hichi hakikutumika, kwa sababu kilitolewa 2000 ili kutumika kwa uchaguzi kwa bahati mambo yakenda vyenginevyo kwa hivyo uraia huu ukafa hafla haukuwahi kufanya kazi yoyote.
Hatimae kikaja hiki kitambulisho cha Mzanzibari mkaazi ambacho ndio sasa tunatumia.

Sasa mimi ningeishauri au kuiomba Serikali pamoja na kwamba sheria ipo kuna tofauti iliyokuwepo zamani pawepo na raia wa Mzanzibar na Mkaazi wa Zanzibar sote tusiwe wakaazi tu hii ni nchi na nchi lazima iwe na raia na raia ndio sisi, tusiwe wakaazi tuwe raia wahiliki.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Idara hii na kutokana na Sheria iliyotungwa na Baraza hili la kutoa vitambulisho kwa Wazanzibari hii sheria kwa kima fulani ina mapungufu, ningeomba Wizara husika iweke sheria ya marekebisho ili kila aliyehusika kupata kitambulisho hiki cha ukaazi awe na haki ya kukipata, hasa kwa sababu pia kuna sheria kama mtu hanacho hichi na akikamatwa na akifunguliwa mashitaka anaweza kufungwa, sasa mtu asije akaingia kosani wakati ambao hana kosa lakini kuna chombo ndicho kilichomsababisha aingie katika kosa hilo. Sasa kwa sababu hii ni haki ni vyema kama hii sheria kidogo inabinya ifanyiwe marekebisho ili kila mmoja aweze kupata haki hiyo ya kuwa na kitambulisho cha ukaazi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kidogo katika Mamlaka ya Serikali za Mikoa na niingie katika Mkoa wangu wa Kusini Pemba, kuna kipande kidogo niyanukuu kutokana na utekelezaji wa majengo yao wanasema kuimarisha viwango vya taaluma kwa wafanyakazi saba kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, halafu kutekeleza malengo wamesema wafanyakazi sita wanaendelea na masomo. Nataka kujua wafanyakazi hawa sita ni wangapi wapo nje ya nchi masomo yao na ni wangapi wanaume na wangapi wanawake.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya Mkoa wa Kusini Pemba imeeleza kwamba kulitokea upepo na mvua kubwa ambayo imeleta maafa katika Mkoa wa Kusini Pemba, nyumba kadhaa karibu nyumba 175 ziliathirika lakini 52 ziliathirika vibaya sana, ningeomba kujua nyumba hizi zimeenea katika maeneo yepi na yepi, na pia Mkoa baada yakufanya utafiti na kujua athari zilizopatikana na kufanya tathmini ya fedha inayohitajika Serikali imesaidia vipi zile koo au zile nyumba ambazo zimeharibika vibaya, Je serikali ya Mkoa ina mchango wowote iliyotoa, na je nyumba hizo ziko katika maeneo yepi na yepi.

Kadhalika kuna vipando vilivyoharibika karibu ekari 194 za mazao mbali mbali kwanza nitoe pole kwa wote walioharibikiwa na nyumba zao na vipando vyao nawatakia kuwa na subira ili waendelee na maisha katika hali iliyopo hivi sasa, kwa kuwa kuna mazao yaliathirika nataka nijua kama Mkoa umechukua hatua gani angalau ya kuwasaidia hawa ambao wamepata athari katika mazao yao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara Maalum mimi sitaki niseme mengi kuhusu idara hii kwa sababu mengi na mazuri tayari yamesemwa na mwenzangu nami sitaki nijibu hoja, lakini mchangiaji mwenzangu mmoja alifarijika kusema kwamba kuna watu ambao ni wapinzani kuwa wanaviunga mkono vikosi, katika wakati huu kama sikosei katika baraza hili hakuna mpizani kwa muundo wa sasa sote tunakwenda pamoja, pengine hao wanaotoa upinzani ni wapinzani wa Serikali sote *back benchers* pale Serikali ilipofanya vibaya tutaiandama na kama itafanya vibaya tutaifuta. Lakini hapa kwa kweli nadhani hakuna mpinzani na kama angekuwa yupo angeleta huo upinzani .

Mhe. Mwenyekiti, nimesema juu ya hii Idara Maalum katika malengo yao kulikuwa na kuendelea na ujenzi wa Chuo kipya cha Mafunzo cha Hanyegwamchana ambapo Mhe. Waziri alisema kifungu hiki kiondolewe. Mhe. Mwenyekiti kile Chuo tayari kimetumia pesa nyingi na dhana ya kukiendeleza ilikuwa ni dhana nzuri, sasa ningeomba kama Mhe. Waziri ana sababu kubwa na nzuri ya kuona kuwa ujenzi usiendelee katika awamu hii ningeomba nizijue, kwa sababu mimi wakati nikiwa Katika Kamati ya Viongozi wakuu katika awamu iliyopita

tulitembelea mradi ule tukauwona na baada ya kupata maelezo ya makamanda tulitumia lugha fulani hivi, mradi huu hautomaliza hadi kiyama.

Sasa leo Mhe. Waziri anaungana na mimi kwa sababu huu mradi unaendelea na kujengwa leo kwa sababu moja au nyengine kwa kipindi hiki umesimamishwa usiendelee. Sasa fedha ambayo kikosi hiki imetumia ni fedha nyingi ya OC alikuwa anajikamua anabana matumizi mengine ili aendeleze ule mradi leo umepigwa stop katika kipindi hiki, pengine ipo sababu ya msingi ikiwezekana hiyo sababu na mimi nikaijua itakuwa ni vyema lakini mimi sijaona mradi huu kusimamishwa wakati ambapo ni mradi mkubwa na ungeweza kuweka wanafunzi watoto mbali, wanawake mbali, na kadhalika pindipo pale ukikamilika. Kwa hivyo kusimamishwa kwake pamoja na kwamba mimi nilikuwa naona kuwa haumaliki lakini kusimamishwa na Serikali sikuona vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mji wetu wa Unguja yaani kwenye Manispaa, na mimi nitaanzia kwenye hizi packing za magari na vituo ambavyo vimesambaa mji mzima, baadhi ya wakati unapojaribu kuondoa tatizo mara nyengine huwa una *create* tatizo jengine kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, kama mimi kuna mtu ananidai hapa barabara na akanishika koo lazima utanilipa, baadae na mimi nikaenda kumsikitikia Mhe. Abubakar akanipa pesa nikalipa yule aliyenikamata koo ataniwachia lakini bado tatizo ninalo kwa sababu gani nimeweka deni pahala pengine, ndio hivyo hivyo ilivyofanya Wizara hii imeondoa msongamano pale Darajani na hatimae imegeuzwa kuwa packing ya gari binafsi, lakini wameongeza msongomano, tafrani kwa magari na watu katika maeneo kadhaa, kuna kundi lipo uwanja wa Malindi, kuna kundi moja lipo Baraza la Wawakilihi, kundi jengine Afisi Kuu ya CCM pale ni vurugu moja kwa moja, hatujui lengo la kufanya hivi ni lipi tumechukua hatua bila ya kujitayarisha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, pamoja na msongamano huo pia sasa unazidishwa kwa mfano gari ambazo zamani zinapaki pale Kikwajuni Baraza la Wawakilishi la zamani zinapoondoka kuchukua abiria zinapita njia ya hospitali huku inakwenda zake moja kwa moja, sasa zinaambiwa kule zisipite tena lazima zizunguruke huku Kisiwa Ndui ambako kuna msongamano mkubwa sana na gari inayokwenda Chukani inapoondoka ghalabu haina mtu wa kuteremka Kisonge wala Kariyakoo, aghalabu inapoondoka lakini ikiondoka Chukwani kuja Mjini inakuwa na watu wanaoshuka Kisonge, Kariakoo na kwengineko, sasa kuifanya gari kuwa isipite njia ya hospitali lazima ipite huku ni kuongeza msongamano ambao hauna haja yoyote.

Sasa kama lengo ni kutoa huduma nzuri hapa Mhe. Mwenyekiti tunatoa huduma mbaya na tunaongeza msongamano ambao hauna haja yoyote. Mara nyingi Mhe. Mwenyekiti, mimi huwa ninasema unaposafiri kutoka ama Pemba au popote sana penginepo ukianza kusikia harufu mbovu jua tayari umefika mji wa Zanzibar kwa taka ambazo na nyengine zinarundikana kwa jaa ambalo limewekwa pale mjini. Kazi kubwa inafanywa na Manispaa lakini kulingana na wingi wa taka zinazozalishwa, nadhani bado uwezo wao wa kusafisha mji ni mdogo.

Mara nyengine Mhe. Mwenyekiti, kuwaona wale wanawake wanaosafisha hata zana za kuzolea taka hawana wanakuwa na maboksi mabovu mabovu mikono iliyo wazi haina kinga yoyote wanakusanya taka kwa mikono, kwa kweli si jambo zuri kwa sababu zile ni taka na ni chafu na wale ni watu sina hakika kwa watu wanaofanya kazi hizi ngumu na nzito kuwa wanaangaliwa afya zao na taasisi husika. Kwa sababu kazi wanazofanya ni ngumu na ni ya hatari ni vyema iwe kila kipindi watu hawa wanaangaliwa afya zao.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii pamoja na kuwa

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Haya, pamoja na kuwa ukusanyaji wao wamedai kuwa makusanyo ni madogo lakini kimtazamo hawa wanakusanya mapato mengi sana, kwa sababu kila kipembe, kila kona, kila palipokaa sawa wakijiona kijigari kime-*park* bila shaka lazima itachangia. Wanaouza biashara za kila aina wanatoa michango yao. Sina hakika kuwa kila kinachokusanywa kinafika kulikokusudiwa au la, lakini makusanyo ni mengi na makubwa tena ya kila siku hasa kuonesha katika kitabu hiki kuwa hawakufikia lengo kwa kweli sijui kwa sababu gani. Kwa sababu vyanzo vyao vya mapato wanavitumia vizuri sana, sana, sana. Ama kama vinafika kulikokusudiwa au havifiki ni suala jengine lakini Baraza la Manispaa linakusanya mapato tena bila ya uzembe, bila muhali na mara nyengine kuna watu wanavunja sheria. Wanafanya biashara mwahala ambamo hamukubaliki lakini na serikali nayo inaungana na wao kuvunja sheria. Kwa sababu inawanyang'anya bidhaa zao kuwanyang'anya ni kuwaibia, sasa kuvunja sheria serikali isichukuwe sheria mikononi mwake kwa sababu kaweka hapa ndio mitumba yake aibebe,

tungule zake azibebe ende nazo wapi? Je zile baadae Manispaa wanaziuza, wanazitupa mali ile wanayoiteka wanafanyaje?

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa wamevunja sheria lakini walionyang'anya na kuchukua mali yao nao pia wamevunja sheria zaidi vile vile. Lakini wao hawana pa kwenda waende wapi serikali ndio iliyowanyang'anya kubwa wanalofanya ni kwenda mbio watu wakachukua wanachochukua, cha kugawana wakagawana si hakika mali kama ile wanaifanyaje. Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba Waziri anijibu ile mali ambayo inaporwa baada ya mtu kuvunja sheria inaishia wapi. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wachangiaji waliobakia ni sita na muda uliobakia kwa kweli hatutoweza kugawana dakika ishirini, ishirini kila mmoja wetu. Na tunatarajia kesho tukijaaliwa tunamaliza Wizara hii. Sasa nilikuwa naomba sana wale ambao watahisi kwamba wanataka kuchangia kitu kimoja, kwa sababu tumekuwa tunachangia mambo hayo kwa hayo. Kwa hivyo mimi naona sasa ile michango mingi imeshajitosheleza, sasa wale ambao wanahisi kuna jambo muhimu tu anataka kulisisitiza au kulizungumza ningeomba michango hiyo ielekee huko zaidi.

Kwa hivyo wanaofuata ni Mhe. Salma Bilal, Mhe. Raya Suleiman, Mhe. Jaku Hashim na baadae atafuatia Mhe. Amina Idd Mabrouk.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii kuweza kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu na kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Mwenyekiti, pia nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kuwa kuweza kutuwasilishia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nianze Mkoa wa Kusini Unguja. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini pamoja na watendaji wake kwa mashirikiano yao makubwa na wananchi wao katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi katika Mkoa huu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nimuombe Mhe. Waziri katika kasma za Mkoa wa Kusini Unguja aongezee kasma hiyo kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Mkoa wa Kusini una tatizo kubwa la usafiri wa watumishi katika Mkoa. Mhe. Mwenyekiti jografia ya Mkoa wa Kusini nadhani unaielewa, Ofisi ya Mkoa kwa sasa hivi imehamia Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, kuna watumishi ambao wanatokea Kiboje, mtumishi huyu hana usafiri anatoka Kiboje anakuja mpaka Kidimni aende mpaka jumba lamazwe atafute usafiri mwengine aende mpaka Tunguu pale penye *junction.* Atoke Tunguu pale atafute usafiri mwengine mpaka afike Tunguu Ofisini hata akifika ufanisi wa utendaji unakuwa sio mzuri. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri afanye juhudi za makusudi uwaongezee kasma ili angalau waweze kutafuta usafiri wa kusaidia watumishi wao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa kuwa linatoka Mkoa wa Kusini nalo nitalisema ni tatizo japo lina Wizara yake lakini nitalizungumza kidogo. Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine ni la uhaba wa fedha za misaada kwa wazee wa Mkoa Kusini Unguja. Msaada wa wazee hadi leo ni shilingi elfu tano, elfu tano haimsaidii mzee isipokuwa inamzidishia mashaka. Kwa sababu hiyo elfu tano ataikopea ukifika mwisho wa mwezi kwanza haipati kwa wakati halafu yaani inamchanganya kwa kweli naomba Mhe. Waziri waongezewe angalau ifike elfu hamsini nadhani zinaweza zikawasaidia. Ninajua tatizo hili ni la Mikoa yote lakini kila mmoja analia mama yangu kwa hivyo mimi nawasemea wazee wa Mkoa wa Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, umesema tusizungumze yaliyosemwa lakini hatuwezi lazima tuzungumze haya haya kwa sababu haya ndio yaliyokuwemo kwenye kitabu kwa hivyo lazima tuyachangie.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Ofisi ya Usajili wa Kadi za Utambulisho. Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimpongeze kwa dhati kabisa Mkurugenzi kwa jitihada zake za kuondoa malalamiko ya upatikanaji wa vitambulisho hivi. Lakini bado mimi ninahisi bado iko haja ya ofisi hii kutoa elimu ya ziada kwa wananchi na viongozi kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa vitambulisho hivi. Mhe. Mwenyekiti nasema hivyo kwa sababu gani? Ninasema hivyo kwa sababu sheria ya upatikanaji wa kadi za utambulisho imepitishwa katika hili Baraza lako Tukufu na kuweka utaratibu mzuri wa upatikanaji. Lakini sasa hadi leo tunapoona wenzetu bado wanalalamikia upatikanaji wa vitambulisho hivi na utaratibu wameupanga wenyewe na umepitishwa hapa lakini bado wanalalamika sielewi ni kwa nini? Cha kushangaza zaidi ni kwamba bado katika Wilaya zetu kuna mrundikano wa vitambulisho bado havijachukuliwa,

halafu tunalalamika vitambulisho havipatikani. Kwa hivyo ndio maana ninasema Mhe. Mwenyekiti, itolewe elimu ya ziada wananchi waelimishwe lakini na viongozi pia tuelimishwe tuwahimize wananchi wetu wakavichukuwe hivyo vitambulisho visirundikane pale, pale havina kazi, kazi tunazo sisi wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo niende Idara ya Maalum ya SMZ. Pia na mimi niipongeze tena kwa dhati Idara Maalum kwa ujumla wake kwa juhudi zao kubwa wanazochukua katika utekelezaji wa majukumu yao bila ya kujali changamoto mbali mbali ambazo zinazowakabili.

Mhe. Mwenyekiti, ombi langu kwa Mhe. Waziri. Mhe. Waziri naomba kwa unyenyekevu sana uangalie vizuri Idara hizi kimaslahi stahiki kutokana na uzito wa kazi zao. Pia naomba katika changamoto ambazo kubwa zinazowakabili licha ya maslahi ya kipato lakini pia na makaazi yao hayafai kabisa kwa maisha ya binaadamu. Nadhani ulipopata nafasi hii ya Uwaziri ulitembelea mote uliyaona makazi ya wafanyakazi wetu hawa. Ulipotembea nadhani Kengeja uliyaona makaazi ya magereza hali zao mbaya, kama walivyozungumza wenzangu humo ndani unaziona nyota juu usiku. Kwa hivyo naomba sana uwaboreshee makazi yao vijana wetu hawa.

Pia Mhe. Mwenyekiti, namuomba Waziri atakapokuja kutoa majumuisho yake nataka unieleze ujenzi wa gereza la Hanyegwa mchana umefikia wapi na hatua gani umezipanga katika ukamilishaji wa gereza hilo. Mhe. Waziri utakapokuja kutoa majumuisho naomba uniambie hilo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa kama ulivyosema tuchangie kidogo kidogo ninajali wakati wako, namuomba Mhe. Waziri achukuwe juhudi za makusudi kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi. Kikosi hiki nacho kiko hali mbaya, magari machache halafu mabovu spare hayana na spare zenyewe hapa pia hazipatikani. Kama alivyosema Mhe. Salma alisema kwamba gari za Zimamoto hata likifika kwenye Zimamoto halizimi isipokuwa linakwenda kushuhudia jivu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aliangalie kwa jicho la huruma Idara hii ili wapatiwe vifaa vya kuweza kuhudumia wananchi na kuokoa mali za wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba vijana wetu wa KMKM nao pia wanahitaji wapatiwe utaalam wa ziada na vifaa vya kisasa kwa kushughulikia shughuli zao. Pia vijana wetu wa JKU nao halkadhalika wanafanya kazi zao nzuri za uchongaji lakini wanafanya kwa uzoefu tu hawana vifaa vya kisasa wala hawana vifraa bora. Naomba nao pia waboreshewe ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa naomba kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini na mimi mwenyewe binafsi naunga mkono hoja asilimia mia moja. Mhe. Mwenyekiti, nimekatisha kwa sababu najali sana muda wako kuna mengi. Ahsante.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu na ninakushukuru vile vile na mimi kwa kunipa angalau dakika tano tu kwa sababu mengi yameshazungumzwa na mimi nizungumze tu machache vidokezo dokezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Waziri na watendaji wake na vile vile na wafanyakazi wote ninawapongeza lakini nitakuwa na machache kidogo ya kuzungumza katika Manispaa zetu na nitaanzia Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nizungumze habari ya kujenga soko Chake Chake na *parking* za magari. Mimi ninafahamu 2009 tupo Baraza la Kikwajuni nilichngia na alikuwa ni Mhe. Nyanga na nikamuuliza utatujengea wapi hizi *parking* za magari akanambia Mava ya Mbaruk. Nikamuuliza Mava ya Mbaruk Mheshimiwa unapajua? Nikafanya kama ubishi akacheka Mhe. Spika. Maana ninamwambia upande huu huku yako mava upande huu naona kuna bonde kubwa sana, je huyo mfadhili ushakuwa nae wa kuweza kwenda kutuchawanyia pale ikaweza kuwa pale ndio *park* za magari? Akasema tayari lakini yeye mwenyewe alishindwa kueleza kwa sababu pale pahali alikuwa Mhe. Nyanga hapajui vizuri.

Sasa nataka niulize je ujenzi ule wa *park* za magari Chake Chake kwa pale imefikila vipi Mhe. Waziri akija hapa ataweza kutueleza. Kwa sababu mimi nilipokuja zungumza niliambiwa pale ndio panataka pajengwe kwa ajili mji uko Chake Chake lakini vitu vitateremkia pale watu wende kule. Mimi ninajua pasimamapo magari lazima na soko liwepo. Sasa atakuja kutueleza Mhe. Waziri kuwa yeye pale patakuwa na *stand* za magari, patakuwa na soko au soko litajengwa wapi mimi nikawahi kuzungumza nikasema, kwa nini wakati ule ilikuwa Gongomawe bado hakujaa

majumba kuna sehemu kubwa sana, nikasema kwa nini ile *stand* haiendi kule ni mbali sana na maji. Lakini sasa kule ilikuwa ni rahisi sana kwa uwanda wake ulivyo ulivyo kuliko hapo mava ya Mbaruk kwa kujenga, hivi sasa hivi hakupatikani tena kwa sababu Gongomawe hivi sasa ni mji chanjaa lile lote lishakatwa viwanja na watu sasa hivi wanajenga tutakuja pata maelezo baadae Mheshimiwa akitueleza.

Halafu katika miji dhamana sijui kuwa ni Manispaa lakini naona ni Manispaa ndio wenye dhamana ya jiji. Kwa nini miji ikawa *zebra cross* hamna, mnapita watu mbali mbali na mule lazima mna magari lazima gari zisimame watu wapate kupita tukiwemo walemavu na watu wengine hata watoto. Zikiwekwa pale panawekwa mfano wanaandika kwa chaki hawaeki kitu kinachokaa stahiki kikadumu ukipita mwenye kiatu cha raba akipita keshafuta. Tunaomba Mhe. Waziri hili alione na vile vile atupe jawabu, maana mara moja nilichangia hapa hapa jamani *zebra cross* katika miji muna watu wengi wanapita, hizi sheria ziko pahala gani? Ziko Mawasiliano au ziko kwa hawa. Ikiwa ziko kwa hawa kwa nini hawasimamii? Ina gharama gani na inataka pesa kiasi gani yakuwa hawawezi kuziweka alama kama zile.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, nikija katika vikosi nitazungumzia JKU. JKU ilikuwa ni kikosi cha kujenga uchumi na watoto wetu wote wa hirimu zangu mimi watoto wangu niliozaa wamepitia. Kule sisi tukitumia Msaani pamoja na bonde lile ukijia Vikunguni Kwapweza, lakini naona kabisa maendeleo yale yameondoka, na pale Kwapweza pakilimwa na kuzalishwa vitu mbali mbali; vitunguu, mbatata, na mpunga kwa wingi lakini hatujui yale mabonde kama wamerudishiwa wananchi au yako katika mikono ya serikali.

Sasa naomba wawezeshwe watu hawa ili kuweza kusonga mbele wale watoto tunaowapeleka pale kuweza kuifanya ile kazi na kuweza kuibuka na uchumi mzuri katika nchi yetu. Tulikuwa tukijitahidi sana kwa miaka hiyo watoto waliokuwa wakienda JKU nafikiri chakula kilichokuwa kikizalishwa Msaani na pale kilikuwa ni kingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, halafu askari hawa hawa wanajituma masaa 24 hawana *over time*. Tumeshapita na mimi nishakwenda, kipindi kimoja nimekwenda mimi na Mwenyekiti wangu alikuwa ni Mhe. Abass Juma Muhunzi, tukawahoji hawa hawana *over time* na mpaka sasa hivi hawana.

Halafu hawa hawa JKU askari hawa walipelekwa *ZSSF* tukakaa kama muda mdogo tukasikia kwamba wameondolewa kwenye *ZSSF* kwa sababu gani na hawa ni wafanyakazi kama wafanyakazi wengine. Kwa sababu haya mapato yao na wao ni kidogo kidogo watakapokuja kustaafu pale ndiyo watapata zile stahiki zao, serikali itawapa kidogo na pale watapata ili ziweze kuwaendesha. Mhe. Mwenyekiti, ndiyo ukaona wakistaafu; maaskari kwa muda wa miaka mitatu ni masikini humtamani hata ukamuona hapo njiani, hujui kama mtu huyu alikuwa ni askari akiitumikia nchi hii.

Tunaomba vikosi vyote vya SMZ wapate stahiki zao, wapate posho zao ikiwa wanajituma kwa kweli kweli *over time* wapewe, kwa sababu muda wa kufanya kazi ni kuanzia asubuhi mpaka saa tisa, hawa wanalala kazini, na siku waliokuwa wana mafunzo ndiyo kabisa atafika hata siku mbili afande huyu kwake hajarudi yuko kule kule anafanya kazi ya serikali, anafanya kazi ya kulinda wananchi na mali zao na mengi mengineyo. Kwa hiyo, tunaiomba serikali ione na Wizara ya Fedha isiwe na ugumu kuzizidisha bajeti zao wakaweza kupata mafao ya kuweza kuwafaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nizungumze mengi kwa sababu yameshazungumzwa na ni haya haya tunayoyapitia, nilikuwa na haya kidogo nilitaka tu niyazungumze.
Mhe. Mwenyekiti, stahiki hizi za askari hazina viwango, askari anayefanya kazi miaka 30 mpaka 35 ukiuona mshahara wake na huyu aliyeingia kwa miaka kumi hawajapishana mbali. Tunasema vikosi vya SMZ vitupiwe jicho sana kwa sababu hawa ndiyo askari tuliowategemea. Halafu wale watoto wanaokwenda pale kupewa mafunzo wapo wanajitolea itakapofika siku za kutoa ajira siyo mtoto wa Raya Suleiman Hamad amekaa pale miaka miwili aje mtoto wa Mhe. Fatma akae siku moja apewe kazi.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri hilo nalo alione na aweze kutusaidia katika kufanya kazi hizo, kwa sababu watoto wanasikitika sana wanaenda wanafanyishwa kazi wanakaa pale miaka miwili, lakini ikifika kuchukuliwa ajira watoto wale wanatupwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa na mjukuu wangu ilifika kwamba watu wameshachukuliwa kwenda kupimwa aliambiwa kama hana shilingi 400,000/= basi hachukuliwi, na akanipigia simu. Mimi nikamwambia sitoi ikiwa umeshachoka rudi, nilimjibu hivyo hivyo sitoi shilingi 400,000/= ikiwa umeshachoka rudi umeshajitolea mwaka

mmoja na nusu imefika siku za kwenda ikiwa wenzako wameshakuja kuchukuliwa kupimwa hukupata basi pumzika. Na mtoto akawa ana moyo wa kujenga Taifa kwa nchi hii, kwa sababu ni pao hawezi kuacha, lakini kwa nini tufanyiwe mambo kama hayo. Kwa hivyo, tunaomba majina ya watu hawa wasichukuliwe wakapewa watu wengine, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mimi nikikupa mifano imeshanifika hiyo mifano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mtoto wangu amekwenda kupima Jeshi na akapasi na alipokwishapasi siku ile ya kozi ya mwisho wanataka kuchukuliwa basi walitoka vijana Unguja nafasi ile ya Gombani ikachukuliwa akapewa mtoto wa Unguja na mtoto wangu akarudi. Mhe. Mwenyekiti, aliniambia hutaki kunituma chochote mimi nahama nitatafuta pahala niende, nikatafuta pahali niende kuuza japo machungwa, sitokaa mkitutupa hapa ikawa sisi hatupati kazi. Kwa kweli niliona uchungu na si wangu tu hata wa ndugu yangu yameshamfika hivyo hivyo. Sasa naomba serikali iwe makini sana kwa watoto waliokuwa wana fani na wakawa wamepata wasiwavunje moyo, kwa sababu hawa watoto tunawategemea kwa mambo mengi sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi naomba katika bajeti hii itakapopita Mhe. Waziri tunamuamini ni kijana, ni mtoto na penye nguvu kazi ukimpa mtoto unaamini kuwa yeye atafanya ile kazi, tunamuamini sana Mhe. Haji Omar Kheri aweze kututekelezea zile sifa tunazozitaka tusipate kuhangaika.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na naiunga mkono bajeti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wakati Mjumbe anapozungumza msimkere, kwa sababu anatakiwa azungumze na Kiti na siyo na nyinyi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nitakuwa si mwingi wa fadhila kama sikukushukuru wewe Mwenyekiti uliyeniruhusu kuchangia Wizara hii.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa jumla kwa kujituma kwao. Shukurani za dhati kabisa zimfikie Mkurugenzi wa Manispaa kwa jitihada anazozichukua, na sisi wengi humu tumekuwa mashahidi, ikiwemo kuongezeka kwa mapato. Na muda mfupi tu alipoanza kuiboresha bustani ya Gofu pale katika kiwanja cha Mnazi Mmoja, hongera sana Mkurungenzi wa Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka nianze na huduma za jamii kituo cha daladala cha Darajani. Mhe. Mwenyekiti, serikali hii isingekuwa madarakani bila ya kuwepo wananchi, wananchi wana haki zao na zinatakiwa kuheshimiwa.

Nafikiri tungebaki sisi Waheshimiwa tu humu sijui tungeongoza nini bila ya kuwa na wananchi na haya mbele tutakwenda kuyakuta na sisi ndio wasemaji wao, kituo hichi kwa masikitiko makubwa sana na kinanitia huzuni sana kimeondoshwa pale sijui kwa mazingira gani na sijui kama utaratibu umetolewa wa elimu kwa wananchi pale kufahamu kwamba kile kituo kinaondoshwa wanapelekwa pahali, huwezi kumuondosha mtu bila ya kumuonesha pengine pa kumuweka. Leo watu wanateseka kwenda hospitali, na cha kutia uchungu zaidi mimi leo asubuhi nimelia kwa sababu ya wananchi, wameondosha kituo leo kuna gari zimewekwa pale, tunafanya nini? Ni kitu cha masikitiko makubwa sana. Maana yake pangekuwa patupu, lakini tumeondosha tunakuja kuweka kitu chengine. Leo mwananchi katoka Pemba anaitafuta daladala kuja pale gari haikuti; ana watoto sita au wanne *mashaallah*, tunawafanyia haki wananchi kweli?

Mhe. Haji Omar Kheri hili nafikiri ukae tulizingatie, leo imekuja kuhamishwa katika Afisi ya Chama kikubwa kuliko vyama vyote Tanzania, chama kisikivu chenye ilani za Chama cha Mapinduzi hapa hatujaisoma humu.

Kwa hivyo mimi bado nataka kuelimishwa mpaka niweze kufahamu kituo kile kwa misingi gani leo anafuata Kiongozi Mkuu Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe shahidi umechangia suala hili kweli ndio kituo pale wanafunzi watasoma tumeshuhudia Skuli za Vikokotoni na Darajani bughudha zilizotokea, Mkurugenzi aliyepita kafanya jitihada pale pamekaa sawa *alhamdulillah* jambo la kushukuru, wananchi wamekosa nini kuhamishwa kituo kile halafu kituo kipo mbele ya skuli mbele ya Ofisi za Chama; jambo la kusikitisha hili tutaenda kuulizwa mbele ya safari kwa Mwenyezi Mungu, tunawafanyia haki wananchi, kweli hili?

Mhe. Mwenyekiti, juzi tunauliza swali hapa sipo nilipata mtihani siku ya Ijumaa naomba kwa ruhusa yako nilisome.

Kumekuwepo na msongamano mkubwa wa magari ya watu katika eneo la Bandari ya abiria ya Malindi unaosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi hasa wanaopita ofisini nyakati za jioni; kwa kuwa ni kawaida kwa serikali kama ilivyowahi kusema na mawaziri humu Barazani huyafunga maeneo ambayo husababisha msongamano kwa magari kama vile Darajani na Forodha Mchanga.

a) Kwa nini eneo hili la bandari Malindi limekuwa likiachwa msongamano uendelee.

b) Hatua gani za dharura kwa muda mrefu zilichukuliwa zilizosababisha msongamano ambao unasababisha wafanyakazi wengi wa Serikali, hili swali liliulizwa kwa niaba yangu na Mhe. Saleh Nassor.

Mhe. Mwenyekiti, leo utamaduni gani huu; kumewekwa makalbi maana yake ni kitu ambacho hata kichwani hakiingii, njia yenyewe ni nyembamba, leo imekuwa na msongamano keshokutwa pengine bandari inataka kuvunjwa kwa kutokutosha bandari ile. Hilo Mhe. Waziri linazungumzika, basi ndiyo utaalamu, wewe Mhe. Haji umetembea umekwenda Ulaya umekuta makalbi kama vile kuwekwa kwenye njia? Maana yake baada ya msongamano bado tunaongeza msongamano mwingine, itakuwa tunapiga kelele kama kuuza minazi siku zote humu ndani hatusikilizwi chochote tunachosema.

Mhe. Mwenyekiti, msongamano uliokuwepo pale na bado umechukua makalbi, kalbi lina karibu mita mbili umeweka pale kwa sababu gani? Ndani mule muna mabanda yanataka kuvunjwa mengine kwa kuwa hayakidhi nafasi. Nimeuliza swali hili leo ya nne au ya tano nikafikiri litachukuliwa hatua, basi hamna hata zebra mkaweka alama ya chaki.

Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Waziri hili linazungumzika tusije tukafika pahali tukaanza kupigana mabuti yaliyokuwa hayana maana, ukayaondoshe makalbi kwa heshima na taadhima, ndugu yangu nikuombe jambo hilo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, wananchi vile vile narudia tena wana haki, mimi niombe sana wale wauza mikate wanaochangia shilingi 1000 jamani wale mkate faida yake ni shilingi ngapi? Halafu tunakwenda kuwakera wakati mwengine wakati faida ya mkate ni shilingi tano, wale watu wana watoto na wengine wana wake wawili, watoto wanataka mabuku na penseli. Mimi sifikiri hoja serikali wazingatie hayo. Serikali imeshapoteza kodi ngapi watu wakapewa msamaha wa ushuru, wale ni binadamu nao hawakutaka hali ile kukaa na masusu kwenda kutarazaki kule kila mmoja alikuwa anahitaji utajiri lakini ni kazi ya Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, nije na suala la vikosi vyetu vya KMKM. Suala hili wengi watu wamechangia hata Mhe. Haji nafikiri ulifikirie vile vile. Hawa wana kawaida, kama ni kweli miaka mitatu hupewa likizo wakapewa shilingi 1000, leo hakuna shilingi 1000 hakuna elfu 20, 000 wala hakuna elfu 10,000. Mhe. Mwenyekiti, hawa ndiyo wanaofanya kazi ngumu, likizo yao hakuna chochote kinachopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakuwa mkaidi zaidi sasa hivi kuhusu suala la Gongoni, hapa sitosikia lolote humu nafikiri nimeshaandika swali na majibu, mtaro ulianzia *Wireless* mpaka kwenda Gongoni; ule mtaro ni hatari kwa wananchi hivi sasa unafuka maji machafu, mbu watupu. Kwa suala hili mimi humu ndani nitakuwa mkaidi kwa wananchi wa Gongoni, mtaro ule ukakae ukautizame Mhe. Haji kama ndiyo utaratibu ushakumbuka na usiku ni hatari, leo miaka mitano mpaka kumi tunawafanyia haki kweli wananchi wale wa Gongoni? Mhe. Mwenyekiti, kuanzia kule mpaka mwisho kumefumuka, hata vile vikalbi vya kufunikia havipo kabisa. Suala hili Mheshimiwa nitakuwa mkaidi sana humu ndani naanza kutangaza mapema kwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mitaro mengine hii ya Mombasa nao tumeshuhudia ng'ombe akivunja miguu kila siku, mtaro wa Mombasa kwenye maduka ya *Supermarket* mitaa ile hili suala nalo liangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, nije na suala hili la soko la samaki Malindi bado haliridhishi hata kidogo. Mhe. Haji ningekuomba kuna siku ungekwenda kuangalia hilo soko la samaki juu ya utamu wake basi utashindwa kununua mule ndani na ni kitu kidogo; ni *floor* mifuko 20 nafikiri haifiki hapa. Leo ni miaka mingapi na wale wanachangia siyo hisani wanayofanyiwa wale wauza samaki, wale wanachangishwa pesa hawakupewa bure pale, ile hali hairidhishi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, soko la mboga mboga nalo niliuliza swali juzi Mhe. Haji nalo ukaliangalie Mhe. Waziri haya mengine yanazungumzika, haliridhishi mvua zote zile miaka karibu 30 kipaa hata milioni nane hakifiki nacho. Haya ndiyo mambo ya kuzingatia ya wananchi…

Mhe. Mwenyekiti, jengine la mwisho kabisa gari ya Mstahiki Meya ile gari sifikiri kama inaendana na hadhi yake, gari anayotumia Mhe. Meya. Meya ni mtu mkubwa, hiki ni kitu cha kusikitisha sana. Mhe. Mwenyekiti, baada ya haya machache namsubiri Mhe. Waziri atakaponijibu hoja zangu tumalizane.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi jioni ya leo kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Awali ya yote kwanza nichukue fursa hii kwa dhati kabisa kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti kwa kazi nzuri unayoifanya leo hii kuanzia asubuhi hadi jioni, hongera sana. Nakupa hongera hizi kwa sababu ni mwanamke mwenzangu, kwa hiyo nataka kukuhakikishia kwamba kina mama tunaweza bila ya kuwezeshwa. Baada ya pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti nianze mchango wangu katika ofisi ya usajili na vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii ya dhati kabisa kuipongeza idara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti sote ni mashuhuda katika kikao hiki malalamiko yamepungua tukilinganisha na kikao kilichopita. Hii inamaanisha kwamba kwa kweli wenzetu hawa wanafanya kazi nzuri na wanajitahidi, na sote tunaamini kwamba idara hii siyo rahisi, idara yoyote ambayo inamgusa mwananchi moja kwa moja kwa kweli inakuwa ni idara nzito sana.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, basi tunastahili pale wizara au idara inapofanya vizuri tusiwe tunalalamika tu, lakini pale tunapoona kwamba mambo poa basi pia tuwasifu.

Nikiendelea Mhe. Mwenyekiti, na mchango wangu nije katika Kikosi cha Zima Moto na Uokozi. Mhe. Mwenyekiti, nimeona hapa malengo yao ni mazuri sana, lakini nije katika kipengele hiki cha kwanza ametwambia kwamba ana mpango wa kupunguza muda wa kuwahi kufika katika tukio la moto na majanga mengine bila ya kuzidi dakika 15.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani hii siyo rahisi sana, siamini kwamba kwa dakika 15 kweli tunaweza kufika katika maeneo ya tukio, hasa tukizingatia kwamba kutokana na mji wetu ulivyo, lakini pia maeneo mengine hayawezi kufikika kwa rahisi, kwa sababu kuna maeneo mengine yamejengwa *un planning*. Labda nikumbushe tu kipindi kilichopita kulitokea janga hili la moto, sasa wenzetu hawa wa Zimamoto walipokwenda kule gari yao ilikwama kati kati baina ya nyumba na nyumba. Kwa hivyo, gari ile ilishindwa kufika kwa haraka katika tukio baada ya ajali ile, ikabidi gari ile ivutwe huku na huku nyumba ikabomoka.

Mhe. Mwenyekiti, hii inaonesha kwamba bado wananchi wetu ni wakaidi wanajenga ovyo, wanajenga maeneo ambayo hayafikiki, *unplanned*. Kwa hiyo, naomba kutoa wito kwa wananchi wajitahidi na wao wajenge kwa mpangilio wasijenge sehemu zisizofikika, lakini pia tusifike hadi kwenye vianzio vya maji.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba sasa hivi tuna janga kubwa ambalo limefika katika maeneo ya mahoteli. Sote ni mashuhuda kwamba tumepata habari kuwa mahoteli kwa mujibu wa kitabu hiki wanasema, hoteli 25 za kitalii zimepata majanga haya ya moto. Sasa mimi nilitegemea Mhe. Waziri katika kitabu chake atatueleza mikakati gani ameiweka katika kuhakikisha haya mahoteli yetu tunawajengea vituo vya karibu ili kuepukana na janga hili au kupunguza.

Mhe. Mwenyekiti, Kaskazini tunacho kituo cha Zimamoto lakini kituo kile kina gari moja tu na gari yenyewe ndogo. Kwa hiyo, hata kama itakwenda katika sehemu ya tukio pengine moto hauwahi kuzimika gari ile imeshakwisha maji. Tunafahamu kwamba gari za Zimamoto maji yake yanatoka kwa kasi sana, sasa maji yale yanapokwisha katika gari ile inabidi waanze kazi ya kurudi kwenda kwenye kituo cha Zimamoto kwenda kuteka maji mengine.

Lakini jengine hata katika maeneo ya mjini, kweli idara hii ipo katika eneo la mjini lakini hata yenyewe ukiangalia unakuta wana vifaa pungufu. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri tuangalie Idara hii kuhakikisha kwamba yale mapungufu waliyokuwanayo basi tunayarekebisha ili idara hii waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije katika Chuo cha Mafunzo. Lengo la Chuo cha Mafunzo kwenda kuwafunza wale wanafunzi ili baadae wasirejee yale matendo mabaya ambayo waliyafanya mpaka kuwapelekea kuwekwa katika chuo kile. Lakini inaonekana sasa hivi adhabu inayotolewa katika vyuo hivyo ni dhaifu ukilinganisha na zamani. Hii inaonesha kwamba matukio haya ya wanafunzi au idadi pale vyuoni inaendelea kuwa kubwa siku hadi siku, ukiangalia siku za zamani wanafunzi wakitoka chuoni hapo wanakuwa wanajirekebisha na mambo yale mabaya, lakini sasa kinyume na hayo. Niseme pengine hii inatokana na hizo haki za binadamu, basi mimi nimuombe Mhe. Waziri kulingana na mazingira yetu ya nchi hii lazima adhabu zile ziongezwe, pamoja na kwamba tuna haki za binadamu lakini tusiziache kabisa.

Kwa sababu adhabu za sasa hivi wanazozipata wanafunzi labda tuseme ni kule kutengana tu na familia zao kuwa hawazioni kwa muda mrefu, kinyume cha hapo hakuna adhabu kubwa ambayo wanapata wanafunzi wale, na ndio maana baadae wanakwenda kufanya makubwa kuliko waliyoyafanya mwanzo. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri hilo aliangalie.

Jengine nije katika Manispaa yetu ya Mji. Mwenyekiti ili mji upendeze lazima tuwe na mipango miji, na mipango miji haiwezi ikaja yenyewe tu bila ya kupangwa na kutekelezwa. Mimi nishukuru taasisi kwa kuwekwa taasisi zinazoshughulikia mipango miji ambazo ni Taasisi ya Ardhi, wanacho kitengo na Taasisi ya Manispaa pia, lakini ukiangalia kiundani mipango yenyewe inakuwa haionekani.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamezungumza kuhusu Kituo cha Daladala cha Kisiwandui. Mimi sitaki kukizungumzia hicho, lakini naomba nizungumzie Kituo cha Daladala cha Michenzani ambacho sijamsikia Mjumbe kukizungumzia.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa kuona kwamba ipo haja ya kujenga mnara pale Michenzani, lakini pia kwa kuamua kutengeneza bustani ili watu wapumzike. Mtu baada ya kutoka kazini keshafanya kazi nzito basi akipenda kwenda pale atakwenda kupata upepo. Kwa kweli naipongeza sana serikali. Lakini hatujaangalia kwa upande wa pili wa mnara ule, haitapendeza kuona kwamba upande huu kuna mnara mzuri, miti mirefu inapendeza, bustani ya kijani inaonesha; inapendeza, lakini upande wa pili kuna yale makontena madogo madogo na msongamano wa daladala ambazo zinasimama pale.

Si hilo tu Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa undani hata pale kituo cha daladala mimi naamini kwamba serikali haijapanga kuwa daladala zisimame pale, kwa sababu kama imepangwa tungeona ile *cutting* ya barabara kuwa imeingia ndani kwa kuonesha ishara kwamba daladala zinatakiwa zi-*park* hapa, kwa kupanda wananchi lakini pia kwa kuteremsha.
Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri atapokuja kutoa majumuisho atueleze ana mpango gani wa kuhakikisha kwamba kuwa bustani nzuri, mnara mzuri, lakini upande wa pili uwe unapendeza mtu akipita pale aseme kweli hapa ni eneo la kupumzika. Mimi naamini kwamba inawezekana kujengwa majengo marefu pale, makubwa ili kuwasaidia wafanyabiashara wetu waweze kuweka biashara vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia mchango wangu nije katika ukurasa wa 48. Katika kitabu hiki Mhe. Waziri ametwambia kwamba amesimamia kilimo cha mpunga eka 9,857 zilizolimwa kwa kutumia jembe la mkono na ekari 7,457 zimelimwa kwa kutumia trekta. Kwa kweli hili jambo linasikitisha na la aibu, kwamba jembe la mkono wamelima ekari nyingi kuliko kutumia matrekta, na tunafahamu kwamba sasa hivi ni wakati wa sayansi na teknolojia, kila pahala sasa wanalima kwa kutumia matrekta. Sasa Mhe. Waziri hatuoni kuwa tunamuumiza mkulima wetu hapa? Bado tutaendelea kumuumiza huyu kwa kutumia jembe la mkono, hatimaye atapokuwa mzee mgongo utapinda kutokana na kutumia jembe hili la mkono. Mhe. Waziri hapa hii hesabu sijui kama imekosewa au vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu mdogo tu kwa kuheshimu muda wako nije katika Chuo cha Mafunzo kwenye ujenzi wa Chuo cha Mafunzo. Kitabu kilichopita Mhe. Waziri tuliona bajeti ya ujenzi, mara hii nimejitahidi sana kukisoma kwa umakini lakini hakuna bajeti ambayo inaonesha ujenzi wa jengo hili. Sasa sijui Mhe. Waziri amesahau au vipi. Kwa sababu mimi naamini kwamba walipoamua kujenga Chuo hiki wananchi na sisi humu ndani tulimpongeza sana Mhe. Waziri, kwa kusema kwamba Chuo cha Mafunzo cha sasa hivi kimepitwa na wakati, hata dunia nzima ukienda huwezi kukuta chuo kama kile. Kwanza sasa hivi kishazungukwa na mji, wananchi wanapita saa 24 katika chuo kile. Sasa wanafunzi hao wanaweza wakafunzwa pale? Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri atapokuja anieleze vizuri kwamba hili jengo limeishia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu mdogo tu nije katika hivi vikosi vyetu. Kuna sheria inaonesha kwamba mtu yeyote anapoajiriwa katika hivi vikosi akiwa mwanamke haruhusiwi kwa miaka mitatu kuolewa. Na sisi tunaamini kwamba mtoto wa kike yeyote akitimiza umri wa kuolewa lazima afanye tendo la ndoa.

Sasa Mheshimiwa hatuoni kwamba kumzuia mtoto huyu wa kike kwa miaka mitatu si tunaweza kumhatarisha na janga hili la Ukimwi? Lakini vile vile hatuoni kwamba anaweza akafanya kitendo cha ngono kiholela? Kwa hiyo, mimi namuomba Mhe. Waziri apunguze sheria hii isiwe miaka mitatu ili akina dada hawa watapoajiriwa waweze kuolewa labda wajikinge tu wasipate mimba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ. Kwa kweli Vikosi vya SMZ ni askari kama askari wengine wowote wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hali ya matumizi ya vikosi hivi ni ngumu sana, hasa kwa wakati huu tunaokwenda nao wa utandawazi; kwamba vikosi vyote vya Tanzania vinapatiwa majenzi ya *quarter***,** askari anatakiwa ahakikishe anakaa na familia yake kila wakati wakati wa amani. Sasa utashangaa sana vikosi vyetu vya SMZ ni vingi ambavyo havina *married quarter* wakati askari anatakiwa wakati wa amani aweze kukaa na familia yake.

Naomba Mhe. Waziri atapokuja anihakikishie ni lini vikosi vyetu vitakuwa na *quarter* katika kambi zao. Kwa sababu nimechunguza katika kambi nyingi za vikosi hivi kuanzia KMKM, Zimamoto, KVZ, JKU na vyengine, isipokuwa Mafunzo peke yake ndio yenye *quarter* na zimejengwa tangu wakati wa ukoloni zote zimeshakuwa mbovu. Namshauri Mhe. Waziri wapatiwe *quarter* tena ziwe za kileo, zinazokwenda na wakati kama vilivyo vikosi vyengine vya Tanzania. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kuhusu vikosi vyetu hivi jinsi vinavyoendelea na kazi nzuri za mfano katika Jeshi letu la Tanzania. Kwa sababu vikosi hivi hatuwezi kuviteua kusema kwamba si vikosi vya Tanzania, hivi ni vikosi vya Tanzania ingawa viko Zanzibar, ninafahamu wazi kwamba vikosi hivi katika mapambano ya vikosi vya Tanzania tulikuwanavyo bega kwa bega wakati wa vita. Sasa hakuna sababu vikosi hivi vikapewa silaha maalum za kulindia, vinahitaji kupata zana za kisasa kama lilivyo Jeshi letu la Tanzania.

Hivi sasa kuna vikosi vinaonekana vya kileo ambapo juzi tumetimiza miaka 50 ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar vimeonesha maendeleo ya vikosi vya sasa ambavyo vina vitu vya kileo. Tukaangalia kuhusu mambo ya vifaru, magari, zana za kivita na mambo mengine. Hakuna sababu ya kwamba vikosi vyetu hivi vya JKU na vyengine, kuwa hivi sasa vishindwe kuwa na silaha za aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia Kikosi chetu cha KMKM ni kikosi ambacho kinategemewa sana katika mambo ya magendo; ambacho sasa hivi kina boti za kisasa zinazoweza kufukuza boti nyengine zinazoweza kubeba vitu vyetu vya uchumi kama karafuu. Vikosi hivi sasa vinapaswa kupatiwa zana nyengine za kisasa kama vile helikopta ambazo zinaweza kufukuza vile vyombo vinavyokwenda kwa *speed* kuliko hata boti zetu za KMKM. Kikosi hiki kama kinataka kununuliwa boti mbili hatuwezi kukosa helikopta moja, tuhakikishe vikosi hivi vinakwenda na wakati ili kupambana na maadui wote wa Tanzania pamoja na magendo ili kufanya majukumu yake na kuhakikisha kwamba uchumi wetu haupotei katika nchi yetu.

Vile vile nikienda katika ukurasa wa 78 Vikosi vya KVZ. Vikosi hivi ni vikosi mama ambavyo vimeanzishwa muda mrefu sana, wakati wa *ASP* ni kikosi cha kwanza Zanzibar kilichokuwa kinalinda hadhi yetu katika nchi ya Zanzibar. Kikosi hiki ni vyema kikapewa silaha ambazo zinatoa ulinzi mzuri katika nchi yetu, zana ndogo ndogo sasa wasitumie na watumie zile *light machine gun, heavy machine gun, RPG* ambazo zinahakikisha ulinzi wa uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika ukurasa wa 65; Jeshi la Kujenga Uchumi. Jeshi hili ndilo tulilioliweka katika hali ya kujiendeleza kuhakikisha kwamba linaendelea sana katika hali ya uchumi, tuone kwamba linapata zana za kisasa hasa mambo ya matrekta ili uchumi wetu uende sambamba na hali ya maisha ya kileo. Tukiangalia kikosi hiki kimezoea mambo ya porini, hivyo kipewe silaha za kileo ili kujilinda na kulinda nchi yetu katika mambo

ya porini. Hivyo, kikosi hiki tujue kwamba ni kikosi chetu tunaweza kukiweka cha hakiba na kukipatia silaha za kileo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika ukurasa wa 73 kifungu 187 kuhusu kikosi chetu cha Zimamoto. Namuomba Mhe. Waziri kikosi hiki nacho kiweze kupata magari ya kileo ambayo yana winji kubwa kuweza kurusha maji katika nyumba za ghorofa hata kumi, ili kutoa huduma za kileo na za kisasa. Vile vile kiweze kupatiwa magari ambayo yanaweza kubeba maji mengi kuliko kumaliza maji wakati wa janga la moto linapotokea na kuepukana na kwenda kuchota maji mengine. Kwa mfano, hivi sasa kikosi hiki kina gari moja tu la kubeba maji, hivyo kuwe na gari zaidi ya tano za kuzimia moto. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hali ya usafi wa nchi yetu kwa ndugu zetu wa Manispaa. Kwa kweli Manispaa hapa Zanzibar bado iko katika hali ngumu ya usafi. Mara nyingi majanga ya miripuko yanatokea kutokana na kwamba nchi yetu haijawa na usafi wa mji wake. Ningelipendekeza atapokuja Mhe. Waziri anihakikishie ni lini watu wetu wa Manispaa watapata kwenda nje kusomea usafi ili tulingane na nchi za wenzetu?

Kwa kweli nchi yetu ni nchi ambayo watalii wanakuja sana, lakini utakuta sehemu nyingi unazopita ni harufu tupu; ambapo Manispaa inashindwa kutekeleza wajibu wake. Ningeomba watu wa Manispaa wakapatiwa masomo kuhakikisha wanafanya usafi na kusoma sio lazima kusoma kwa buku, kusoma kutembea. Hivyo, iko haja kwamba watu hawa wafanyiwe ziara maalum za kupita katika nchi mbali mbali kuona usafi unafanywa vipi, si lazima kwenda nje lakini hata hapa hapa Tanzania kuna mikoa mingi tu ina sifa ya usafi.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda Moshi utaona kuna sifa ya usafi, Arusha nako ni safi kunapigiwa mfano na hivi juzi tulikuwa Dodoma huko nako kwa kweli kunasifika sana kwa usafi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atoe nafasi maalum au ofa kwa wafanyakazi wa Manispaa kama 300 au 200 wagaiwe makundi kwenda katika mikoa yetu kuona hali ya usafi.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na wakati wako sitozungumza sana zaidi ya hayo, lakini namshauri Mhe. Waziri anapokuja atuhakikishie kwamba vikosi vyetu vinakwenda na wakati wa leo hasa kwa mambo ya ulinzi, vikosi vidhibitiwe na wao wapatiwe maposho yao wanapokwenda likizo na mambo mengine yote yanayofaa kupata vikosi hivyo katika majeshi yetu ya Tanzania. Isiwe vikosi hivi vimepewa nafasi ndogo ya ulinzi kumbe wanafanya kazi kubwa.

Ahsante Mwenyekiti kwa haya naunga mkono kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa naona makofi mengi yanapigwa juu yako. Waheshimiwa Wajumbe nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu wenu, tukijaaliwa kesho baada ya maswali na majibu tutamaliza wizara hii.

Waheshimiwa Wajumbe naakhirisha kikao hiki mpaka kesho tarehe 03/06/2014 saa tatu asubuhi.

(Saa 1:45 Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 03/06/2014 saa 3:00 asubuhi)